# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA TANO

**Kikao cha Tano – Tarehe 6 Novemba, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## DUA

*Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 53

**Mgao wa Fedha za *TACAIDS***

**MHE. VICTOR KILASILE MWAMBALASWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali pamoja na wahisani mbalimbali imeongeza maradufu mchango wake kwenye Taasisi ya Kupambana na UKIMWI (*TACAIDS*), na kwa kuwa Taasisi hiyo hivi sasa inapeleka fedha hizo kwenye Mikoa na Wilaya.

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha hizo kilipelekwa katika kila Wilaya kwenye Mkoa wa Mbeya kwa miezi mitatu iliyopita?

(b) Je, ni vigezo gani vinatumika katika kugawa fedha hizo Kiwilaya?

(c) Je, ni kwa nini *TACAIDS* hawaitumii Taasisi ya *TASAF* kupeleka fedha kwa walengwa maana *TASAF* ina mafanikio makubwa kwa hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI (MHE. DR. LUKA J. SIYAME)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa Mbunge wa Lupa, naomba kutoa maelezo ya ufafanuzi kama ifuatavyo:

Udhibiti wa UKIMWI na athari zake ni shughuli ya Taifa zima pamoja na Wahisani waliomo ndani ya nchi. Kazi kuu ya *TACAIDS* ni kuratibu shughuli ili ziendane na Sera ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI na Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI. Kugawa na kusimamia matumizi ya fedha ni sehemu tu ya kazi hiyo. Fedha hizo zinatoka sehemu mbalimbali na kwa njia mbalimbali. Baadhi zinapitia *TACAIDS,* na nyingine hazipiti huko. Kwa hiyo, msaada unaotolewa si lazima upitie *TACAIDS* na pengine katika uratibu aliyepata fedha kutoka upande mmoja anaweza asipate kutoka upande mwingine. Kwa hiyo, mhitaji anaweza asipate fedha kutoka *TACAIDS* akapata kutoka chanzo kingine, zote zikiwa ni za udhibiti wa UKIMWII, ikumbukwe pia kwamba *TACAIDS* hutoa fedha kwa Mikoa na Wilaya kulingana na umuhimu wa maombi ya mipango yao. Mipango hiyo inafanyiwa tathimini ili kuona ubora wake hususan katika kubhibiti maambukizo ya virusi vya UKIMWI kwa walengwa, kuhudumia waishio na virusi vya UKIMWI na yatima, na taarifa ya matumizi ya fedha zilizowahi kutolewa kabla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miezi mitatu iliyopita, hakuna fedha zilizopelekwa kwa Taasis za kiraia Mkoani Mbeya kupitia Wakala *GTZ.* Sababu za kutofadhili asasi za kiraia kwa kipindi hicho zinatokana na ukweli kwamba wakala *GTZ* alianza kazi ya uwakala mwezi Aprili 2005 na alishatoa fedha kwa baadhi ya asasi za kiraia zilizopo Mkoani Mbeya na utekelezaji unaendelea. Hivi sasa yuko kwenye mchakato wa kuchambua mipango ya asasi nyingine katika mkoa huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, fedha zilizopelekwa Mkoani Mbeya kwa miezi mitatu iliyopita ni kama ifuatavyo:-

(i) Jiji la Mbeya Sh. 16,992,000;
(ii) Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya Sh. 33,814,100;
(iii) Halmashauri ya Wilaya ya Chunya Sh. 15,856,000;
(iv) Halmashauri ya Wilaya ya Ileje Sh. 40,982,400;
(v) Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali Sh. 35,829,100;
(vi) Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi Sh. 20,529,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utoaji wa Fedha umekuwa ukifanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wake kutoka kwenye vyanzo husika. Kwa mfano, mgao wa fedha kwa Halmashauri za Wilaya za Kyela na Rungwe Mkoani Mbeya na nyinginezo katika mikoa mingine utatolewa mara baada ya fedha kupatikana.

Fedha kutoka Mfuko wa Dunia kwa ajili ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria zilizopelekwa Mkoani Mbeya ni kama ifuatavyo:

(i) *Mbeya Referral Hospital* Sh. 359,992,248;
(ii) *Mbeya Municipal Council* Sh. 43,014,772;

(iii) *Mbeya Regional Hospital(RHMT)* Sh. 58,059,941;
(iv) *Mbeya District Council (CHMT)* Sh. 40,355,603;
(v) *Mbozi District Council (CHMT)* Sh. 47,989,737;
(vi) *Mbarali District Council (CHMT)* Sh.57,195,422;
(vii) *Ileje District Council (CHMT)* Sh. 30,309,393;
(viii) *Rungwe District Council (CHMT)* Sh.36,536,404;
(ix) *Chunya District Council (CHMT)* Sh. 33,745,014;
(x) *Kyela District Council (CHMT)* Sh. 60,878,099.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika maelezo ya awali, fedha, hutolewa kwa Wilaya na Asasi za kiraia kulingana na maombi ambayo hufanyiwa tathimini na halmashauri husika na *TACAIDS,* na upatikanaji wa taarifa ya matumizi ya fedha zilizowahi kutolewa.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, *TACAIDS* hutumia njia mbalimbali kupeleka fedha wa walengwa. Uzoefu wa *TASAF* ni mzuri sana. *TACAIDS* inawasiliana na *TASAF* ili kuziwezesha jamii kuibua matatizo ya UKIMWI miongoni mwao na hivyo kuziwezesha kupewa fedha kwa ajili ya udhibiti wa tatizo hilo.

**MHE. DR. HARRISON GEORGE MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili mafupi mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wilaya ya Kyela Mkoani Mbeya inaongoza kwa maambukizi ya UKIMWI lakini si kwa Mkoa wa Mbeya tu bali Kitaifa vilevile, ni taarifa zipi za ziada zinahitajika ziifikie *TACAIDS* ili Wilaya ya Kyela iweze kupewa kipaumbele? Nakata kuelewa ni kiasi gani.

**MWENYEKITI – MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Dr. Mwakyembe kwa sababu ni swali la nyongeza unatakiwa kuuliza swali moja tu la nyongeza.

**MHE. DR. HARRISON GEORGE MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI (MHE. DR. LUKA J. SIYAME):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe, Mbunge wa Kyela kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nimemsikia vizuri alikuwa anauliza kama ni taarifa zipi zinatakiwa kufikia wilaya ya Kyela ili kuweza kupelekewa hizo pesa, sijui kama niko sahihi.

Kama hivyo ndivyo, taarifa zinazohitajika kufika wilaya ya Kyela kwa kweli zote zinapitia wakala ambaye ni *GTZ* kwa Mkoa wa Mbeya na kwa hali hiyo *GTZ* ndiye ambayo inapeleka taarifa zote kutoka kwenye asasi au taasis zilizopo Mkoani Mbeya kwa *TACAIDS* na baada ya hapo *TACAIDS* huchambua hizo taarifa ambazo ni muhimu na kupeleka hizo fedha kwa hiyo *GTZ* ambayo hupeleka hizo fedha kwenye hizo asasi kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kyela.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kwa kuwa majibu yamechukua karibu dakika tano nzima basi naomba tuendelee na swali linalofuata.

Na. 54

**Dampo Lililopo Mtoni kwa Azizi Ali**

**MHE. COSMAS MASOLWA COSMAS** aliuliza:-

Kwa kuwa, dampo lililopo Mtoni kwa Azizi Ali liliwekwa na Jiji na kuvamia mashamba ya watu pasipo ridhaa yao au kulipwa fidia ya mashamba yao, na kwa kuwa dampo hilo limekuwa ni kero kubwa kiafya kwa wakazi wa eneo hilo pamoja na viumbe wa baharini kwa vile uchafu wenye sumu hutiririka kuelekea baharini:

(a) Je, Serikali inatambua kuwa, wananchi walinyang’anywa mashamba yao kwa nguvu tena bila kulipwa fidia zao zinazostahili wakati wa kuanzishwa kwa dampo hilo?

(b) Je, ni madhara gani ya kiafya kwa binadamu yanayosababishwa na kuwepo kwa uchafu huo mbali na harufu mbaya inayotokana na uchafu wa takataka zinazokusanywa hapo?

(c) Je, serikali ina mikakati gani ya kuliboresha au kuliondosha kabisa dampo hilo hatari ili kukoa afya na maisha ya wananchi waishio karibu na dampo hilo pamoja na viumbe wa baharini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cosmas Masolwa, Mbunge wa Jimbo la Bububu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Dampo la Mtoni kwa Azizi Ali lilianzishwa rasmi tarehe 05/01/2001 baada ya wananchi wa eneo husika kwa kupitia vikao halali kuiomba Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ilitumie eneo hilo kwa kumwaga taka kuzuia mmomonyoko uliokuwepo na ambao ulianza kuharibu nyumba za baadhi ya wananchi.

Hivyo taka ngumu zilitumika kuinua eneo lililoathiriwa. Halmashauri ilitenga viwanja saba (7) sehemu za Buza (Temeke) na kuvigawa kwa familia saba ambazo nyumba zao ziliathiriwa vibaya. Hivyo, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam haikuvamia wala kunyang'anya mashamba ya wananchi na hakuna mwananchi aliyetakiwa kulipwa fidia kwa dampo hilo kuwekwa katika eneo hilo.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, madhara yatakayopatikana kiafya kwa wananchi iwapo dampo hilo havitadhibitiwa ni pamoja na :-

- Athari ya macho na kikohozi kwa sababu ya vumbi na moshi

- Mazalia ya wadudu waletao magonjwa

- Hatari ya moto kuunguza mali na viumbe haiHata hivyo athari hizo zinadhibitiwa kama ifuatavyo:-

- Kutumia mitambo ya kusambaza na kusindilia taka;

- Kufukia taka kwa udongo;

- Kupulizia dawa za kuua mazalia ya wadudu;

- Kupunguza vumbi kwa kumwagilia maji na kuboresha barabara inayokwenda dampo la Mtoni; na

- Kuwa na kikosi cha kuzima moto

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ina mpango wa Kuanzisha eneo maalum la kutupa taka ngumu huko Pugu na Kinyerezi (Ilala). Eneo hili limeonekana linafaa baada ya kutathimini athari za mazingira na mali za watu. Eneo jingine ni Chamazi na Mbande, (Temeke). Eneo la Kisopwa katika Manispaa ya Kinondoni linafanyiwa utafiti ili kuwepo na dampo. Vilevile Halmashauri zimeanzisha mradi wa umeme kwa kutumia gesi itokanayo na taka kwa kushirikiana na kampuni toka Italia. Ni mategemeo yetu kuwa mipango hii ikikamilika tatizo la dampo na hatari za maisha ya watu na mazingira litapungua.

**MHE. COSMAS MASOLWA COSMAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Pamoja na maelezo yako ni swali moja la nyongeza.

Kwa sababu amesema kwamba Serikali ina mpango wa kuanzisha Dampo lingine huko Kinyerezi lakini kwa mujibu wa maelezo kwenye *TV* wananchi wa eneo hilo wnalalamika kwamba Dampo hilo lisianzishwe. Je, Serikali ina mpango gani wa kutafuta maeneo ambayo hayana mgogoro na kuyahifadhi ili wananchi wasiendelee kupata madhara?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA :** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Masolwa kama ifuatavyo:-

Kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi ni kwamba hayo maeneo yanafanyiwa kwanza utafiti, kuongea na wananchi na kuangalia mazingira kama yanaruhusu. Iwapo kama Serikali itaona kwamba mazingira hayaruhusu na wananchi wa sehemu hiyo hawaafikiani na Serikali kuhusu kufanya sehemu hiyo ni Dampo, Serikali itaamua na itatafuta sehemu nyingine, sehemu bado zipo na tunafanya utafiti wa kina kuhakikisha kwamba haziathiri wananchi na wala hazileti madhara kwa wananchi.

Na. 55

**Utaratibu wa Kuandikisha Magari**

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imeanzisha utaratibu wa kuandikisha magari *Number Plates* kwa mtindo mpya tangu mwaka 2004, na kwa kuwa mfumo huo mpya umeanza kwa herufi T ikifuatiwa na tarakimu halafu tena herufi nyingine tatu:

(a) Je, tafsiri halisi ya herufi hizo ni nini, na kwamba kwa vile nchi nyingi zenye mfumo kama huo wa kuweka *Number Plates* zinasaidia hasa wakati wa uhalifu kutambua gari husika limeandikishwa na nchi gani, mji gani na kwamba utaratibu tulioanzisha hapa Tanzania unasaidia vipi kutambua gari hilo ni la eneo gani?

(b) Kwa kuwa, uandikishwaji huo umetolewa kwa magari ya nchi nzima kwa kampuni moja. Je, Serikali imejifunza ni faida na hasara au matatizo gani yanatokana na kuwa na kampuni moja tu kwa nchi nzima?

(c) Je, ni nini hasa lengo la kulipia *Number Plates* kila mwaka, kwani Serikali haioni kuwa ushuru/malipo hayo ni sehemu ya ushuru unaoleta usumbufu kwa watumiaji na kuwachukulia fedha zao bila sababu za msingi na kwamba, ni nchi ngapi duniani zina utaratibu wa kutoa *Number Plates* kila mwaka?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Wilbrod Peter Slaa, Mbunge wa Karatu, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kila chombo cha moto kinachosajiliwa katika mfumo mpya wa kuandikisha magari kinapewa namba mpya katika utaratibu wa tarakimu na herufi mfano T 100 AAA. Herufi T inamaanisha nchi ya Tanzania ikifuatiwa na tarakimu tatu na herufi tatu ambazo zinatofautiana utambulisho wa gari moja na gari jingine. Usajili unaofanywa ni wa kitaifa, hakuna utaratibu wa kusajili chombo cha moto Kimkoa au Wilaya. Mfumo huu umesaidia sana Jeshi la Polisi kupata taarifa muhimu hususani wakati wa uhalifu kutambua gari husika limesajiliwa kwenye kituo gani, wakati gani na

linamilikiwa na nani. Taarifa hizi husaidia Jeshi la Polisi kufuatilia gari iliyohusika katika tukio na kuchukua hatua zinazostahili. Utaratibu huu wa kuwa na mtengenezaji mmoja wa vibao vya nambari za usajili hutumika pia na nchi kama Kenya na Sweden.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha shughuli za kiutawala na kudhibiti wimbi la wizi wa magari. Serikali iliamua kumteua mtengenezaji mmoja tu wa vibao vya namba za usajili. Vibao vinatengenezwa kwa mfumo na viwango vya kitaifa na kimataifa kwa maagizo toka kwa Serikali ikisaidiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Mtengenezaji huyo ameunganishwa kwenye mtandao wa mfumo mzima wa usajili wa magari ili aweze kufanikisha majukumu yake kirahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mfumo huu Serikali imeweza kupata faida zifuatazo; kuongeza mapato yake zaidi kwa vile mfumo huu unazuia udanganyifu unaoweza kufanywa na watu ambao si waaminifu. Kutokana na mfumo huu Serikali imeweza kusajili magari 290,572 na kukusanya jumla ya shilingi bilioni 22,325.9.

Aidha, Serikali imefanikiwa kuboresha shughuli za utawala wa kodi katika usajili wa magari, kudhibiti uingizaji holela wa magari bila ya kufuata sheria, kupunguza wimbi la wizi wa magari na kuboresha huduma kwa wenye magari kuondoa usumbufu usiokuwa wa lazima. Aidha, Serikali pia imejifunza kutokana na matatizo yaliyotokeza katika utekelezaji wa mfumo huu, kwa mfano vibao vya namba za usajili kuchelewa kumfikia mhusika kwa muda unaotakiwa kwa sababu ya ukubwa wa nchi yetu. Hata hivyo, Serikali kwa kupitia Mamlaka ya Mapato imekuwa ikiboresha mfumo mzima wa utengenezaji na usambazaji wa vibao vya namba ili viwafikie wahusika kwa urahisi.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wetu wa usajili wa magari hauna Utaratibu au Sheria ya kulipia vibao vya namba za usajili kila mwaka. Vibao vya namba za usajili hulipiwa mara moja tu pale chombo cha moto kinaposajiliwa kwa mara ya kwanza. Baada ya hapo vibao hivyo hulipiwa endapo vitaharibika au kupotea yaani *replacement*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utaratibu huu, mwenye gari anatakiwa kuchangia gharama za uendeshaji kwa kupilia ada ya kila mwaka (*motor vehicle annual fee*) ya shilingi 20,000/= tu. Utaratibu wa kulipa ada ya mwaka kwa wenye magari umekuwa ukitumika katika nchi nyingi duniani kwa m fano Uingereza, Sweden, Zambia, Malawi, Uganda, Botswana na kadhalika.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Aidha nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake ya kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Waziri ameeleza kwamba utaratibu huu unasaidia sana polisi katika kuwanasa wahalifu, lakini kwa kuwa wananchi pia ni sehemu muhimu kuwapa Polisi taarifa muhimu kuhusu uhalifu hasa wa magari.

Je, ni kwa kiwango gani Waziri atakubaliana kwamba kuandika magari haya kwa mtindo wa mikoa utarahisisha wananchi kutambua magari haya yamesajiliwa wapi na hivyo waweze kuisaidia Polisi?

Pili, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba utaratibu wa sasa wa kuandikishwa na mtu mmoja tu kumeleta ucheleweshaji mkubwa. Je, Serikali itafanya utaratibu gani mtu huyu huyu mmoja angalau afungue ofisi zake katika mikoa ili kuwaondolewa wananchi usumbufu na ucheleweshaj?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dr. Wilbrod Peter Slaa, kama ifuatavyo.

Ni kweli kimkoa ingekuwa ni rahisi kwa wananchi kujua vilevile lakini kwa sasa kama nilivyosema hali tunaiboresha ili kuhakikisha kwamba usajili uko mahali pamoja tu tuangalie baadaye baada ya kuona *volume* ya magari imekuwa nyingi zaidi katika Mkoa au katika Wilaya tunaweza kuliangalia hilo lakini kwa sasa ucheleweshaji si mkubwa sana.

Kuhusu mwananchi kutambua nambari za magari nadhani hili halina utata au kumpa mtu mmoja afanye hizi shughuli ni sawasawa vilevile hatutaki kuwe na watu kuweza kughushi zile namba, tunataka mtu mmoja na mtandao wetu huo huo wa kompyuta tunawasiliana naye palepale. Lakini kwa sasa kwa kuwapa watu chungu nzima inaweza kuleta matatizo ya kughushi.

**MHE. RAYNALD ALFONS MROPE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa, Serikali imeamua kutoza shilingi 22,000/= kwa ajili ya *Annual Fee* katika hizi *Number Plates* au magari, ningependa kuuliza kwa nini kusiwe na utaratibu ambapo mwenye gari anapolipa Bima kwa nini asilipie hiyo *Annual Fee* wakati huohuo anapolipia Bima badala ya kwenda kupiga foleni ofisi za *TRA* ili kuweza kupata hiyo kodi kama ilivyotakiwa kisheria?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Raynald Mrope kama ifuatavyo:-

Bima inalipiwa kwenye Kampuni ambayo si *excess* ya Serikali, Taasis yetu ya Kiserikali ya kupokea hizi fedha na malipo ya 20,000/= na siyo 22,000/= ni *TRA,* kwa hiyo mnapokwenda kulipia Bima ni tofauti kabisa.

Mfumo huo vilevule uko Zanzibar kila mwaka wenye magari wanalipia *Road Licence* na Bima inalipwa mbali na ile *Road Licence* ya kila mwaka inalipwa mbali.

Na. 56

**Umilikaji wa Silaha**

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS** aliuliza:-

Kwa kuwa, suala la ujambazi linaonekana kushamiri nchini mwetu na kwamba maeneo yote yanaweza kulengwa na wahalifu hao:

(a) Je, ni lini Serikali itabadilisha Sheria ya umilikaji wa silaha za kujilinda kwa Tanzania Zanzibar na Tanzania Bara?

(b) Je, ni njia gani nyepesi ambazo raia wanapaswa kuzitumia ili kuweza kupata kibali cha kununua silaha za kujilinda?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani, swali lake lenye sehemu (a) na (b) napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu la kulinda usalama wa raia na mali zao ni la Serikali kupitia polisi na vyombo vingine vya Dola.

Hivyo Serikali inafanya jitihada za kuimarisha usalama wa wananchi na ma mali zao kwa kuboresha na kuliwezesha Jeshi la Polisi kufanyakazi zao kwa ufanisi zaidi kwa lengo la kutokomeza kabisa wimbi la ujambazi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini ya Wizara yangu kwamba kufuatia uboreshaji huo, haja ya watu binafsi kumiliki silaha kwa ajili ya kujilinda itapungua.

Aidha, uzoefu unaonyesha kwamba baadhi ya raia hawatunzi vizuri silaha ambazo wamemilikishwa kihalali na matokeo yake ni kwamba silaha hizo huangukia mikononi mwa wahalifu ambao hutumia silaha hizo kutenda makosa ya mauaji na ujambazi na pengine majambazi wanapojua raia anamiliki silaha huamua kumuua kwanza kabla mtu huyo hajaitumia silaha yake kujilinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi linalofanywa na Wizara yangu kupitia Jeshi la Polisi la kuandikisha na kuhakiki upya silaha zinazomilikiwa na raia limeiwezesha Serikali kubaini mambo mengi ambayo ni kinyume na taratibu za umilikaji silaha. Zoezi hilo likikamilika hatua mbalimbali zitachukuliwa kurekebisha kasoro hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria inayotumika ya umilikaji na matumizi ya silaha kwa raia nchini Tanzania ni *Arms and Ammunition Act No. 2/1991.* Sheria hii inatumika kwa upande wa Tanzania Bara. Kwa upande wa Tanzania Visiwani hivi sasa hakuna sheria inayoruhusu raia kumiliki silaha.

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kueleza katika maelezo yangu ya utangulizi, baada ya zoezi la kuandikisha na kuhakiki silaha kwa raia kukamilika Serikali kupitia Jeshi la Polisi inakusudia kuifanyia marekebisho Sheria Namba 2 ya Mwaka 1991 ili iendane na wakati na mahitaji ya sasa kwa kufuata miongozo iliyopo katika itifaki na maazimio mbalimbali ya Kikanda na Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna njia yoyote nyepesi inayoweza kutumika ili kupata kibali cha kununua na kumiliki silaha kila anayetaka kununua na kumiliki silaha ni lazima afuate taratibu zote ambazo zimeainishwa wazi katika Sheria ya *Arms and Ammunition Act* Namba 2 ya Mwaka 1991. Sheria inamtaka mwombaji atume maombi yake kupitia Kamati za Ulinzi na Usalama kuanzia ngazi ya Kijiji au Mtaa, Wilaya na Mkoa anaoishi mwombaji. Baada ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa kuridhia maombi hayo, kuwasilishwa kwa Kamanda wa Polisi wa Mkoa ambaye hutoa kibali cha kumiliki silaha kulingana na aina ya silaha. Iwapo silaha hiyo ni bastola Kamanda wa Polisi wa Mkoa hupeleka maombi hayo kwa Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai *(DCI)* Makao Makuu ya Polisi ambaye ndiye mwenye dhamana ya kutoa kibali cha kumiliki silaha ya aina hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumalizia kwa kuwaomba wananchi wanaomiliki silaha kuzitunza ipasavyo ili zisiangukie mikononi mwa wahalifu na kutumika kinyume na madhumuni yake. Aidha, natoa wito kwa wananchi ambao

hawajapeleka silaha zao kuhakikiwa na kuandikishwa upya wafanye hivyo mapema ili kuiwezesha Serikali kuendelea na hatua za marekebisho ya Sheria namba 2 ya mwaka 1991 ya Umiliki wa Silaha Nchini.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza suala moja tu la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa mimi naamini kwamba wimbi la uhalifu limeshamiri kule Zanzibar limesababishwa kwa namna moja au nyingine au ukweli kwamba wahalifu wanaelewa kuwa wale waliofanyiwa uhalifu hawana aina yoyote ya silaha ya kujilinda. Je, Serikali kwa maana Jeshi la Polisi itakubali ukweli kwamba kuchelewa kuwapatia silaha Wazanzibar kunachangia katika kuimarisha ili wimbi la mauaji na wizi linalofanywa na wahalifu hao?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sikubaliani na Mheshimiwa Salim kwamba kwa sababu sheria ya Tanzania Zanzibar haimruhusu raia kumiliki silaha na hicho kuwa chanzo kikubwa cha uhalifu kule Zanzibar. Hata hapa Bara ambapo ruhusa inatolewa ya kumiliki silaha bado uhalifu upo na maeneo mbalimbali mmeona yakitokea hayo. Cha msingi ni kuhakikisha kwamba wananchi wanashirikiana na Jeshi la Polisi kutoa taarifa pale ambapo wanaona wahalifu wanaendeleza vitendo hivyo. Hatua mbalimbali zimechukuliwa kwa upande wa Tanzania Zanzibar kuhakikisha kwamba usalama unakuwepo. Hivi sasa Jeshi la Polisi limejipanga vizuri na nyote ni mashahidi kwamba sasa hivi hali ya uhalifu kule Zanzibar imedhibitiwa ipasavyo. *(Makofi)*

**MHE. FATMA MUSSA MAGHIMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kumwuliza Naibu Waziri swali lifuatalo. Kwa kuwa silaha ni kitu cha hatari sana. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapima akili na viburi wale wanaopewa silaha? *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema awali hatua mbalimbali za hadhari huchukuliwa kabla mtu kupewa ruhusa ya kumiliki silaha na wafuatao hawaruhusiwi kumiliki silaha wakiwemo wendawazimu, watoto wenye umri chini ya miaka 18, wasiojiweza, wenye rekodi ya uhalifu, watu wasio na akili timamu hao ndio kabisa hawapewi kibali cha kumiliki silaha.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa silaha ni chombo hatari sana. Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa mafunzo kwa wale wote wanaomiliki silaha ili waweze kujua jinsi ya kuzitumia vizuri na pia kupata nidhamu ya kutumia silaha. Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na ushauri wa Mheshimiwa Kimaro kwamba upo umuhimu wa kuongeza mafunzo kwa wale ambao wanamiliki silaha na ndiyo maana nikasema sasa hivi nataka kufanya maboresho katika sheria yetu ili mambo mengine tuyaangalie yale ambayo yataleta udhibiti katika umiliki wa silaha. Jambo lake la msingi hivi sasa linafanyiwa

kazi na ninawahakikishia wananchi wote wa Tanzania kwamba wale watakaopewa kumiliki silaha ni wale tu wanaopaswa kupewa silaha hizo.

Na. 57

**Ujambazi wa Kutumia Silaha Zanzibar**

**MHE. FATMA ABDALLAH TAMIM** aliuliza:-

Kwa kuwa, ujambazi wa kutumia silaha umeshamiri katika Kisiwa cha Zanzibar:-

(a) Je, Serikali inafahamu ni majambazi wangapi yaliyokamatwa yakitumia silaha au kufanya uhalifu;

(b) Je, kesi ngapi zinazohusu utumiaji wa silaha zimetolewa maamuzi na ni kesi ngapi bado hazijatolewa maamuzi?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Abdallah Tamim, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi, swali lake lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya matukio 20 ya ujambazi wa kutumia silaha yaliripotiwa katika Visiwa vya Zanzibar kati ya kipindi cha Januari – Oktoba, 2006. Katika matukio hayo jumla ya majambazi 22 yamekamatwa na kesi kumi na moja (11) ziko Mahakamani. Mpaka sasa hakuna kesi yoyote ambayo imeshatolewa uamuzi. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba hatua mbalimbali zimekwisha chukuliwa na hali ya usalama katika Kisiwa cha Zanzibar inaendelea kudhibitiwa. Aidha, naomba kuchukua nafasi hii kuwaondoa wasi wasi wananchi wa Zanzibar kwamba hali ni shwari, na Serikali kupitia Jeshi la Polisi imejipanga vyema ili kupambana na uhalifu wa aina zote katika visiwa vya Zanzibar na Tanzania kwa jumla.

**MHE. FATMA ABDALLAH TAMIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kumwuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba ucheleweshaji wa kesi ndiko kunakosababishwa ongezeko la ujambazi?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuongezeka kwa ujambazi ni tamaa za kimaumbile za wanadamu wenyewe. Kwa kiasi fulani inaweza pia ucheleweshaji wa kesi unaweza kuchangia kuongeza kwa uhalifu lakini kwa asilimia ndogo sana hasa inatokana na tamaa za wanadamu wenyewe za kutaka kipato cha haraka kwa njia zisizo halali, ndiyo chanzo kikubwa kilichopelekea kuongezeka kwa ujambazi hapa nchini.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Usalama wa Raia kwa majibu yake lakini nina swali moja la nyongeza.

Kwa sababu amesema kwamba hali ya ujambazi nakubaliana kwamba ni mbaya kule Zanzibar lakini inaendelea kudhibitiwa. Hivyo anaweza kulieleza Bunge hili Tukufu ni sehemu gani kule Zanzibar kati ya Unguja na Pemba yenye kesi nyingi za ujambazi?

**MWENYEKITI**: Ni swali linalohusu idadi sijui …..

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya Mjini Magharibi matokeo yaliyotokea yalikuwa sita (6) katika kipindi cha Januari mpaka Oktoba 2006. Kaskazini Unguja hakuna tukio lolote. Kusini Unguja matukio 14 jumla kwa Unguja na Pemba ni matukio 20 kama nilivyosema. Watu waliokamatwa kwa Mjini Magharibi ni 17, Kusini Unguja ni 5 jumla ni watu 22. Kwa hiyo, Mikoa mingine ya Zanzibar hakuna matukio yaliyotokea ya ujambazi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea lakini nampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwenye swali la nyongeza halafu anakuwa na *data* ambazo zinazohusu suala lenyewe. Hicho ni kitu kinachothihirisha kwamba tunakwenda na Kasi Mpya, Ari Mpya na Nguvu Mpya. *(Makofi)*

Na. 58

**Kutoa Ruzuku Kwa Madawa ya Kuogesha Mifugo**

**MHE. SAID JUMA NKUMBA (K.n.y. MHE. LUCAS L. SELELII)** aliuliza:-

Kwa kuwa, ili kufikia ubora wa mifugo na viwango vya Kimataifa, mifugo yetu hasa ng'ombe hutakiwa kuogeshwa kwa dawa ili kuondoa wadudu wanaosababisha magonjwa; na kwa kuwa, bei ya dawa hizo ni kubwa sana:-

Je, Serikali ipo tayari kutoa ruzuku kwa dawa hizo ili kuwawezesha wafugaji kununua dawa hizo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:_

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii, Mbunge wa Nzega, kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba ili kufikia ubora wa mifugo na hata baadhi ya viwango vya Kimataifa, mifugo hutakiwa kuogeshwa. Serikali imekuwa ikiwahamasisha wafugaji kuzingatia taratibu zinazotakiwa katika kuogesha mifugo ili

kutokomeza wadudu hasa kupe na mbung'o pamoja na kudhibiti magonjwa yaenezwayo na wadudu hao. Katika juhudi za kudhibiti magonjwa hayo ya mifugo, kati ya mwaka 2003/2004 hadi 2005/2006 Serikali kupitia Mipango ya Kuendeleza Kilimo Wilayani *(DADPs)* ilikarabati majosho 420 kwa gharama ya shilingi 1,958,601,540 katika mikoa yote nchini. Aidha, katika kipindi hicho Mashirika yasiyo ya Kiserikali na vikundi vya wafugaji walikarabati majosho 172 na kufanya jumla ya majosho yaliyokarabatiwa kuwa 592.

Pamoja na juhudi zilizopo za kukarabati majosho ili yaweze kutumika kuogesha mifugo, dawa za kuogesha ni ghali ambapo lita moja inauzwa kati ya shilingi 10,000/= na shilingi 70,000/= na kufanya wafugaji wengi wasiweze kuogesha mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua tatizo hilo Serikali kupitia Wizara yangu imetenga jumla ya shilingi bilioni 2 kwa ajili ya kutoa ruzuku ya kununua dawa za kuogesha mifugo katika mwaka wa fedha 2006/2007. Ruzuku hiyo itawawezesha wafugaji kununua dawa hizo kwa bei nafuu. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali itaendelea na juhudi za kutafuta fedha ili ruzuku kubwa zaidi iweze kutolewa kwa lengo la kupata dawa nyingi zaidi za bei nafuu na hivyo kuwawezesha wafugaji wengi zaidi kuogesha mifugo yao.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Kwa kuwa kwa maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri inaonyesha kwamba Serikali haijawa na utaratibu maalum wa utoaji wa ruzuku wa madawa ya mifugo. Na kwa kuwa Serikali inaendelea kuwahamasisha wafugaji wajiunge kwenye Vyama vya Akiba na Mikopo. Je Serikali itakuwa tayari kuziwezesha *SACCOS* ambazo zitaanzishwa na wafugaji kwa kutoa ruzuku maalum ya kusaidia wafugaji kupata elimu bora ya ufugaji, kupata mikopo na kupata madawa kwa bei ya nafuu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa Serikali imepata mafanikio makubwa kupitia Mpango wa MMEM. Je, Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Mifugo ina mkakati gani kuanzisha mpango maalum wa ujenzi wa majosho na mabwawa katika maeneo yote ya wafugaji nchini ili kudhibiti magonjwa ya mifugo na wafugaji waweze kutulia eneo moja bila kuhamahama kwa kutafuta malisho na maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, si kweli kwamba Serikali haina utaratibu mzuri wa kutoa ruzuku hii. Kwa taarifa tu ni kwamba ruzuku zote ambazo Serikali huwa inazitoa huwa inaandaa mkakati na utaratibu maalum ambao ruzuku hiyo inatolewa. Kwa ruzuku hii niliyoisema ambayo kwa mwaka huu wa fedha ni shilingi bilioni 2 mkakati wa utoaji wa ruzuku hii umeshaandaliwa kinachosubiriwa tu ni Hazina kutoa fedha ili kusudi zabuni ziweze kutangazwa kwa wanunuzi wa dawa hizi ili hatimaye ziweze kuuzwa kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Nkumba amesema utaratibu wa MMES na MMEM utumiwe kwenye ujenzi wa majosho. Napenda tu kumhakikishia Mheshimiwa Nkumba na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba ina mpango unaojulikana kama *Agricultural Sector Development,* Mpango ambao unatekelezwa chini

ya *District Agricultural Development Plans (DADP's)* ambapo wananchi vijijini wanatakiwa wao wenyewe kuibua miradi ya kuendeleza sekta ya kilimo ambapo mifugo imo na hivyo wakiamua kulingana na mahitaji yao kujenga majosho basi watajenga majosho kulingana na mahitaji yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zipo na kinachotakiwa ni wananchi wenyewe kuamua mahitaji yao ili kuweza kutumia fursa hii. Hakuna sababu ya kupoteza muda kutengeneza utaratibu mwingine wakati tayari utaratibu upo mzuri kabisa. Namwomba Mheshimiwa Mbunge aweze kuitumia fursa hii kwenye eneo lake na sisi Waheshimiwa Wabunge kwenye maeneo yetu ili kuweza kuwasaidia wananchi wetu.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali ilisamehe ushuru wa kuingiza dawa za mifugo nchini. Lakini msamaha huo waliofaidi ni wafanya biashara wanaonunua hizo dawa. Je, Serikali ina utaratibu gani katika mikakati hiyo Naibu Waziri anayosema ya kufikisha madawa hayo kwa bei rahisi kwa wafugaji nikiwemo mimi?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Mifugo imeandaa utaratibu mzuri kabisa wa namna ya kutoa ruzuku hii ambapo itakuwa nafuu kulingana na fedha zilizopatikana kwa mwaka huu wa fedha. Ni azma ya Serikali kuendelea kuongeza ruzuku hii ili kusudi madawa mengi zaidi na kwa bei nafuu zaidi yaweze kutolewa. Kwa sasa hivi namwomba Mheshimiwa Laizer pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine turidhike kuwa hiki kilichopatikana mwaka huu wa fedha ni azma nzuri ya Serikali na Serikali ina azma ya kuendelea kusaidia wafugaji ili kuendeleza sekta hii ya mifugo.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa ubora wa mifugo unategemea vile vile na uimarishaji wa vituo vya utafiti wa mifugo na vituo vya uchunguzi wa magonjwa ya mifugo. Na kwa kuwa madawa mengi ya akiba ya chanjo za mifugo tunaagiza nje. Je, Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba sasa wakati umefika hayo madawa vituo vyetu vya utafiti na uchunguzi wa mifugo waweze kutengeneza hapa nchini badala ya kuagiza na madawa mengine yamekuwa yame-*expire*?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la vyuo vya utafiti umeainishwa vizuri kwenye sheria inayoanzisha *Institution* hizo. Suala la uzalishaji mara kwa mara linafanywa kwa uzuri zaidi na sekta binafsi. Sekta ambayo ina watengenezaji ambao watakuwa wamebobea kwenye utengenezaji. Sasa kurundika shughuli zote kwamba utafiti pamoja na utengenezaji pamoja na uuzaji

ambazo ndiyo *stage* ambazo zinafuatwa *commercialization* ya *product* yote inayofanyiwa utafiti na kugundulika itakuwa haina tija sana kwa upande wa vituo vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba kupitia Bunge lako Tukufu na Waheshimiwa Wabunge kuhamasisha sekta binafsi na tayari wameshaanza hasa hivi viwanda vinavyotengeneza madawa ya binadamu na mifugo tayari wengine wameshaanza. Kwa hiyo, ni vyema shughuli hii ikafanywa na sekta binafsi.

Na. 59

**Kiwanda cha Nyama**

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ya Awamu ya Nne ina mipango mizuri ya kuendeleza kilimo na ufugaji hapa nchini; na kwa kuwa, lipo tatizo kubwa hapa nchini la ukosefu wa masoko ya uhakika kwa mazao ya matunda na mifugo; na kwa kuwa Serikali ina mpango wa kujenga machinjio ya kisasa Dar es Salaam hivi karibuni:-

(a) Pamoja na nia hiyo nzuri. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Kiwanda cha Kusindika nyama Dar es Salaam ili kusaidia kuleta tija kwa wafugaji;

(b) Kwa kuwa, mbali na *Tanganyika Packers* vipo viwanda vingine Mikoani ambavyo vilikuwa vinasaidia sana *processing* ya matunda na nyama. Je, Serikali itavifufua lini viwanda hivyo ambavyo kwa sasa vimekufa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupitia Bunge lako Tukufu na Waheshimiwa Wabunge kuhamasisha sekta binafsi na tayari wameshaanza hasa hivi viwanda vinavyotengeneza madawa ya binadamu na mifugo tayari wengine wameshaanza. Kwa hiyo, ni vyema shughuli hii ikafanywa na sekta binafsi.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum naomba nitoe maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi za kuendeleza sekta ndogo ya nyama zimeanza muda mrefu ambapo Serikali imekuwa ikiwekeza na kuhamasisha sekta binafsi hapa nchini pamoja na wawekezaji kutoka nje kwa kuwekeza katika kuanzisha ranchi za ng'ombe wa nyama na kujenga machinjio za kisasa. Machinjio ya kisasa ya Dodoma na Chuo cha Ukataji Nyama ni ushahidi tosha wa nia nzuri ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa zipo machinjio nne hapa nchini. Machinjio ya Dodoma na Arusha zinafanya kazi na zile za Morogoro na Sumbwanga zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Aidha, kuna kiwanda kidogo cha kusindika nyama Dar es Salaam kinachoitwa *TANMEAT* ambacho kinasindika aina mbalimbali za nyama. Baada ya maelezo haya naomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia mabadiliko ya kiuchumi na kisera yanayoendelea hapa nchini, shughuli za kibiashara zikiwemo uzalilshaji na usindikaji wa nyama na biashara ya mifugo zinafanywa na sekta binafsi.

Serikali imebakia na majukumu ya kuhamasisha na kuwezesha sekta binafsi kuwekeza katika mifugo ikiwa ni pamaoja na kujenga viwanda vya kusindika nyama. Serikali itaendelea kusaidia kuleta ushawishi na kuweka vivutio ili sekta binafsi ili iwekeza katika viwanda vya kusindika nyama kwa ajili ya soko la ndani na la nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, machinjio ya kisasa ambayo yanatarajiwa kujengwa na sekta binafsi pamoja na Jiji la Dar es Salaam na Manispaa za Temeke, Ilala na Kinondoni huko eneo la *Kiltex* Ilala, Dar es Salaam kitakuwa pia na sehemu ya kusindika nyama.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vilivyokusudiwa kusindika nyama vya Mbeya na Shinyanga hadi sasa vipo chini ya Kamati Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma *(PSRC)* na tayari zabuni za kuvibinafsisha zilikwisha tangazwa ili kuwapata wawekezaji makini ambao wataviendeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali itafanya kila linalowezekana kuhakikisha kuwa viwanda hivi na vingine vitakavyojengwa vinafanya kazi iliyokusudiwa.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa Serikali inasema kwamba inategemea sana sekta binafsi kwa ajili ya kuwekeza kwenye sekta hii ya mifugo na kilimo. Na kwa kuwa kuendelea kusubiri wawekezaji kuwekeza katika sekta hii na hatujui kwamba tutawekeza leo ama kesho.

Wakati huo huo asilimia kubwa ya Watanzania ni wafugaji na wakulima. Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kuwa na mpango kamili na wa dhati Serikali yenyewe angalau kusaidia wananchi kulikoni kuendelea kusubiri sekta binafsi ambazo ni za kubahatisha hazina uhakika?

Pili, kwa kuwa Serikali ya awamu hii ina mpango wa kumpatia kila mwananchi maisha bora. Na kwa kuwa wananchi wengi wanategemea kilimo na ufugaji haioni kwamba kusema kwamba wananchi wanapata maisha bora wakati huo huo hakuna mpango wa dhati wa kucheleweshа maendeleo ya wananchi hawa ambao ni wengi kwa Taifa la Tanzania?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba juhudi za Serikali za kubinafsisha au kuviuza hivi viwanda ambavyo vinalenga kutengeneza mazao ya mifugo zimekuwa na kasi ambayo sio nzuri sana.

Kwa hiyo, kuanzia mwaka kesho kupitia Bunge lako Tukufu tutaomba fedha ili kuweza kuanzisha viwanda hivi ambavyo vitakuwa mpaka wakati huo havijapata wawekezaji kuviweka katika hali ya umakini wa kutengeneza bidhaa hizo za mifugo na baada ya hapo tunaweza sasa kuvikabidhi vikiwa kwenye hali ya kufanya kazi kama tunavyofanya kwa Dodoma na tutakavyofanya kwa Shinyanga na sehemu nyingine.

Suala la pili, ni kweli kwamba jitihada zetu za kupunguza umaskini ni vyema zikaenda sambamba na juhudi za kuwaleta katika misingi bora wafugaji ambao ni watu muhimu sana katika Taifa hili.

Kwa hiyo, mipango tayari iko mbioni ili kuwezesha mifugo kwanza kuipatia mahali ambapo tunaweza kuipa ugani. Kuipatia huduma za kutosha na pili kupitia Bunge lako Tukufu ni kuwaomba wafanyakazi wakiwemo Waheshimiwa Wabunge kuanzisha miradi ya kunenepesha mifugo ambao watakuwa tayari kwa ajili ya kwenda kwenye viwanda hivi ambavyo tutakuwa tumevifufua hivi karibuni, jinsi mipango yetu ya kufufua ilivyo.

Ni shughuli njema na nina matumaini kwamba sekta hii ya mifugo itakuwa haraka sana kwa ushirikiano wa Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa ujumla, ambao wana uwezo wa kufanya hizo shughuli za kuendeleza mifugo yetu hapa nchini.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Naibu Waziri alipokuwa anajibu swali la msingi alisema kwamba Jiji na Manispaa zake na mwekezaji wako tayari kuanzisha Kiwanda cha Nyama pale palipokuwa na Kiwanda cha *KILTEX.* Na kwa kuwa Jiji na Manispaa ya Ilala na Kinondoni zimeshachangia na Temeke tunategemea watachangia wiki hii.

Kwa kuwa tatizo ni Wizara ya Ardhi inakwamisha kuhamisha milki ya eneo hilo kwenda Jiji. Je, Waziri ya Mifugo au Waziri Mkuu atasaidia kuhimiza hii ili mwekezaji asikate tamaa kwa sababu amekuja na mapesa mengi hapa nchini?

**WAZIRI WA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Manispaa pamoja na Jiji walikuwa na mpango kuingia kwenye ubia na mwekezaji ili kujenga kiwanda cha nyama sehemu kilichokuwa kiwanda cha Kiltex. Lakini katika kufanya hivyo ni vyema masharti yanayohitajika hiki ni kiwanda cha chakula ni kiwanda cha nyama, masharti yanayohitajika yakafuatwa na si kweli kwamba Wizara ya Ardihi walichokuwa wanakifanya kiko katika urasimu wowote ambao umekwamisha mradi huu. Kilichokuwepo ni kwamba mradi wenyewe pia umechukua muda mrefu sana kwa wawekezaji kukubaliana masharti ya kukianzisha na baada ya hapo mambo yalipokamilika ilibidi taratibu nyingine zifuatwe ambazo ni muhimu sana sisi kama Taifa kwa wananchi wetu na pia kwenye soko la nyama nchini na nchi za nje. Ni lazima kiwanda kiwe kwenye sehemu inayokubalika na kiwe na *facilities* zinazokubalika kuwa kiwanda cha kutengeneza nyama.

Na. 60

**Kupanua Wigo wa Mtandao wa Utalii Nchini**

**MHE. JAMES D. LEMBELI** Aliuliza:-

Kwa kuwa sekta ya utalii ina fursa nyingi kwa mtalii kuona kuwa mfano, uwindaji, kupiga picha, fukwe za bahari na maziwa, maeneo ya utamaduni na mambo ya kale; na kwa kuwa sera ya utafiti nchini inasisitiza kupanua wigo wa mtandao wa utalii nchini kwenda katika maeneo mengine yenye vivutio ya Mikoa ya Kusini, Magharibi na Kanda ya Ziwa:-

(a) Je, Serikali ina mipango gani ya dhati ya kutekeleza azma hiyo kwa kuzingatia bajeti ya Wizara ya 2006/2007?

(b) Je, Serikali ina utaratibu gani wa kufanya Pori la Akiba la Moyowosi kuwa la kuvutia sio tu kwa watalii wa uwindaji ila pia kwa kipiga picha. Hivyo kuongeza pato la Taifa na kuongeza ajira na nafasi ya biashara ndogo ndogo kwa wanachi wa Kahama?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa James Lembeli, Mbunge wa Jimbo la Kahama lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Katika Bajeti ya Mwaka 2006/2007, Wizara yangu itabainisha vivutio vya utalii na maeneo ya uwekezaji katika Ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi ili kuhimizia uwekezaji katika maeneo hayo na kukuza utalii wa ufukwe. Hatua hii pamoja na mambo mengine inalenga kutatua wigo wa mazao ya utalii kwa kuendeleza utalii wa fukwe.

Aidha katika Bajeti ya mwaka 2006/2007 Shirika la Hifadhi ya Taifa litanunua ndege tatu kwa ajili ya kurahisisha shughuli za usafiri na usafirishaji katika kutekeleza kazi mbalimbali za uhifadhi. Kati ya hizo ndege tatu zitakazonunuliwa ndege moja yenye uwezo wa kuchukua abiria 14, itafanya safari zake ikiwa ni pamoja na kutoa huduma ya

usafiri kwa watalii watakao hitajika kwenda kutembelea Hifadha za Mahale ilipo Mkoani Kigoma, Katavi Wilayani Mpanda na Ruaha Mkoani Iringa. Hii itasaidia kurahisisha usafiri katika shughuli za utalii nchini.

Vilevile ili kuhimizi juhudi za kuendeleza utalii katika Mkoa ya Kanda ya Ziwa Mkoa wa Kagera uliadhimisha siku ya utalii duniani kitaifa tangu tarehe 26 hadi tarehe 29 Oktoba, 2006 ili kutangaza fursa za utalii zilizopo katika Mkoa huo na Kanda ya Ziwa kwa ujumla.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ipo katika hatua za mwisho za maandalizi ya mpango wa usimamizi za pori la Moyowosi, mpango huo unaainisha mpango wa matumizi mbalimbali ya rasilimali zinazopatikana katika pori hilo kulingana na Sheria ya wanyamapori ya mwaka 1974.

Aidha wamiliki wa vitalu vya uwindaji wa kitalii wameruhusiwa kuendesha biashara ya utalii wa picha kwa miezi ambayo uwindaji wa kitalii haufanyiki. Juhudi hizi zinalenga kutanua wigo wa utalii hasa kwa kutoa fursa za kuendeleza utalii wa picha kwa maeneo yale yasiyokuwa ya Hifadhi ya Taifa ambako utalii wa picha unaruhusiwa kwa sasa. Pori la Akiba la Moyowosi ni miongoni mwa mapori yaliyoko katika mpango huu. Kwa kufanya hivyo tuna imani kuwa pato la Serikali litaboreka na pia pato la wananchi wakiwemo wananchi wa Kahama.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza. Kwa vile sekta ya utalii wa uwindaji imedhihirisha kutolipatia Taifa pesa zinazostahili ukizingatia mwaka jana liliingizia Taifa shilingi bilioni 12 tu. Ukilinganisha na Hifadhi za Taifa na Ngorongoro ambayo wanaendesha biashara ya utalii wa kupiga picha na kuliingizia Taifa karibu shilingi bilioni 50 kwa mwaka uliopita. Je, Serikali haioni sasa ni wakati mwafaka wa kufuta baadhi ya vitalu vya uwindaji ili kutoa fursa ya utalii wa kupiga picha ambao unatija kubwa kwa Taifa lakini pia unatoa fursa nyingi kwa wananchi kupata kipato na pia hauui wanyama?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi kwamba, utalii wa picha ni moja tu ya aina ya utalii ambayo inaongeza wigo wa utalii hapa nchini. Tumezoea kuwa na huu utalii wa kwenda kuangalia wanyama lakini ili kuongeza wigo tumeona tuongeze aina nyingine za utalii.

Hata hivyo kutokana na ombi la Mheshimiwa Lembeli tutaangalia na pengine ingekuwa vema atufahamishe ni vitalu gani vya uwindaji ambavyo anaona havileti tija kwa Taifa na kwa wananchi. Atueleze ni vitalu gani hivyo ili tuweze kuangalia kwa pamoja. Lakini hata hivyo naendelea kusisitiza kwamba utalii wa upigaji picha ni moja tu ya aina nyingi za utalii ambazo zinaongeza wigo wa mapato ya kiutalii.

Na. 61

**Kulinda mazalio ya Samaki Mto Ruhuhu**

**MHE. CAPT. JOHN KOMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa mto Ruhuhu unaomwaga maji ndani ya Ziwa Nyasa na una mazalio mazuri sana ya samaki kama vile mbelele, mbasa, ngumbu, mbufu na kadhalika, ambao hutoa ajira kwa wananchi waishio kando mwa Ziwa Nyasa.

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kulinda mazao hayo na kuweka *cage culture* ili kuongeza wingi wa samaki wanaovuliwa?

(b) Je, Serikali inalinda vipi mazingira ya mazalio hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Kapteni John Komba, Mbunge wa Mbinga Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) ninapenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Ninakubaliana na maelezo ya Mheshimiwa Mbunge kuwa Mto Ruhuhu ni eneo zuri la mazalio ya aina mbalimbali za samaki zikiwemo mbasa, ngumbu, mbufu na mbelele. Aidha Wizara inahimizi kuwa jukumu la kulinda rasilimali za uvuvi lisiachiwe Serikali peke yake bali liwe jukumu la jamii ya wavuvi na wadau wote wa sekta ya uvuvi ili kuhakikisha kuwa rasilimali inalindwa inatunzwa na kudumisha usimamizi na uvunaji endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti baada ya kutoa maelezo hayo sasa ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Kapteni John Komba, Mbunge wa Mbinga Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Wizara ya Maliasili na Utalii inayo Sheria Na. 22 ya mwaka 2003 na Kanuni za Uvuvi za mwaka 2005. Sheria hii inampa uwezo Waziri wa Maliasili na Utalii kutenga maeneo ya mazalio ya samaki baada ya kupata taarifa za kuridhisha kutoka kwa wataalam wa mazingira na sekta ya uvuvi pamoja na wadau. Baada ya eneo kukubalika kuwa ni mazalio ya samaki, dhamana ya kusimamia utekelezaji huo iko chini ya Halmashauri za Wilaya pamoja na jamii ya wavuvi. Aidha Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003 inaruhusu wadau wa sekta ya uvuvi kuanzisha vikundi vya usimamizi wa mialo/forodha ili kusimamia maeneo ya mazalio pamoja na kudhibiti uvuvi harama kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kufuga samaki kwenye uzio (*cage culture)*, ninapenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa ufugaji wa njia hii inabidi

ufanyike baada ya kufanya utafiti kuhusu ubora wa maji na teknolojia inafanya pamoja na tathimini ya athari za mazingira *(Environment Impact Assessment)* ili kazi hiyo iwe endelevu. Kwa kuwa Mto Ruvuma unamwaga maji kwenye Ziwa Nyasa ambalo linamilikiwa kwa pamoja na nchi za Malawi, Msumbiji na Tanzania, ufugaji wa samaki wa aina hii ni lazima ukubaliwe na nchi zote tatu baada ya kufanya utafiti na kukubaliana na aina ya *Cage Culture* inayofaa na samaki watakaofungwa kwenye mito inayomwaga maji ziwani ukiwemo Mto Ruhuhu. Wizara ya Maliasili na utalii haina mpango wa kuanzisha ufugaji huo kwenye Mto Ruhuhu badala yake inawahimiza wananchi wachimbe mabwawa ya samaki. Wizara yangu iko tayari kushirikiana na wadau kwenye kuendeleza ufugaji wa samaki kwenye mabwawa.

**MHE. CAPT. JOHN KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri na sauti nzuri ya kupendeza ya Naibu Waziri, (*Kicheko*)

Nina maswali mawili ya nyongeza; kwa kuwa kaskazini mwa mto huo ambako unanzia kuna machimbo ya vito vya thamani na kwa kuwa wachimbaji hawa wanachekecha vito hivyo na udongo wake kuingia kwenye maji ya Ziwa Nyasa kupitia mto huo na kwa kuwa kemikali zinazotumika katika kuchekecha madini yale mengine yanamadhara kwa binadamu, kwa samaki na kwa wanyama wanaokunywa maji hayo. Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti hali hiyo.

La pili kwa kuwa Serikali kupitia Bajeti ya mwaka huu 2006 imeahidi kutoa fedha kwa ajili ya mafunzo ya uvuvi bora katika mto huo. Je, fedha hizo zitatolewa lini?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu udhibiti wa uchafuzi wa mazingira unaotokana na wachimbaji wadogo wadogo wa vito ambao Mheshimiwa Mbunge anaona unaleta uchafuzi. Taarifa tuliyonayo ni kwamba uchimbaji unaofanyika kando kando ya mto huo zaidi ni uchimbaji wa rubi na katika kuchimba vito hivyo mara nyingi wachimbaji hawa huwa wanatumia baruti kupasua miamba ili kupata hivyo vito. Kwa maana hiyo basi uchafuzi ni kweli kwamba unatokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa Wizara yangu na Wizara zinazohusika tutafanya utafiti kuhusu hali ya uchafuzi na kuangalia hatua ambazo zitaweza kuchukuliwa ili kuweza kunusuru hali hiyo; na kuhusu mafunzo kwa wavuvi naomba nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba azma hiyo bado ipo na mafunzo yatafanywa kwa wavuvi kama ambavyo Wizara ilivyoahidi. Vile vile naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi anavyofutilia kwa makini kabisa kuhusu maslahi ya wananchi wa Jimbo lake hususan masuala ya wavuvi. *(Makofi)*

Na. 62

**Kampuni ya *Placer Dome*-Kununua Mafuta kwa Fedha zetu za Kigeni**

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA (K.n.y. MHE. CHACHA Z. WANGWE)** aliuliza:-

Kwa kuwa, fedha za kigeni ni muhimu kwa uchumi wa Taifa hivyo inatakiwa zitumike kwa uangalifu na kwa mahitaji muhimu; kwa kuwa Kampuni ya *Placer Dome* inayochimba dhahabu huko Nyamongo – Tarime, hununua mafuta yote yanayohitajika kuendesha migodi toka nje kwa fedha yetu ya kigeni; na kwa kuwa mafuta hayo hutumika kuzalisha umeme ambao ni magewatt nyingi sana;-

(a) Je, Serikali haioni kwamba inapoteza fedha za kigeni kuiagizia kampuni hiyo mafuta ambayo hayatozwi kodi wala ushuru?

(b) Je, Serikali haioni kwamba ingeweza kuokoa fedha hizo za kigeni kwa kupeleka umeme wa *TANESCO* ambao tayari uko Tarime Mjini km 32 tu kutoka mgodini ili kampuni hiyo ilipie gharama zake lakini pia vijiji vya Magobiri, Nyamwigora, Rosana, Kemakorere, Nyarero, Nyamwaga, Kewanja na Matongo vinunue umeme huo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe, Mbunge wa Tarime, lenye sehemu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, migodi mikubwa ya madini hutumia umeme mwingi katika kuendesha shughuli zake. Hapa nchini Migodi ya Bulyanhuku Wilayani Kahama, Mwadui katika Wilaya ya Kishapu na Lusu Wilaya ya Nzega pekee ndiyo inayotumia umeme wa gridi ya Taifa kati ya migodi minane mikubwa iliyoko nchini. Migodi iliyobaki, ukiwemo wa Nyamongo hutumia mafuta mengi katika kuzalisha umeme kwa kuwa haijaunganishwa kwenye gridi ya Taifa.

Aidha, kwa mujibu wa *Notice* ya Serikali Na.480 ya tarehe 25/10/2002, mafuta hayo hayatozwi kodi wala ushuru kwani hivyo ni vivutio kwa makampuni yanayowekeza kwenye madini.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa kama mgodi wa *North* Mara ungekuwa unatumia umeme wa *TANESCO*, baadhi ya vijiji vilivyotajwa katika swali la msingi vingeweza kutumia umeme huo na hivyo kuharakisha maendeleo katika maeneo hayo. Hata hivyo, baadhi ya vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge vya Nyamwaga na Kewanja ni kati ya vijiji vitakavyopatiwa umeme chini ya Mpango wa Usambazaji Umeme Vijijini (*Energizing Rural Transformation – ERT*), wa mwaka 2006/2007.

Na. 63

**Kampuni inayofanya Ukaguzi wa Gharama za Uwekezaji na Uendeshaji Migodi**

**MHE. AZIZA SLEYUM ALLY** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna kampuni ambayo inafanya ukaguzi wa gharama za uwekezaji na uendeshaji migodi inayoitwa *Alex Stewart (Assayers) Government Business Corporation – ASAGBC.*

(a) Je, kampuni hiyo imeanza lini kazi hiyo na itakamilisha lini ili tenda hiyo itangazwe upya?

(b) Je, kama imemaliza muda wake wa tenda ikatangazwa upya ni kampuni gani imepata tenda hiyo?

(c) Kama ni kampuni hiyo hiyo, ndiyo imepata tenda. Je, tenda hiyo imetangazwa lini na ilipitishwa na nani?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mbunge Viti Maalum, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyingi duniani zenye biashara ya madini kama Tanzania zimejiwekea utaratibu wa kuwa na kampuni za ukaguzi *(audit firms)* ili kuhakiki gharama za kweli za uzalishaji wa madini, usafirishaji wake, uwekezaji na uendeshaji wa madini, usafirishaji wake, uwekezaji na uendeshaji wa midogo mikubwa, lengo ni kuzishauri Serikali husika juu ya kiasi cha kodi halali ambazo zinatakiwa kulipwa na makampuni ya madini katiak nchi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya makampuni yenye jina kubwa duniani inayoheshimika kwa utaalamu wake, uzoefu wake na uhakiki mzuri ni kampuni ya Alex *Stewart* (*Assayers*) G*overnment Business Corporation*.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu a, b na c kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Juni mwaka 2003, Benki Kuu kwa niaba ya Serikali yetu, iliingia mkataba wa miaka miwili na kampuni ya *Alex Stewart* (*Assayers*) *Government Business Corporation* kwa lengo la kuhakiki uzalishaji na gharama za uzalishaji na usafirishaji wa dhahabu pamoja na uwezekaji na uendeshaji wa migodi mikubwa nchini. Mkataba huo ulimalizika mwezi Juni, 2005.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mkataba huo wa miaka miwili kumalizika, Benki Kuu, kwa niaba ya Serikali na kwa kutumia kifungu Namba 2.4 cha mkataba huo, iliamua kuipa kampuni ya *Alex Stewart* Mkataba wa miaka miwili zaidi utakaomalizika mwezi Mei, 2007.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki Kuu, kwa niaba ya Serikali haikulazimika kuitisha tenda tena kama ilivyofanya mwaka 2003. Kama nilivyosema, Benki Kuu iliipatia Kampuni ya *Alex Stewart* Mkataba wa pili kwa kutumia kifungu namba 2.4 cha Mkataba kinachoruhusu Benki Kuu kuongeza muda wa Mkataba iwapo inaridhika na utendaji kazi wa kampuni hio ya ukaguzi.

**MHE. AZIZA SLEYUM ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza; kwa kuwa Naibu Waziri ameeleza kuwa kampuni hii inafanya kazi vizuri sana na ni kampuni ambayo ina jina kubwa. Je, anaweza kutueleza katika Tanzania kampuni hii imeleta mafanikio ya aina gani ambayo yamewezesha kuleta kipato cha kuongeza kipato katika nchi yetu na wanalipwa na nchi yetu kiasi gani cha mapato ambayo walilipwa kutokana na kodi ya wananchi mpaka *BOT* imeona ni vizuri zaidi kuwaongezea mkataba wao waweze kuendelea?

La pili naomba Mheshimiwa Naibu Waziri aweze kutueleza kuwa baadhi ya vyombo vya habari viliripoti kampuni hii kuwa inalipwa pesa nyingi na *BOT* ambazo pesa hizo nilivyozisoma kwenye gazeti ukizilinganisha na gharama za ujenzi wa jengo hili la Bunge ni sawa na Jengo la Bunge hili jipya. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kutueleza kwamba ni akina nani Wakurugenzi wa Kampuni hiyo wasiokuwa na uchungu wa pesa za wananchi wa Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kazi nzuri iliyofanywa na *Alex Stewart,* ningependa kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwanza kazi tatu ambazo zimafanywa na kampuni ya *Alex Stewart* ni kama ifuatavyo:-

Kwanza imekamilisha utaratibu wa kuratibu na kufanya *Auditing* yaani ukaguzi wa uwezeshaji, uwekezaji wa miradi na hali ya fedha katika migodi mikubwa sita. Mgodi wa Geita, Bulyanhulu, *North Mara,* Lusu pamoja na mgodi wa Buhemba. Hii imekwishafanyiwa kazi ya awali na kampuni ya *Alex Stewart.*

Lakini kwa nyongeza ni kweli kwamba kampuni ya *Alex Stewart* hulipwa kila mwezi ada ambayo inaitwa *Audit fees* kwa kazi hii nzuri iliyofanya ilalipwa kila mwezi na katika kipindi cha mwaka 2003 hadi mwaka 2006 mgodi huu tayari umekwishalipwa na Serikali jumla ya *US Dollars* zisizopungua milioni 31 kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge.

Lakini hizo ni hela za *Audit fees* ambazo ni halali na katika kipindi cha miaka hiyo yote. Serikali inatambua kwamba ingawa kampuni hii iko *credible* na inafaa kufanya kazi nchini, lakini Serikali inatambua pia kwamba ada zake zinazotozwa katika shughuli hii ni kubwa na Serikali inaahidi kwamba mbele ya safari Serikali itafanya tena *review* ya kuangalia mkataba mzima ili kupunguza kiwango cha fedha zinazotozwa kwa kampuni hii ambayo inatusaidia kwa kiasi kikubwa kutathimi ni makapuni gani, yanafanya nini, yanazalisha nini, ili tuweze kuyabana yalipe kodi halali Serikalini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni ya *Alex Stewart* ni kampuni ya Kimarekani, Bodi yake ya Wakurugenzi iko Marekani na kiongozi au *President/CEO* wa Marekani anaitwa Bwana Henrick Segura, *Chief Operation Officer* ambaye yupo Marekani anaitwa Bwana Elvis Florance, lakini hapa nyumbani Tanzania kampuni hii inayo viongozi na ningependa kuwataja wanne kama ifuatavyo:-

Kampuni hii inayo *General Manager* ambaye ni *Representative* wa Tanzania hii anaitwa Bwana George Kaindoa, kampuni hii inayo *Technical Operations Manager* ambaye ni Bruce IBel, *Environment Manager* anaitwa Dancun Stevens na wanaye *Chief Financial Auditor* Bwana Godfrey Urassa. Hiyo ndiyo *composition* ya kamapuni ya *Alex Stewart.*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kulingana na muda na uzito wa hoja iliyopo mbele yetu ninaomba niseme kwamba tunaendelea na shughuli kadri ilivyopangwa. Swali Namba 64 Mheshimiwa Bakar Khamis Faki, ameliondoa swali hilo kwa sababu limeulizwa katika Wizara ambayo si husika. Hivyo naomba nimpe nafasi Mheshimiwa Paul Kimiti tumalizie swali la mwisho kwa leo.

Na. 65

**Kulinda Mazalio ya Samaki Mto Ruhuhu**.

**MHE. PAUL P. KIMITI** aliuliza?

Kwa kuwa Serikali inatambua tatizo la maji mjini Sumbawanga; na kwa kuwa pamoja na jitihada zake za kutoa fedha kidogo kila mwaka kuongeza uwezo wa vyanzo vya maji:-

(a) Je, mpaka hivi leo, mpango wa kudumu wa kuwatumia wafadhili wa *ADB* na *BADEA* umefikia wapi?

(b) Je kwa kuwa Serikali ya Norway inaujua vizuri Mkoa wa Rukwa na hasa Sumbawanga kuhusu hali ya maji, isingekuwa bora kwa Serikali kwamba Serikali ya Norway waje Rukwa kukamilisha mipango waliyokuwa wameianza vizuri sana ya kueneza maji Mkoani Rukwa?

(c) Je, ni nini hatma ya mfuko wa maji kitaifa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paul Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimshukuru Mheshimiwa Paul Kimiti kwa kutambua jitihada za Serikali katika kutatua tatizo la huduma ya maji safi katika mji wa Sumbawanga.

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jibu la swali la Bunge Na. 4479 la mwaka 2005 Mbunge alijibiwa kuwa Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*) ilionyesha nia ya kuikopesha Serikali fedha kwa ajili ya miradi ya kuboresha huduma ya maji katika miji ya Sumbawanga. Shinyanga, Lindi na Mtwara, lakini baadaye ikajiondoa kwa sababu zilizokuwa nje ya uwezo wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Benki ya Nchi za Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (*BADEA*) ilionyesha nia ya kuboresha huduma ya maji mjini Sumbawanga, ila tangu ripoti ya uchunguzi wa awali *(pre-feasibility report)* ilipowasilishwa kwao mwezi Septemba 2004, hatujapata maamuzi yao.

Serikali kwa kuzingatia tatizo kubwa la maji kwa baadhi ya miji nchi, imeamua chini ya mpango wa *National Urban Water Supply and Sewerage Programme (NUWSS)* unaolipiwa kwa mkopo nafuu wa Benki ya Dunia, kuinua kiwango cha huduma ya maji kwa kufanya kazi zenye kipaumbele kwa miji ya Sumbawanga, Mtwara, Lindi na Babati. Usanifu wa miradi hiyo unatekelezwa na Mhandisi Mshauri *(Mott McDonald)* na kazi ipo katika hatua ya mwisho ya maandalizi ya makabrasha ya zabuni. Hatua itakayofuata ni kumpata Mhandisi Mshauri mwingine atakayesimamia mkandarasi wa kuchimba visima na ujenzi.

Sambamba na hatua hizo, mpango wa kutumia mfuko wa *ACP – EU Water Facility* ili kuboresha huduma ya majisafi na majitaka kwa miji ya Sumbawanga, Mtwara, Lindi, Babati, Kigoma, Musoma na Bukoba unaendelea. Mpango huu utagharamiwa na Umoja wa Nchi za Ulaya (*EU*) na Shirika la Kijerumani la *KfW*. Kwa hatua za usanifu *EURO* 2.6 *Million* zimetengwa. Atakayesanifu mradi husika na kuwasimamia wakandarasi watakao utekeleza zitakamilishwa ndani ya mwaka wa fedha 2006/2007.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Serikali ya Norway kupitia shirika la (*NORAD*) ilikuwa ikifadhili miradi mbalimbali nchini ikiwemo miradi ya maji Mkoa Rukwa. Katika kipindi hicho cha ufadhili kipaumbele kilikuwa katika miradi ya maji vijijini.

Katika mji wa Sumbawanga visima 18 vilichimbwa na pampu za mkono zilifungwa. Visima hivyo vinaendelea kuwasaidia wakazi wakati wa uhaba maji. Hata hivyo mwaka 1996 *NORAD* iliamua kuacha kujihusisha na sekta ya maji Mkoani humo.

Mheshimiwa Mwenyekiti katika mwaka 2001 juhudi za Wizara na viongozi wa Mkoa Rukwa kuiomba Serikali ya Norway ikamilishe mpango mzuri ulionzishwa wa kueneza maji mkoani Rukwa ikiwemo mji wa Sumbawanga hazikuzaa matunda.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti kuhusu mfuko wa maji wa Taifa Wizara imeandaa mapandekezo ya kuanzishwa kwa mfuko huo kisheria. Mapendekezo hayo ni sehemu ya mkakati wa uendelezaji wa sekta ya maji *(Water Sector Development Strategy)* ambao upo katika hatua za mwisho za kuwasilishwa Serikalini. Mara baada ya Serikali kuridhika mkakati huo, hatua za kuanzisha mfuko zitachukuliwa.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa jitihada ambazo Serikali inafanya kuhakikisha maji yanapatikana katika Mji wa Sumbawanga. Nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Serikali ina mpango kabambe wa kuhakikisha kwamba kila Wilaya inapewa vijiji angalau kumi vya kuwa na maji katika kipindi cha miaka miwili/mitatu ijayo. Na kwa kuwa tunaelewa kwamba kwa hivi sasa hakuna mashine za kuchimba visima virefu katika nchi hii, yaani zile *rigs*. Je, katika mpango huo ambao Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumzia, isingekuwa vizuri baadhi ya fedha hizo zitumike kwa kuagiza *rigs* nying ili mpango unaoanzishwa na Serikali mwaka kesho uweze kufanikiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili. Kwa kuwa naelewa jitihada ambazo alikuwa akizifanya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward N. Lowassa, wakati akiwa ni Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo katika Mji wa Sumbawanga. Na kwa kuwa yeye mwenyewe anaelewa tatizo la maji katika Mji wetu. Je, kupitia kwako Mwenyekiti, unaweza kuniombea kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ili jitihada hizo hizo alishughulikie suala hili la maji katika Mji wa Sumbawanga ili tuweze kufanikiwa badala ya kungoja hizi au ahadi ambazo zinatolewa kila wakati kupitia Benki ambazo hatuna madaraka nazo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu! Lakini utajibu lile la (a), suala la (b) nadhani kupitia kwangu Mheshimiwa Waziri Mkuu amelisikia na mtawasiliana naye. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bajeti ya mwaka huu Bunge lako Tukufu limetuidhinishia fedha kwa ajili ya shughuli za Kampuni inayochimba visima. Na katika fedha hizo, kimojawapo kinachofanywa ni kuendeleza na kununua vifaa vipya vya kuchimbia visima. Kwa hali hiyo basi, *rig* itakuwa ni mojawapo ya vifaa vitakavyonunuliwa na Kampuni ya *DDCA* ambayo ni *Agency* yetu ya kuchimba visima.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana kwa swali la Mheshimiwa Paul P. Kimiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Paul P. Kimiti, kwa jinsi anavyofuatilia tatizo la maji katika Mji wa Sumbawanga. Tunakiri kwamba liko tatizo kubwa la siku nyingi katika Mji wa

Sumbawanga na tunawashukuru sana wananchi wa Sumbawanga kwa uvumilivu wao. Napenda kuwahakikishia kwa niaba ya Serikali kwamba tutafanya kila liwezekanalo ili wananchi wa Sumbawanga waweze kupata maji safi na maji salama. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakushukuru sana! Waheshimiwa Wabunge, kipindi cha maswali na majibu kimekwisha. Nitatoa matangazo yaliyoko mezani kwangu na baada ya kutoa matangazo, nitamwomba kwa heshima na taadhima, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mbunge wa Kongwa, aje kukalia kiti na kuendelea na shughuli zilizopangwa leo ndani ya Bunge letu. *(Makofi)*

Tangazo la kwanza; nimeombwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, Mheshimiwa William H. Shellukindo, anawatangazia Wajumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara kuwa leo Jumatatu, tarehe 6 Novemba, 2006 saa 7.000 mchana, kutakuwa na Kikao cha Kamati katika Ukumbi Na. 219, ghorofa ya pili, *wing* B.

Tangazo la Pili; Mheshimiwa Paul P. Kimiti kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, anawatangazia wajumbe wa Kamati ya Miundombinu kuwa leo tarehe 6 Novemba, 2006 saa 7.00 mchana, kutakuwa na kikao chao katika ukumbi Na. 227 *wing* C, ghorofa ya pili. Anaomba sana wajumbe wote wahudhurie kikao hicho.

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa na Mwenyekiti wa *TAPAC*, Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o, kwamba anawatangazia Wabunge Wajumbe wa Chama cha Wabunge walio katika mapambano dhidi ya UKIMWI, *TAPAC*, kwamba kutakuwa na kikao leo mchana mara baada ya Kuahirisha Bunge. Kikao hicho kitafanyika katika Ukumbi wa Pius Msekwa au Ukumbi wetu wa zamani. Wajumbe wote wahudhurie kikao hicho.

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo ya wageni. Mheshimiwa Joel N. Bendera, anaomba niwatangaze wageni wake ambao wako nasi hapa leo ambao ni Madiwani 19 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe. Naomba wasimame kama wako hapa ndani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Madiwani, karibuni sana. Vile vile wanafunzi 50 na walimu wawili wa Shule ya Msingi Amani, Mjini Dodoma wamekuja kujifunza shughuli za Bunge. Hao siyo wageni wa Mheshimiwa Bendera lakini ni wageni kutoka Dodoma. Naomba na wao wasimame. *(Makofi)*

Wanafunzi 25 na Walimu na 5 wa Kanisa la Mennonite la Mjini Arusha wamekuja kujifunza nao shughuli za Bunge. Naomba nao wasimame wanafunzi na walimu wao. *(Makofi)*

Viongozi na wanafunzi wa Chuo cha Elimu ya Biashara kutoka Jijini Dar es salaam nao wamekuja kujifunza shughuli za Bunge. Ningeomba na wao wasimame. *(Makofi)*

Mheshimiwa Luhaga J. Mpina, anasema ana mgeni wake ambaye ni Katibu Mwenezi wa Chama kutoka Mwananongu katika Jimbo lake. Naomba na yeye asimame. *(Makofi)*

Tunao pia Waheshimiwa Madiwani kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, ni wageni wa Mheshimiwa Guido G. Sigonga na Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa. Tunaomba wageni hawa Waheshimiwa Madiwani na wao wasimame. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao Madiwani pia kutoka Jimbo la Moshi Vijijini, wako 18. Hao ni Madiwani wa Halmashauri ya Moshi Vijijini, ni wageni wa Mheshimiwa Dr. Cyril A. Chami. Naomba Madiwani hao pia wasimame. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Chrisant M. Mzindakaya, anao wageni wake, kuna Ms. Dinna Talawe anatoka *Kingston University of London, United Kingdom* ameambatana na kijana wake Paul Mzindakaya na yeye anatoka *City of London College, United Kingdom,* na wao naomba wasimame ili waweze kutusalimu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wenyeviti wa Kamati za Bunge kukutana na Katibu wa Bunge kujadili suala muhimu na anaomba kikao hicho kifanyike saa 7.00 mchana Ukumbi wa Spika. Kwa hiyo naomba tafadhali sana Wenyeviti wote wa Kamati wahudhurie kikao hicho.

Waheshimiwa Wabunge, nimeagizwa pia na Mheshimiwa Kidawa H. Salehe, niwatangazie Wabunge wa Chama cha Mapinduzi wayarudishe yale madodoso waliyopewa kwenye ofisi yetu ya Chama cha Mapinduzi (CCM) hapa Bungeni kama tulivyokubaliana siku ya Jumamosi.

Baada ya matangazo hayo, sasa ninaomba nimkabidhi kiti Mheshimiwa Job Y. Ndugai, ili aweze kuendelea na shughuli nyingine za leo.

*(Hapa Mwenyekiti Mhe. Job Y. Ndugai alikalia kiti)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kitakachofuata ni tangazo la Mheshimiwa Spika ambalo limetolewa na Ofisi ya Katibu wa Bunge. Nitalisoma kama lilivyo.

Tangazo hili linahusiana na matamshi ya Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, yaliyotolewa tarehe 3 Novemba, 2006.

Mheshimiwa Spika, amefadhaika sana na maneno aliyonukuliwa kuyasema Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, kama yalivyoripotiwa na magazeti kadhaa tarehe 3 Novemba, 2006.

Kauli hiyo ya Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto pamoja na mambo mengine, imehoji uelewa wa Spika kuhusu Kanuni za Bunge.

Kwenye Bunge lolote, msingi wa uendeshaji wake ni ufahamu wa Kanuni wa Spika na yeyote anaekalia kiti. Uhalali huo ukihojiwa hadharani, unadhalilisha hadhi ya Kiti cha Spika na hatimaye unadhalilisha hadhi ya Bunge zima. Ni kitendo cha utovu wa nidhamu… *(Makofi)*

Naomba kurudia hapo. Ni kitendo cha utovu wa nidhamu kwa Mbunge ambaye hoja yake ikikataliwa Bungeni, akaenda nje ya Bunge na kutamka kama alivyofanya Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto.

Kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Mbunge yeyote ambaye haridhiki na maamuzi ya Spika Bungeni, anatakiwa kupeleka malalamiko au hoja yake mbele ya Kamati husika ili yashughulikiwe kwa utaratibu uliopo. Kutokana na hali hiyo, Mheshimiwa Spika, ameagiza kwamba Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto amwombe radhi kupitia vyombo vya habari kabla ya Jumamosi tarehe 11 Novemba, 2006. *(Makofi)*

Ikiwa Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto atakuwa hajafanya hivyo, hatua za kinidhamu kwa mujibu wa Kanuni hizi za Bunge, zitachukuliwa dhidi yake. Mwisho wa tangazo! *(Makofi)*

Tangazo la mwisho kabisa ni kwamba Kamati ya Maliasili na Mazingira itakutana leo tarehe 6 Novemba, 2006 saa 7.00 kwa ajili ya kupitia hesabu za Kitengo cha Bahari.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Nyama wa Mwaka 2006
### *(The Meat Industry Bill, 2006)*

*(Kusomwa mara ya Pili)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa *The Meat Industry Act 2006*, sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu unaleta mapendekezo ya sheria mpya itakayosimamia shughuli za sekta ndogo ya nyama nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ndogo ya nyama ilikuwa ikisimamiwa na kampuni ya nyama ya *Tanganyika Packers Limited* kuanzania mwaka 1950 hadi mwaka 1974 kupitia viwanda vyake vya Kawe na Arusha.

*TPL*, ilikuwa ikishughulikia usindikaji na bishara ya nyama hapa nchini kabla ya kutaifishwa na kuwa chini ya Mamlaka ya kuendeleza Mifugo *(LIDA)* mwaka 1974.

*LIDA* ilianzishwa kwa sheria Na. 13 ya mwaka 1974 na ilifanya shughuli zake za uzalishaji, usindikaji na biashara ya mifugo kupitia Makampuni Tanzu ya Biashara ya Mifugo kwa kifupi KABIMITA, Chakula Barafu *(NCCO)*, *Ranch* za Taifa *(NARCO)*, Kampuni ya Ng'ombe wa Maziwa – *DAFCO*, Kampuni ya Kusindika Maziwa *(TDL)*, Kampuni ya Kuku *(NAPOCO)*, Kampuni ya Ngozi *(THS)* na Kampuni ya kusindika Nyama *(TPL)* hadi ilipovunjwa mwaka 1984.

Kuvunjwa kwa *LIDA* na kufutwa kwa sheria iliyoanzisha Mamlaka hiyo na kufungwa kwa *TPL* mwaka 1993, kumeacha pengo katika usimamizi wa Sekta Ndogo ya Nyama hapa nchini. Serikali kwa kutambua hilo, katika Sheria Ndogo za Maziwa, ilitunga Sheria Na. 8 ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya sasa ya Sekta Ndogo ya Nyama, Kutokana na kuanza kutekelezwa kwa Sera ya Uchumi wa Soko, Serikali imeiachia Sekta Binafsi kutekeleza shughuli za uzalishaji kama vile kuendesha mashamba ya ng'ombe wa nyama na viwanda vya kusindika nyama na usambazaji wa nyama na mazao yake. Serikali imebakia na jukumu la kuandaa Sera, kusimamia sheria na kuratibu Maendeleo ya Sekta ndogo ya nyama nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokuwepo kwa Sheria ya Nyama na kufungwa kwa *TPL*, kumesababisha shughuli za Sekta Ndogo ya Nyama kutokupanuka kwa kiasi kinachostahili pamoja na kuwepo kwa rasilimali kubwa ya mifugo hapa nchini na mahitaji makubwa ya nyama katika Miji mikubwa, Mahoteli ya Kitalii na Migodi. Hali hii imesababisha uzalishaji na usindikaji na biashara ya nyama kukosa usimamizi madhubuti kisheria na kuathiri vibaya maendeleo ya Sekta Ndogo ya Nyama. Hivyo basi, kuna haja ya kuwa na sheria itakayosimamia Sekta hii Ndogo ya Nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuandaa Muswada huu, wadau mbali mbali walioshirikishwa ni pamoja na:- wafugaji wa asili, wafugaji wa kibiashara, wasindikaji na watoa huduma za mifugo, wasambazaji wa pembejeo za mifugo na Chama cha Wafanyabiashara za Viwanda na Kilimo nchini, *TCCIA*.

Wadau hao wameshirikishwa kuanzia ngazi za vijiji, Tarafa, Wilaya hadi Taifa kwa njia ya mikutano, semina, warsha na makongamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha wadau wengine walioshirikishwa ni Wizara za Afya na Ustawi wa Jamii, Fedha, Biashara, Viwanda na Masoko, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Kilimo, Chakula na Ushirika, Sheria na Katiba na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matarajio baada ya kutungwa kwa sheria; Wizara imejiwekea malengo mbali mbali kupitia dira ya Sekta ya Mifugo ambayo imedhamiria kuwa ifikapo mwaka 2025, Sekta ya Mifugo itakuwa shirikishi na itazingatia ufugaji wa kisasa ulio endelevu na unaoendeshwa kibiashara.

Aidha, dira imezingatia ubora wa tija ya mifugo itakayozalishwa ili kuinua maisha ya Mtanzania na kutoa ajira na kuzalisha malighafi kwa ajili ya usindikaji, kuongeza pato la taifa na kuhifadhi mazingira. Sambamba na dira hii, Wizara yangu inatekeleza Ilani ya Uchanguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini ya Wizara yangu kwamba Sheria hii mpya itarahisisha kufikiwa kwa madhumuni na matarajio ya dira hii na hivyo kufikiwa kwa matarajio ya Watanzania katika kupanua wigo wa ajira na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokwishasema awali, Muswada huu wa Nyama utasaidia kusimamia shughuli zilizokuwa zinafanywa na Mamlaka ya kuendeleza Mifugo yaani *LIDA* katika hali ya mfumo wa sasa wa Uchumi wa Soko na kufanya iwe ni kichocheo halisi cha ukuaji wa Sekta Ndogo ya Nyama na Sekta ya Mifugo kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo muhimu katika Muswada huu. Mambo muhimu yaliyozingatiwa katika Muswada huu ni kama ifuatavyo:

(a) Kuanzishwa kwa Baraza Kuu la Wadau katika Sekta Ndogo ya Nyama;

(b) Kuundwa kwa Bodi ya Nyama;

(c) Usajili wa shughuli mbali mbali za Nyama chini ya Sheria hii;

(d) Kuanzishwa kwa Mfuko chini ya Sheria hii;

(e) Waziri kuweka Kanuni na taratibu mbali mbali za kusimamia Sekta Ndogo ya Nyama; na

(f) Kuainisha makosa na adhabu mbali mbali chini ya Sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kutoa mpangilio na mtiririko wa Muswada huu, naomba nichukue fursa hii kuishukuru Kamati ya Bunge ya Kilimo na Ardhi, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Gideon A. Cheyo, Mbunge wa Ileje, kwa kuchambua Muswada huu na kuukubali kuwa uletwe mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia nashukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali hususan, Idara ya Mwandishi Mkuu wa Sheria kwa mchango wao mkubwa katika kueleza dhana na vipengele mbali mbali kwa wajumbe wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nawashukuru Wataalam na watumishi wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo, kwa maandalizi ya awali ya Muswada huu. Baada ya kutoa shukrani hizi, naomba nitoe kwa muhtasari mpangilio wa maeneo muhimu ya Muswada. Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu saba kama ifuatavyo:-

(i) Sehemu ya kwanza ina utangulizi, inaelezea jina la Muswada, tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria hii na tafsiri ya maneno mbali mbali yalitotumika kwenye Muswada huu.

(ii) Inaelezea kuanzishwa kwa Baraza la Mwaka la Wadau wa Sekta Ndogo ya Nyama, Wajumbe wake na mambo mengine yanayohusu Mkutano Mkuu wa Wadau.

(iii) Inaeleza kuanzishwa kwa Bodi ya Nyama, Wajumbe wa Bodi na Taratibu ya Vikao vya Bodi. Aidha sehemu hii inafafanua mambo ya Utawala wa Bodi ikiwa ni pamoja uteuzi wa Watumishi mbali mbali wa Bodi na kinga kwa Wajumbe na watumishi wa Bodi watakapotekeleza majukumu yao chini ya Sheria hii.

(iv) Sehemu hii inahusu usajili wa wazalishaji, watengenezaji na wauzaji wa nyama na bidhaa za nyama pamoja na wasambazaji wa zana zinazotumika kwenye fani hizo. Sehemu hii pia ina masharti yanayohusu uteuzi wa Msajili na majukumu yake.

(v) Sehemu hii inahusu uanzishwaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Sekta Ndogo ya Nyama. Majukumu ya mfuko huu, Usimamizi wa Mfuko na Ukaguzi wa Mahesabu ya Mfuko na vyanzo vya mapato. Sehemu hii pia inatoa jinsi Mamlaka kwa Bodi ili kuwawezesha kufanya shughuli zao kama ilivyotakiwa na Sheria

(vi) Sehemu hii inaainisha makosa na adhabu mbali mbali chini ya Sheria inayopendekezwa kwenu

(vii) Sehemu hii inatoa Mamlaka kwa Waziri mwenye dhamana ya Sekta ya Mifugo, kutengeneza kanuni na taratibu mbali mbali chini ya Sheria hii.

Mwisho; Muswada huu unapendekeza majedwali kwa ajili ya taratibu za Wajumbe wa Baraza la Mwaka la Wadau na Wajumbe wa Bodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa taarifa hii, sasa naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa namwita Msemaji wa Kamati iliyochambua suala lililo mbele yetu. *(Makofi)*

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH (k.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO NA ARDHI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 70(2) cha Kanuni za Bunge Toleo la 2004. Naomba kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kilimo na Ardhi juu ya Muswada wa Sheria ya Nyama wa 2006 *(The Meat Indusry Bill, 2006).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dr. Shukuru Kawambwa, Mbunge kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Maji. Tunamshukuru sana kwa ushirikiano wake mzuri alipokuwa Waziri wa Maendeleo ya

Mifugo na jinsi alivyotoa maelezo yake fasaha ya awali kuhusu Muswada huu. Aidha, tunapenda kumpongeza Mheshimiwa Anthony M. Diallo, Mbunge, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na tumekwishaanza naye kwa kushirikiana naye. Wote tunawatakia mafanikio mema katika kazi zao walizopangiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu ilipata fursa ya kuujadili Muswada huu katika vikao vitatu. Kikao cha kwanza kilifanyika hapa Dodoma tarehe 4 Aprili, 2006. Katika Kikao hicho Kamati ilipata maelezo ya jumla kuhusu madhumuni ya Muswada huu. Kikao cha pili kilifanyika Mjini Dar es Salaam tarehe 26 Oktoba, 2006, kwa kuwashirikisha Wadau mbalimbali katika Sekta ya Mifugo, kama vile wataalamu wa wizara ya Maendeleo ya Mifugo, Makatibu wakuu wa wizara mbalimbali, Mamlaka ya Dawa na Chakula Tanzania *(TFDA)*, Shirika la Viwango *(TBS)*, Kituo cha wawekezaji Tanzania *(TIC)*, *Tanzania Chamber of Commerce, Industry and Agriculture (TCCIA)*, Chuo Kikuu cha Sokoine *(SUA)*, Ranchi za Taifa *(NARCO)*, Bodi ya Maziwa, Vyama vya wafugaji, Wazalishaji, Wafanyabiashara ya Mifugo na Nyama, Wasindikaji, Vyama vya kijamii, *NGOs* pamoja na Vyombo vya habari kama vile *television, radio* na magazeti. Katika kikao hicho Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Anthony Diallo, Mbunge, alipata fursa ya kuwaeleza Wadau madhumuni na matarajio ya Muswada huu. Aidha, Mheshimiwa Waziri na Wataalamu wa Wizara yake waliweza kujibu na kufafanua hoja zote zilizotolewa na Wadau.

Kikao cha tatu kilifanyika hapa Dodoma tarehe 31 Oktoba, 2006. Katika kikao hicho Kamati ilizingatia michango mbalimbali ya Wadau na maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Wataalamu wake na kuhitimisha mchakato wa kuufikiria Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu imeridhika na madhumuni na matarajio ya Muswada huu ambayo yanalenga kuboresha uzalishaji wa Wanyama kwa ajili ya Nyama kwa matumizi ya binadamu. Aidha Sheria iliyokusudiwa itasaidia katika kuendeleza, kuboresha na kuhamasisha usindikaji, utafutaji wa masoko na matumizi ya nyama na bidhaa zitokanazo na Nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweka tafsiri sahihi ya maneno mbalimbali yaliyotumika ndani ya Muswada huu, na kwa kuzingatia nafasi ya Sekta binafsi katika kumiliki Vyuo Vikuu binafsi, tumeshauriana na Mheshimiwa Waziri kufanya marekebisho machache katika Ibara za 3, 5, 9 na 33 za Muswada. Marekebisho hayo yamekwishatolewa na Mheshimiwa Waziri na kusambazwa kwa Waheshimiwa Wabunge pamoja na Orodha ya Shughuli za Bunge kwa kikao cha leo. Kamati yangu inaunga mkono marekebisho hayo na inamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuyaweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili sheria inayokusudiwa iweze kutekelezwa kwa ufanisi, Kamati yangu inatoa ushauri ufuatao:

(i) Ili Baraza la Mwaka la Wadau wa Sekta Ndogo ya Nyama na Bodi ya Nyama ya Tanzania viweze kufanya kazi zilizoainishwa katika Muswada huu, Serikali na Wadau wachukue hatua za makusudi kuhakikisha kuwepo kwa Vyama na Makundi yanayotajwa

kuwa Wajumbe wa Baraza la Mwaka na Bodi ya Nyama kama ilivyo katika Ibara za 5 na 9 za Muswada.

(ii) Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ziwe na Mipango endelevu ya huduma za Ugani katika Sekta ya Mifugo ili Wafugaji waweze kufuga mifugo bora itakayotoa Nyama Bora.

(iii) Serikali kwa jumla itambue umuhimu wa Sekta ya Mifugo na Wafugaji, na itekeleze kwa Vitendo Sheria za Ardhi Na. 4 na Na.5 za 1999 zinazoelekeza kutenga na kuwamilikisha Wafugaji maeneo ya Ufugaji. Aidha, Serikali itenge Bajeti ya kutosha kufanikisha kazi hii.

(iv) Wafugaji wenye mifugo mingi wahamasishwe kuivuna ili kuboresha hali yao ya kiuchumi

(v) Serikali ifufue viwanda vya kusindika nyama katika Mikoa ya Shinyanga na Mbeya na maeneo mengine yenye Wafugaji, kwa kuwavutia Wawekezaji kwenye sekta hii ya nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu inamshukuru sana Mheshimiwa Anthony Diallo, Mbunge, Waziri wa Maendeleo ya Mifugo,kwa mashirikiano na kuendeleza majadiliano ya Miswada pale alipoacha mwenzake. Pia Kamati inamshukuru Mheshimiwa Dr. Mlingwa Mbunge, Naibu Waziri na Wataalamu wao kwa ushirikiano wao mzuri na kuiwezesha Kamati hii kukamilisha kazi yake vizuri. Vile vile, Kamati inawashukuru Wadau wote walioshiriki katika kikao cha tarehe 26 Oktoba, 2006 kwa michango yao mizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kilimo na Ardhi kwa Uchambuzi na michango yao ya kina wakati wa majadiliano ya Muswada huu. Napenda niwatambue Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mwenyekiti, Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Kheri Ameir Mjumbe, Mheshimiwa Idd Azzan Mjumbe, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Joyce Machimu, Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, Mheshimiwa Fredrick Mpendazoe, Mheshimiwa Manju Msambya, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Martha Umbulla na Mheshimiwa Chacha Wangwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho napenda kuishukuru ofisi yako kwa ushirikiano na uwezeshaji katika kushughulikia Muswada huu. Mwisho kabisa nisingependa kumsahau Katibu wa Kamati hii ndugu Frank Mbuni kwa kufanya kila jitihada ili kuhakikisha maoni ya Kamati hii yanakamilika kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Bunge lako Tukufu lifikirie na kupitisha Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Muswada huu na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nichukuwe nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii kutoa maoni kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kuhusu Muswada wa Sheria wa *Meat Industry Bill, 2006* kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu 43 (5)(c) na kifungu 70 (2) Toleo la 2004.

Kadhalika, napenda kutumia fursa hii kumpongeza Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa Anthony Diallo, Mbunge wa Ilemela kwa kuwasilisha vyema Muswada huu.

Sambamba na hilo napenda kuipongeza Kamati ya Kilimo na Ardhi, kwa namna ambavyo imeujadili kwa kina Muswada huu na kuweza kuwasilisha maoni yake mbele ya Bunge lako Tukufu. Sina shaka mapendekezo ya Kamati hii yanalenga katika kuuboresha Muswada huu kwa nia ya kukuza ufanisi katika utekelezaji wa sheria yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani, umeutafakari vyema Muswada huu na hasa kwa kutilia maanani sababu na madhumuni ya kuwasilishwa kwake pamoja na athari zake kwa wadau. Aidha, tumezingatia mabadiliko ya Sera ya Kilimo na Mifugo ya mwaka 1997 inayoelekeza kuimarishwa sekta binafsi katika uzalishaji pamoja na biashara ya mifugo na mazao yake. Kwa muda mrefu sasa wafugaji na wafanyabiashara mbalimbali wamekuwa wakijishughulisha na biashara ya mifugo kwa ajili ya kuwapatia wananchi nyama na mazao yake. Kwa bahati mbaya katika kipindi chote hicho hapakuwepo na udhibiti wa kutosha wa biashara hii. Ni dhahiri basi kupitishwa kwa Muswada huu na kuwa sheria kamili kutasaidia kusimamia na kudhibiti ipasavyo uzalishaji wa wanyama na kwa ajili ya nyama na mazao yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, sheria hii itasaidia kuendeleza, kuboresha na kuhamasisha matumizi ya nyama na bidhaa zitokanazo na nyama, usindikaji na utafutaji wa masoko ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia niliyoyataja hapo juu, Kambi ya Upinzani haina pingamizi kupitishwa Muswada huu kwani hatimaye sheria itakayokuwepo itatuwezesha kuwa na mipango iliyo madhubuti ya kukuza na kuendeleza biashara ya nyama hapa nchini.

Aidha, Muswada huu unatoa fursa ya kuwashirikisha wadau katika kuleta maendeleo kwenye sekta hii ndogo ya nyama pamoja na kutatua matatizo yanayojitokeza. *(Makofi)*

Kambi ya Upinzani, inaona kupitishwa kwa Muswada huu na kuwa sheria kamili kutatoa uhalali na kuupa nguvu mfumo wa uchumi wa soko ambapo sekta binafsi inashughulikia uzalishaji na biashara ya mifugo, uagizaji na usambazaji wa pembejeo za mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Kambi ya Upinzani inaridhia kupitishwa kwa Muswada huu, hata hivyo tunapenda kushauri mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno yaliyoandikwa katika sura ya II, aya ya 5 kifungu cha tatu yamaeonekana kujirudia katika sura ya III aya 10 kifungu cha (v) tunadhani moja katika maandishi haya yangefutwa.

Aidha, sura ya IV aya ya 23(2) inayosema, nami nanukuu: *"Any appeal may be lodged to the Minister in respect to any refusal of the Board to issue or renew registration provided under this Act or against the revocation or suspension of persons subject to this Act and the Minister's decisions shall be final."* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika dunia ya leo inayozingatia dhana ya utawala bora, sheria inampa kila mtu fursa kutumia nafasi aliyonayo kutafuta haki yake. Kadhalika maendeleo ya kisheria siku hizi hayaruhusu utaratibu wa kuweka *finality clause* kama ilivyowekwa katika aya hii. Tunaona haingekuwa haki kumpa nguvu kubwa ya kisheria Waziri, kazi ambayo inatakiwa kufanywa na mahakama. Kambi ya Upinzani inashauri kwamba Waziri, asiwe na kauli ya mwisho katika masuala haya isipokuwa Mahakama ichukuwe nafasi yake. *(Makofi)*

Kadhalika sura ya 6 aya ya 35 imempa Waziri uwezo wa kubadilisha chochote kilichomo katika sheria iliyotungwa. Kwa sababu sheria hii inatungwa na Bunge ni vyema basi ikaelezwa wazi kwamba marekebisho yoyote yanayokusudiwa kufanywa katika sheria hii basi ni lazima yapitishwe na Bunge lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo na kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kuwasilisha. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ningependa kuwaarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba ninao wachangiaji watatu tu. Kwa hiyo, nafasi bado ipo kwa Mheshimiwa yeyote atakayependa kuchangia katika suala lililopo mbele yetu.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, ili na mimi nitoe mchango wangu kuhusu Muswada wa Sheria ya Nyama.

Kwanza, napenda kuishukuru sana Serikali kwamba imefikia wakati kuiangalia sekta ya nyama. Tuna mifugo mingi sana lakini kulikuwa hakuna sheria ya kusaidia kufanya biashara ya mifugo iweze kuchangia katika pato la taifa. Kwa hiyo, napenda kuipongeza sana Serikali.

Vile vile napenda kumpongeza sana Waziri wa Maendeleo ya Mifugo kwa kutuletea Muswada huu ambao ni mpya kabisa na kuleta vile vile mambo mengine ambayo ni mapya anazidi kuimarisha namna ya kuongoza shughuli za Mifugo. *(Makofi)*

Mimi nitakwenda kwenye Muswada wenyewe. Maana sisi Wabunge tutumie muda mwingi kutazama hizi sheria, vinginevyo kama hatuko makini kuzitazama zitatoka halafu baadaye tunaweza kuulizana ilimekuwa kuwaje. *(Makofi)*

Mimi nina moja ambalo nitaomba nipate maelezo. Inahusu sehemu ya pili ya Muswada Ibara ya 4 inayosema *Establishment of the Annual Council.* Nilikuwa nadhani kunaweza kuwa na *Annual Councils* nyingi sasa ni vizuri hii ingechukua *Annual Council* ya kitu gani ili hata katika mawasiliano iwe rahisi. Nimeona kwenye *interpretation* imetumiwa *Annual Council* sawa inaanzishwa na kifungu cha 4. Lakini ukija kwenye madhumuni kama tungechukua ilivyoeleza kwenye madhumuni basi huku ndani ndiko ingeeleza vizuri zaidi kwa sababu kwenye sehemu ya pili, katika madhumuni imesema hivi hivi, inapendekeza masharti yanayohusu kuanzishwa kwa Baraza la mwaka la Wadau wa Sekta Ndogo ya Nyama. Sasa ukiingia kwenye Muswada kwenye kifungu cha 4 sehemu ya pili kinasema tu *Annual Council*. Mimi nadhani tungetumia hii iwe kamilifu kwa sababu kuna uwezekano kuwa na *Annual Council* ya watu wa korosho au *Annual Council* ya watu wa chai. Kwa hiyo, haya ni maoni yangu kuhusu hii. Hii inasaidia kutochanganya.

Eneo la pili, nilitaka kuzungumzia ni kuhusu kazi za *Annual Council*. Kwa sababu ukishaitamka kwamba ni *Annual Council of Meat Stakeholders* sasa unaweza kutumia *Council* kwa sheria hii inaeleweka kwamba ni *Annual Council of Meat Stakeholders* kuliko kuiacha tu yenyewe tuna-*hang as Annual Council* kwamba ukiandika tu *Annual Council* kila mmoja anajua ni ile ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ibara ya saba ya sehemu hiyo, pale kwenye kazi za *Council* ile sehemu (a), (b), (c), (d), (e) ya ibara ya 7 kimesema: *"To carry out any other function as may be necessary for effective implementation of this Act."* Mimi nadhani ukiangalia katika sheria nyingine zilizotungwa, hapa *specifically* ni Waziri ndiyo ana- *assign* hiyo. Kwa hiyo, ningependa hicho kifungu kitazamwe sehemu (e) kiwe ni *to carry out any other function as may be assigned by the Minister for effective implementation of this Act.* Ukiachia tu kwamba wazungumze lolote nadhani si sawa, lazima ipewe *direction* hiyo.

Nikienda katika ibara ya 9 kwenye Bodi, amezingatia vile vile marekebisho yaliyofanywa na Mheshimiwa Waziri, naunga mkono kabisa pale kuondoa *Public University* kuacha tu *University of Agriculture*. Lakini nilikuwa nadhani katika eneo hili tuna *Vertinary Professionals* katika kifungu hiki. Sasa nilikuwa nashauri kwamba angekuwepo mwakilishi wa *Vertinary Professional Association* hapo ndio ambapo kwa kweli wangeweza kutoa mchango wao mzuri sana kwenye Bodi hii. Naamini ipo, *Medical Doctors* wanayo, *Engineers* wanayo, kwa hiyo, kama hawana kwa kweli itakuwa ni chagizo kwamba sasa waanzishe hiyo.

Katika sehemu ya tatu ule ukurasa wa 9 kifungu cha 13 hapa nilikuwa na wasiwasi kidogo. Mimi nadhani ile *Council* kwa kweli zaidi ni ya mashauriano na ushauri, haina *Executive Function*. Lakini ukiangalia kwenye kifungu cha 13 inapewa kazi ambayo inaingiliana na kazi za Bodi. Kwa mfano ukisoma kifungu hicho kinasema: "*The Board may on such terms and conditions after approval of the Annual Council employs such number of staff to hold appropriate offices under the supervision of the Registrar."* Sasa Bodi kwa kawaida ndiyo yenye kazi hizo. Sasa kama unataka wapate *approval* kwenye *Council* lazima ile *Council* iwe *accountable* kwa baadhi ya vitu vya hiyo *Board*. Kwa sababu hao ndiyo wanaofanya *approval*. Mimi nadhani ile *Council* ingekuwa ni ya ni ushauri kuliko kuipa madaraka ya yale ya *executive* katika bodi. Ingawaliwe isije ikaleta mgongano katika utekelezaji wa shughuli hizi nzuri sana ambazo tunazihitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nilisisitiza ile ibara ya 18 pale anaposema: *"The Board may refuse to register an applicant under section 17 if the applicant does not meet the prescribed condition."* Mimi nadhani hapa kwenye kanuni Mheshimiwa Waziri, ahakikishe kwamba tunaweka muda wa kumjibu mtu huyo. Kwa sababu mara nyingi mtu kitu hakubaliwi, hajibiwi. Kama anakubaliwa ndiyo anajibiwa. Sasa na wale ibadilike kama anakubaliwa ajibiwe kama anakataliwa ajibiwe vile vile. Kuna malalamiko mengi sana ambayo yanatujia Waheshimiwa Wabunge, mengi ni ya kutotekeleza tu, mtu hastahili kitu lakini hajibiwi anapigwa dana dana mpaka mwisho unakuta pengine anapeleka hoja hizi kwa Waziri, hapa nadhani kuna vitu vinatakiwa hapa na kadhalika.

Halafu nilikuwa naangalia kifungu hicho cha 20 ambacho kinahusu *registration* ya vyombo au watu ambao watashughulika na biashara ya nyama kwamba itakuwa kila mwaka. Mimi nadhani tutazame kama ni *registration* ya kumtambua mtu kwamba huyu ni *dealer* wa nyama sasa kwa nini tuiweke *standard* kila mwaka afanye hiyo *registration*, nadhani kazi ya Bodi itakuwa ni ku-*monitor* kama hafanyi kazi hizo basi anamuondoa katika *register*. Lakini isiwe ni kila mwaka mtu wa *registration* ni tofauti na *license* ya kufanyia shughuli lakini ile ya kuji-*register* kwamba *I recognize the meat dealer* kitu kama hicho, mimi nadhani ingefikiriwa hii iwe *once and for all* kuwe na kazi ya kuji-*register* kwa mtu kwamba amekosa sifa za kuwa katika *register* hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo moja ambalo nilitaka kulichangia ni sehemu ya 5 kuhusu *functions of the fund.* Kuna eneo pale wametaja suala la *extension services*. Mimi nadhani hapa kwa kweli Wizara ingejitahidi sana tufufue *extension service* ya mifugo kwa kweli haipo. Kwa hiyo, wakulima, wafugaji wanahangaika. Ingekuwa ni kazi kubwa sana kufufua *extension* ya mifugo. Vile vile hapa tuna suala la *development*. Nakumbuka siku zilizopita nilipokuwa Arusha, Mkurugenzi wa Mkoa mwaka 1975 na kuendelea kulikuwa na mradi maalum wa *Range Development*. Ulikuwa unaitwa *Masai Range Development Project* ambao ulikuwa *financed* na *USAID.* Nakumbuka tulikwenda *Texas* - Marekani kuangalia jinsi wafugaji wa kule wanavyotumia ardhi zao.

Sasa ili kusaidia wafugaji hawa wachukue ufugaji kama ni kazi ya kuondoa umaskini kwa kweli lazima tuwe na mpango maalum wa *Range Development* ambao utaingiza mambo mengi sana. Ujenzi wa mabwawa, ujenzi wa shule za watoto ambao hawawezi kwenda kwenye malisho halafu huku aende na vitabu. Mimi nadhani mpango huu ungetazamwa hapa maadam sasa tunaunda bodi hiyo ambayo itakuwa na suala la *development* na mambo mengine ya *research* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo moja ambalo nimeliona hapa kwenye kifungu 30 ambapo *Controller and Auditor General* ana-*approval appointment* ya *Auditor*. Halafu katika kifungu cha 30 (3) hapa kuna sentensi inayosema hivi, *"The Chairman of the board shall cause copies of each Annual Report together with a copy of opinion of the Auditors or firm of Auditor to be laid before the Annual Council within 3 months after receipts."* Mimi nadhani tunakwenda nje. *Auditor* akiandika, wanaandikiana na Mwenyekiti wa *Board*. Sasa kwenda ku-*table* tena mambo hayo kwenye *Council* kwa kweli ni kuingilia madaraka humu ndani. Kwa sababu *opinion* itakayotolewa hapa ni *opinion* ya bodi kwa mujibu wa sheria. Kwa sababu Mwenyekiti na *register* ndiyo ambao wana-*handle* hizi *day to day operations* za fedha na vitu kama hivyo. Sasa kutoa madaraka kwenye chombo kingine kunaweza kuleta matatizo nadhani ingeangaliwa hiyo. Tubaki kwenye msingi huu *Council* iwe ni ya mashauriano *advisory capacity role* yake hiyo, juu ya sekta hii ambavyo itaweza kwenda.

Eneo lingine katika hicho hicho kifungu cha 30 (5) pale inapohusu mambo ya *accounts* kwamba *as soon the accounts of the Board have been audited* na kuendelea. Kuna eneo pale la *Minister* ku-*table accounts* hizi kwenye Bunge, katika sheria nyingi ukizitazama ipo lakini kwenye hii haipo. Lakini ni vizuri iwepo kwa sababu kuna *population* ya fedha kutoka kwenye Bunge hapa katika kifungu kinachohusiana na utekelezaji wa shughuli za bodi wanapata fedha kutoka kwenye Bunge. Kwa hiyo, *tabling the accounts* ni kitu cha lazima. *(Makofi)*

Sehemu ya saba kuna *mention* ya masuala ya *regulations* ambazo zitaongoza mambo ya *ranches, livestock markets and butcheries*. Mimi nadhani hapa sehemu ya Serikali za Mitaa ijitokeza mahali kwamba ifanyike hii *concentration with local councils or local government* kwa sababu kuna masoko kule ya nyama na mabucha ya nyama sasa isije yakaleta mchanganyiko ijulikane na nani nini sasa isije yakaleta mchanganyiko ijulikane ni nani anasimamia nini. Hivyo vingine vya *inspectors, graders* hivyo vinaweza kuwekewa utaratibu wake kwa sababu kwa vyovyote vile watakuwa kwa wananchi kule. Lakini masoko haya pamoja na masoko ya kuuzia nyama yatazamwe vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika zile *schedule* nilikuwa nasisitiza kwamba hebu itazamwe badala ya kuandika *tenure of office meetings and proceeding of the Annual Council* ingekuwa kamili kabisa *Meet Stakeholder Annual Council* itaweza kukaa vizuri zaidi. Hii ni katika ile *schedule* ya kwanza sasa hapa katika *schedule* ya kwanza ni *council, schedule* ya pili, ni Bodi ya Nyama. Tofauti zionekane kabisa kwamba *Council* iwe kazi yake ni ya ushauri ku-*review policies* na kutoa ushauri kwenye Wizara na Bodi. Lakini Bodi ni *executive* kwa hiyo, ndiyo ipewe zile kazi za kusimamia siku hadi siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu katika kifungu cha 5 cha hiyo *schedule* kunazungumziwa mikutano ya bodi. Pale tungeweka kisehemu kinachosema *The Board may hold extra ordinarily meetings as when circumstances demand* kuliko kuacha tu ukaweka ile mikato na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba niishie hapo, naunga mkono hoja hii na hayo niliyotoa mengine yazingatiwe ili tuweze kuboresha Muswada huu. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia kwa ufupi sana katika Muswada huu. Zaidi kwangu mimi utakuwa ni ushauri na kutaka maelekezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri ambaye ndiye anasimamia shughuli hizi ambazo zimewasilishwa hapa kwetu. *(Makofi)*

Nianzie na pale Mheshimiwa William Shellukindo amemalizia kuhusu bodi kuangalia utaratibu na kusimamia shughuli za siku hadi kutokana na shughuli hizi za nyama. Mimi nimejaribu kuangalia sana katika Muswada huu na katika vipengele mbalimbali. Lakini katika marekebisho yamefanywa huku zaidi ndiko nilikojikita mimi na hasa nikiangalia hali ya kibiashara ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hali kadhalika nikiangalia na Watanzania wenyewe na mbele tunakokwenda.

Kifungu cha 3(e)(4) kinazungumzia pamoja na mambo mengi ni suala la uchinjaji. Nimejaribu kuangalia Muswada huu sikuona mahali ambapo pana sheria, pana taratibu, pana Kanuni. Inazungumza hawa watu binafsi au watu tunaotaka kuwapa kazi ya kushughulika na mambo haya ya nyama wawe wasindika wawe wanafanya vingine vyote wawe wanapeleka kwenye mabucha. Nazungumza suala hili kwa sababu nilikuwa nataka nijitosheleze kwamba Serikali basi iangalie na hali halisi ya Watanzania walivyo katika suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaambiwa kwamba Tanzania haina dini lakini Watanzania wana dini. Sasa katika hili kila nikiangalia naona wenzetu hawakwenda kidogo huku. Lakini pia nikiangalia suala la biashara, biashara hatutaki kufanya Tanzania peke yetu, tunataka kwenda nje tufanye kazi hii ya nyama. Lakini na huko nje tunakokwenda nako tuna marafiki, tuna wenzetu.

Sasa kama tunataka kufanya biashara isiwe na dosari na tusiwape watu wengine wabaya maneno ya kuja kusema baadaye au ya kuja kutafuta *loophole* ya kusema kwamba Tanzania ina kadha na kadha katika suala la nyama. Ningemwomba sana Mheshimiwa Waziri akaliangalia hili. Lakini pia akatoa mwelekezo kwa viwanda vinavyohusika katika uchinjaji wa nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana nina wasiwasi tusije tukachukua ule msemo aangukavyo ndivyo achinjwavyo tutafika mahali wengine watakuwa hawanunui nyama hii kwa sababu ya taratibu zao. Kwa sababu wengine anavyoanguka ndivyo alivyochinjwa hatukubali. Lakini aanguke vizuri achinjwe vizuri ndivyo atakavyoliwa.

Sifikirii hata mwingine yeyote hata wewe Mwenyekiti, kwamba akianguka vyovyote tu akichinjwa siku nyingine utanunua tu lakini huridhiki na uchinjwaji huo.

Sasa Mheshimiwa Waziri, ningemwomba basi akaangalia na sehemu zote hizi mbili. Sitaki aende ndani sana lakini ninachosema ni kwamba bodi ifike mahali iweke sheria, kuwe na kanuni za uchinjaji wa nyama ambao tunataka tuwatumie. Tusichinje tu. Ndiyo nikasema kwamba Tanzania haina dini lakini Watanzania wana dini, tunakula kula nyama hii. Sasa kuwe na utaratibu maalum. Sasa Mheshimiwa Waziri, hili atakuja kutuambia vipi angalau basi tuweke utaratibu unaofahamika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakupa mfano ukienda nchi za wenzetu hasa nchi za Kiarabu, si kwamba wote watakuwa Waislam kwa sababu ni nchi za Kiarabu hapana. Ndani ya nchi za Kiarabu kuna watu wana dini nyingine na wala usije ukasikia mtu anaitwa *Hafidh Al- Saad* kwa mfano, ukafikiria ni Muislam, hapana ni jina tu hilo. Lakini dini yake ikawa nyingine. Abdulaziz utasema kwa jina hili huyu Muislam hapana si Muislam jina kitu kingine dini kitu kingine. Sasa wenzetu kwa sababu ya kuweka tofauti pale ambapo kunachinjwa nyama halali basi unapokwenda katika *ranch* yao ya kuchinjia kile kisu kimeandikwa *Bismillah* na kule alikoelekea yule ng'ombe ndiko kunakubalika.

Kwa hiyo, akipata kasimama akachinjwa, inakuwa kachinjwa katika sehemu ambayo inakubalika. Kwa hiyo, ikiandika nyama halali maana watu wanakubaliana nayo. Lakini nilivyosema nyama halali maana yake si kwamba mwingine hakubali atakubali. Lakini nilichotaka kusema ni kwamba tujiridhishe kwamba basi Watanzania wote au tunapotaka kwenda nchi za nje, tunapouza nyama yetu, iwe haina dosari. Hakuna mtu ambaye anaweza akatutolea jambo likatuharibia kwenye biashara zetu katika hawa watu ambao wawekezaji wanaokuja hapa *point* yangu kubwa iko huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapotaka kupitisha Muswada huu sasa tusiangalie hapa tulipo, tuangalie mbele. Maadui wa nchi wanaweza wakatumia kitu chochote ambacho wanasema sasa hivi tuiumize Tanzania katika biashara kwa hili na akalitumia. Lakini tukianza kujikinga sasa hivi kuona tunatumia taratibu gani ili sote basi tujiridhishe kwamba tumefanya jambo lenye msingi lililokuwa halituletei tofauti kwa pande zote mbili. Kwa sababu nimemwomba Mheshimiwa Waziri, akakaa akalifikiria hili ili tusije tukatoa nafasi kwa watu wabaya kwa nchi yetu wakaja wakatutafsiri vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyama zinauzwa Dar es Salaam, Dodoma na mahali pengine, *wallah* hawaulizwi kwenye bucha wamechinja wapi nyama hiyo, hawaulizi wala hawaulizwi kwamba n'gombe huyo alivyochinjwa kaelekea *Kibla,* sote tunakwenda kununua nyama, tunaondoka. Lakini nasema lazima kama ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tunataka kupitisha jambo hili lazima tuwe na tahadhari. Sasa namwomba sana Mheshimiwa Waziri awe na tahadhari na hili mbaya hajitokezi sasa anajitokeza baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja kwa sababu ya ufanisi na biashara katika Tanzania. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:**Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na mimi kwa kunipa nafasi ili nichangie Muswada huu. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa mikakati aliyoanza kujaribu kufufua zao la mifugo, sasa alipoitisha mkutano ule alioitisha hapa Dodoma na mkutano wake aliyeitisha Mara. Mheshimiwa Rais katika mkutano wake huo wa Mara alizungumzia sana suala la ufugaji. Aliagiza kwamba viwanda vijengwe maeneo ya mikoa ya wafugaji. Kwa kweli nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nategemea tukiwa na viwanda vya mifugo, uchumi wa wananchi wengi utaimarika. Tukipata masoko ya mifugo uchumi wa wafugaji utaimarika zaidi. Ni muda mrefu sana Tanzania ina mifugo na Tanzania ni namba ya tatu Barani Afrika kuwa na mifugo mingi. Lakini ukiangalia wanaofaidi mifugo ya Watanzania ni majirani, kwenye masoko ya Kenya asilimia 60 za mifugo wanaouzwa Kenya ni ng'ombe kutoka Tanzania.

Kwa hiyo, nyama zinazokwenda nje kama Kenya, inaonekana kwamba Kenya ndiyo wana mifugo kuliko Tanzania. Ngozi zinazouzwa nje, Kenya inaonekana kwamba Kenya ndiyo wana mifugo mingi. Kwa hiyo, unaona kuwa hatufaidiki na mifugo iliyoko Tanzania, Kenya ndio inafaidika. Kenya wana kiwanda kikubwa cha *Kenya Meat Commission* na kwa siku wanachinja zaidi ya ng'ombe 300, lakini asilimia 60 ya ng'ombe wanaochinjwa humo ni wa Tanzania. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Serikali Awamu ya Kwanza, Awamu ya Pili, Awamu ya Tatu hawakufikiria kabisa suala la kuimarisha masoko ya mifugo. Kwa hiyo, ndiyo maana namshukuru sana Mheshimiwa Rais. Nawapongeza Mawaziri wa Mifugo, kwanza wote wawili ni wafugaji, kwa hiyo Rais hakukosea kuwaweka wafugaji wawili, kwenye Wizara hii. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ningependa kusema kwamba mnategemewa sana na wafugaji na tumeanza vizuri kwa sababu hata Waziri Mkuu ameanza kunenepesha mifugo. Kwa hiyo, wafugaji wote tunafuata nyayo sasa za Waziri Mkuu kunenepesha mifugo na kuuza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie Bodi. Nadhani mnanisikia kila siku nikidai kwa nini hakuna Bodi ya Mifugo. Hii Bodi ndiyo inatatua matatizo ya mifugo, ndiyo inatatua matatizo ya masoko tuliyokosa. Tanzania kila siku mimi nilipoingia Bungeni hapa nilikuta suala la minofu, minofu ya samaki. Sasa hii minofu ya samaki nasema hivi, samaki tu ana minofu, ng'ombe hawana minofu? Hakuna anayefikiria masuala ya mifugo. Sasa minofu ya samaki ina masoko nje, lakini sisi Tanzania hatuna masoko nje ya kuuzia mifugo, ni Kenya tu ndiyo wanayo.

Kwa hiyo, naomba Wizara hii ijaribu kabisa kuimarisha masoko, kutafuta masoko nje ya nchi na kutafuta masoko ya kuuza nyama, kutafuta masoko ya kuuza ngozi, hapo ndiyo mfugaji atafaidika na atokane na ile hali Mheshimiwa Rais aliyosema kwamba mfugaji anazunguka Tanzania nzima huku amekonda na ng'ombe wamekonda. Hilo

tunakubali lakini muwawezeshe basi hawa Watanzania wa-*settle* na wawe na mifugo bora na wawe na masoko.

Jambo lingine ambalo ningependa kuongezea ombi langu kuna mashamba yaliyokuwa ya mifugo zamani, hayatumiki kwa sasa. Kuna mashamba ya *NARCO* na yako kule *West Kilimanjaro* na maeneo mengine ya Tanzania. Tunaomba mashamba hayo yasibinafsishwe wapewe hao hao wafugaji yawe maeneo mashamba ya kunenepesha mifugo na kuuza. Tunakubali kabisa kuingia biashara ya kuuza mifugo, tunakubali kabisa kuwa na biashara ya kuuza, kuwa na viwanda vya nyama, lakini tupate maeneo ya kufugia hao ng'ombe wa biashara.

Kwa hiyo, haya mashamba ambayo bado wanatafutiwa wawekezaji, wawekezaji wawe wafugaji Watanzania walioko katika maeneo wanaozunguka katika maeneo hayo. Nadhani Mbunge wa Arumeru Mashariki yuko karibu na hayo mashamba. Hivi akitaka kunenepesha mifugo aombe eneo pale si anaweza akafanya biashara pamoja na wafugaji walioko katika maeneo ya Ngarenanyuki, Ngerejani Longido. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ningeomba sana hayo maeneo tupewe, tufanyie biashara ya kuuza mifugo. Jambo lingine ni Halmshauri zetu wafugaji. Tunaomba Wizara itoe elimu kwa Halmashauri hizo za maeneo ya wafugaji ili waanze kutoa elimu kwa wafugaji. Ili waanze kutenga maeneo ya kunenepesha mifugo, maeneo ya biashara. Siyo mifugo tu, bali ni maeneo ya kunenepesha mifugo na kuuza. Ndiyo viwanda vyetu vinavyojengwa vitapata *market*. Isijengwe viwanda baadaye ikakosekana mifugo wenye *quality* nzuri, siyo mifugo tu, mifugo yenye *quality* nzuri.

Mimi katika Wilaya yangu ya Longido tumekwishaimarisha mifugo, wana *quality* nzuri na tumeimarisha kwa sababu masoko tuliyokuwa tukiuzia ng'ombe ni masoko ya Kenya. Sasa ikawa tofauti kwa sababu Kenya wamekwishaboresha mifugo. Sasa tukipeleka hawa wa kwetu inaonekana kwamba hawana *quality*. Ndiyo na sisi tukaanza sasa kuboresha, sasa mifugo Wilaya Kaijado na Wilaya ya Longido hazina tofauti kabisa. Kwa hiyo, ng'ombe za Wilaya yangu zinaweza zikaingia kwenye *market*. *(Makofi)*

Sasa tatizo ni kwamba masoko yako Kenya na wafanyabiashara ni Watanzania wananyanyasika kweli. Kwanza kiwanda cha *Kenya Meat Commission* Mtanzania hawezi kwenda kupeleka ng'ombe pale kuchinja kwenye hicho kiwanda kwa sababu wewe ni Mtanzania mpaka uwe na *identity card* ya Kenya. Kwa hiyo, unakwenda kumpa mtu wa Kenya hao ng'ombe, kama ni ng'ombe 50 unampa iwe ya kwake akauze kwa jina lake, fedha ziingie kwenye *account* yake ndiyo umfuate fuate aende kukutolea hizo fedha. Baadaye fedha za ngozi kwa kila mwaka, Desemba unaitiwa fedha za ngozi za ng'ombe uliouza mwaka nzima. Sasa anayeitwa ni yule Mkenya ambaye unamkabidhi ng'ombe kila siku kwa sababu yeye ndiyo mwenye ng'ombe, siyo wewe Mtanzania. Kwa hiyo, tunanyanyasika sana. Hivi kwa nini tunanyanyasika na sisi tuna Serikali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wafugaji na wewe umetokana na wafugaji. Nasema kwamba wakati mmoja nilisema kwamba bado hajazaliwa kabisa mtu ambaye

anaweza kuwatetea. Atawatetea wafugaji na bado nasema kwamba labda Serikali hii ndiyo sasa ije kutujali wafugaji na kujali kwamba ina mifugo. Kwa hiyo, naomba Serikali hii ijali kabisa mifugo, ianze kuimarisha masoko ya nje na ya ndani. Tusinyanyaswe tena na Wakenya huku tuna ardhi kuliko Kenya huku tuna mifugo wengi kuliko Kenya. Lakini tunanyanyasika.

Naomba Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, elimu hii uifikishe kabisa vijijini. Kitu kingine ambacho ningeomba ni wataalam wa mifugo. Wataalam wa mifugo kule vijijini hakuna wataalam wa mifugo. Utaratibu uliokuwepo ulikuwa ni vurugu, imewekwa Kilimo na Mifugo, wataalam walioko vijijini kule wanaotoa elimu, ni wa kilimo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, huu utaratibu wa Wizara mbili bado kule Kjijini mpaka kwenye Kata, Tarafa, bado ni vurugu tu. Unamkuta mtaalam wa kilimo ndiyo unamtegemea. Kwanza hawapo na ukienda Tarafani ni Mtaalam unamkuta akilima, anajua mambo ya kilimo, hajui mambo ya mifugo.

Kwa hiyo, tunaomba basi tupate wataalam ambao wanajua suala la mifugo, watakaotoa ushauri kwa wafugaji ili wafugaji waweze wakaingia sasa kwenye biashara ya mifugo vizuri na waweze kuboresha mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana nategemea wale watu wawili wataimarisha Wizara hii. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Awali ya yote nataka kumpongeza Mheshimiwa Anthony Diallo kwa kuchaguliwa kuja kwenye ng'ombe na kwa kuwa yeye bila ng'ombe labda asingezaliwa, atajua umuhimu wa kuwatetea wakulima au wafugaji wa ng'ombe. *(Makofi)*

Pia nampongeza Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, kwa kuendelea na kazi yake kwenye Wizara hiyo.

Baada ya kusema hayo, nataka kutoa ushauri kwa mambo yafuatayo:-

Kwanza kabisa natumia nafasi hii kuwatetea wafugaji. Nawatetea wafugaji kwa sababu tangu awamu hii zaidi ya nne imeingia pameonekana kama vile kuna vita kati ya Serikali na wafugaji ambacho ni kitu cha ajabu sana. Matamshi kama chungia kwenye shamba lako wewe mwenyewe, ambapo unajua umegawiwa eka mbili, utachungia wapi, kama una ng'ombe 30. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matamshi kwamba hatutaki ng'ombe wetu wapite katika Wilaya hii kwenda Wilaya nyingine. Sasa ng'ombe wataruka juu kama vile ni *aeroplane* na ni ng'ombe wanaotoka wapi? Matamshi kwamba hatuwezi kugeuza nchi nzima iwe mahali pa kuchungia. Yote haya hayaonyeshi mapenzi kwa ng'ombe hata kidogo. *(Makofi)*

Kwa hiyo wito wangu wa kwanza naomba mapenzi ya ng'ombe kutoka Serikali ya Awamu ya Nne. Muwapende wafugaji, kama mnawapenda wafugaji basi mambo mengine yatafuata. Lakini kama kuna vita na huku mnataka kujenga viwanda vya nyama mnataka kuboresha biashara ya nyama mtapata wapi, kama wafugaji wote wakiamua kwamba hawatauza ng'ombe wao hata mmoja.

Kwa hiyo, kwa matamshi haya ya watu mbalimbali kusema kweli wanawakatisha tamaa wafugaji, na mimi nataka kusema wafugaji ni watu ambao kusema kweli ndiyo wanaoshikilia uchumi wa nchi hii. Tumekuwa na janga kubwa la njaa juzi, mtu aliye na ng'ombe ni sawasawa na aliye na *bank account* ambayo haifilisiki. *Bank Account* yenyewe ambayo inazaa mara dufu ya zile hela kama ungeziweka ndani ya benki. Watu hawa wametuondosha katika janga la njaa.

Kwa kuwa tuna mifugo ndiyo maana wanaweza hata wakatusaidia kujenga shule. Kwa sababu watu wana mifugo ndiyo maana wanaweza hata wakapata fedha ya kuweza kulipa kodi. Kwa hiyo, mfugaji angependa aonwe na Serikali katika umuhimu unaostahili. Hilo la kwanza.

La pili, Wizara hii ya Mifugo ningependa itengeneze mazingira mazuri ya wafugaji. Kujenga malambo, tumeambiwa hapa kuna mikakati. Hatujaelezwa mikakati hiyo itaanza lini. Lakini mikakati hiyo basi ifanye kazi haraka. Bila kuwa na mazingira mazuri ya wafugaji hatutaweza kupata ng'ombe bora watakaoingia katika masoko ambayo tunahitaji au ambao wataweza kupata nyama ambayo tunaweza tukala ndani ya nchi na pia kuweza kupeleka nje.

Kuna wafugaji wengi ambao wamejitahidi wao wenyewe, kujaribu kuboresha mifugo yao. Lakini sidhani kwamba Serikali inawaangalia hawa watu hata kidogo. Mimi ningependa kuona kama vile tunavyozungumza kwenye kilimo kuna shamba darasa? Pia tungependa kuona ng'ombe darasa yuko wapi? Ili watu waone kweli mfano mzuri wa kuweza kufuga ng'ombe anayeuzika. Kufuga ng'ombe ambaye anaweza akapata nyama ambayo iko laini na inaweza kuliwa na watu ambao kidogo meno yao kuna wasiwasi. *(Makofi)*

Kuna wafugaji ambao sasa wameanza kutoa mfano, kwa mfano wafugaji ambao sasa hivi wanawanenepesha ng'ombe wao katika barabara ya Kahama, hawa wanafanya kazi nzuri sana na wanauza mifugo mpaka wakati mwingine inakwenda mpaka laki sita, laki saba ng'ombe mmoja anaweza akanunuliwa.

Mimi naona vitu kama hivyo ambavyo vimeanzishwa na wafugaji wao kwa wao basi Serikali ingewapa mkono ili waweze kweli wakaona kwamba hii ni kazi nzuri, watu wakiweza kunenepesha mahali padogo basi hata ile sababu ya mifugo kuhama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine itapungua.

Lakini nina mashaka kama kuna jambo lolote ambalo linafanyika, wafugaji kwa mfano sasa hivi wananenepesha kwenye barabara ya pale Mwanza, inayotoka Mwanza kwenda Musoma pale Igoma. Huu ni mfano mwingine nzuri ambao unaweza kuona watu

wanaweka ng'ombe wao pale, wanawanenepesha na kweli unaweza kuona matunda yanaonekana. Lakini Serikali inawapa mkono gani? Sasa kama tukiweza kuboresha mazingira mazuri basi tutakuwa tunatengeneza kweli mazingira mazuri ya viwanda vya nyama.

Nikimaliza ya utangulizi, nataka kujikita kwenye Muswada wenyewe na zaidi nataka kuzungumzia ibara ya 17. Hapa mimi wasi wasi wangu ni utekelezaji wa ibara hii ambapo wanasema kwamba itaundwa Bodi ambayo itaandikisha wafanya biashara wa mifugo, *actualy* wanasema *livestock producers.* Sasa kitu cha kwanza ambacho nataka kujiuliza ni wakati gani ufugaji unakuwa biashara. Hili jambo lazima lielezwe bayana, la sivyo watu wengi watakamatwa kwa sababu wana ng'ombe 30, wana ng'ombe 80, wanaulizwa wewe leseni yako ya kupata mifugo iko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile kusema *business of a livestock producer,* ni wakati gani inakuwa ni biashara. Je, yule mfugaji wa kawaida ni mfanyabiashara? Mtu mwenye ng'ombe 1,000 ni mfanyabiashara? Mtu mwenye ng'ombe 20 ni mfanya biashara? Sheria haisemi. Kwa hiyo, itakuwa kwamba hii haiko bayana watu wengi sana wataingia katika matatizo na hapa nimegundua kwamba Sheria hii kuna adhabu, miezi sita jela. Kwa sababu labda hukuandikishwa na Bodi kama wewe ni *producer* wa *livestock.* Si hivyo tu watu wanaokwenda kwenye minada namna gani. Je, mtu akiwa na ng'ombe watano anawatoa Mwamashimba kuzipeleka Mnadani je na huyo amekuwa ni mfanyabiashara na yeye atahitaji leseni ya Bodi.

Je, mtu ambaye anaswaga ng'ombe wake kutoka mnada wa Bariadi kwenda labda mnada wa Igoma na yeye atakuwa ni mfanyabiashara na yeye atahitaji leseni ya Bodi? Yote haya ni lazima yawekwe bayana. La sivyo tutaweka watu wengi sana katika matatizo ambayo ni ya kisheria. Kwa hiyo, hiyo *section number 17* Mheshimiwa Waziri ningependa uifanyie kazi. Muwaelimishe watu kibayana kabisa juu ya jambo hilo.

Jambo lingine ambalo ningependa kuzungumzia nilikuwa namwuunga mkono Mheshimiwa William Shellukindo amezungumzia kwa ufasaha sana kwamba Bodi hii inapewa fedha kutoka Serikalini kama Bodi inapata fedha kutoka Serikalini basi ni lazima *accounts* zake tuzione hapa ndani ya Bunge. Kwa sababu ni sisi ndiyo tunaotoa hizo fedha. Lakini licha ya hivyo hakuna mahali ambapo ni nani atakayesema au atakayeiambia Bodi isiweke kodi kubwa sana kwa watu ambao wanafanya biashara hizi za ng'ombe au kwa wafugaji kwa ujumla. Hilo pia ningependa nipewe maelezo na Mheshimiwa Waziri. Ili isiwe hii tumetoa kodi kwa ajili ya ng'ombe tumetoa kodi ambazo ni za lazima lakini isiwe tena mgongo mwingine tofauti, mkondo mwingine wa kuweza kuwatoza wafugaji wetu fedha ambazo siyo za lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiondoka hapo pia ningependa kuhamasisha jambo lingine kwamba viwanda hivi vinavyozungumziwa kujenga, tungependa zaidi viwanda hivi viweze kuwa viwanda vya wazalendo sisi tumekuwa watazamaji kwa muda mrefu na uwezo wa Watanzania kuweza kujenga mitaji upo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi hapa pamekuwa kwa mfano watu wa *Poland Cement* wanatafuta fedha kwa ajili ya kuongeza mitaji yao. Mpaka wamerudisha fedha kwa wananchi, wale ambao walioomba hisa mia moja, imekubaliwa tu asilimia 31. Ndiyo kusema uwezo wa Watanzania kuweza kutoa mtaji kwa kampuni ambayo kweli inaonekana kwamba ina uwezo wa kuweza kuendesha biashara katika nchi hii ambayo italeta fedha mtaji huo upo na zaidi mtaji kwa wafugaji kuna watu wengi sana *Sukumaland* ambao wana mamilioni ya ng'ombe wakihamasishwa vizuri, hata kwa kupitia ushirika na mambo kama hayo mimi nina hakika wanaweza wakatoa mtaji utakaoridhisha kabisa na wao pia wakawa basi ndiyo wenye kiwanda siyo tu kila mtu amezungumzia viwanda, tuzungumzie watu wa nje.

La mwisho, mimi kabisa naunga mkono alivyosema Mheshimiwa Michael Laizer. Kuna maeneo mengi sana ya Serikali, Ng'wabuki kwa mfano kuna ng'ombe wangapi wa Serikali mle? Kwa nini hiyo Ng'wabuki isikubaliwe baadhi ya wafugaji na wenyewe waweze wakachungia katika hiyo ranchi kubwa ya Ng'wabuki na sehemu zingine ili sasa hivi maana yake wakulima wote wafugaji wamebanwa, wamebanwa na wakulima, wamebanwa kila mmoja. Sasa hakuna mahali ambapo ng'ombe kuna nafasi yake. Sehemu kwa mfano ukichukua sehemu ya Ramadi kule kila siku kuna ugomvi juu ya Kijeleshi, kwa nini tusiweze kutenga eneo sehemu ya Kijeleshi kule ambapo wafugaji wetu wa Magu na wenyewe wakaweza kupata nafasi ya kuweza kuchunga na kuweza kunenepesha ng'ombe wao?

Kwa hiyo, ninachotaka kusema Wizara hii *actualy* iwe *pro-active* sio *negative,* sio kuzuia, kuzuia, kuzuia. Tunataka sasa hivi kusukuma wafugaji ili na wafugaji na wenyewe waweze wakaweza kuheshimika katika Taifa hili kwa sababu wana mchango mzuri sana katika uchumi wa Taifa letu. Kwa misingi hiyo, kama Mheshimiwa Waziri ataweza kuniridhisha kwamba ibara ya 17 siyo kitanzi cha kila mfugaji, basi nitaweza kufikiria kuunga mkono Sheria hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kwanza kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia siku ya leo katika Muswada huu. Lakini vilevile nichukue nafasi hii kuwapongeza Viongozi wa Wizara hii hasa Mheshimiwa Anthony Diallo, kwa kukubali mabadiliko ya kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii kuja katika Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo na mabadiliko yote ambayo yamewakumba Mawaziri wengine tunaamini yote yamefanywa kwa nia njema kwa kuongeza ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu kwa kusema kwamba sekta hii ya mifugo miaka ya 1970 na 1980 ilikuwa ni sekta moja kubwa sana na jinsi tulivyoanza kuiendesha tulianza kuiendesha kwa mfumo mkubwa ambapo kwa kweli yalikuwepo makampuni mengi sana kwa bahati nzuri niliwahi kufanya kazi katika sekta hii. Kwa hiyo, ilikuwepo kampuni ya Ranchi ya Taifa, kulikuwepo na Kampuni ya Taifa ya Ng'ombe wa Maziwa kulikuwa na kampuni ya Kuku. Kulikuwa na kampuni ya Maziwa na kampuni hii ya ng'ombe wa maziwa nayo ilikuwa na mashamba kadhaa nayo pia kila shamba lilikuwa ni kampuni. Kulikuwa na kampuni pale Ruvu, kulikuwa na kampuni Ngerengere.

Kulikuwa na Kampuni Iwambi, Ihimbo, Kitulo, Azimio Ranchi kule Tanga, Utegi na kadhalika.

Sekta hii ilitusaidia sana katika miaka hiyo, kwa sababu kwa kweli ilikuwa ni sekta ambayo ilitoa ajira. Ukitazama utitiri wa makampuni haya na yote yalikuwa na menejimenti yake na wafanyakazi wake, sekta hii ilitoa ajira sana kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wengi tulikuwa tunajiuliza hivi kweli kwa kuwa na kampuni zote hizo ambazo nimezitaja kampuni hizi zitakuwa endelevu? Kwa sababu ili uweze kuendesha kampuni vizuri lazima kampuni hiyo iweze kujiendesha yenyewe hasa kwa kuzingatia mapato yake na matumizi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yametufikisha hapa ambapo tumefika, makampuni mengi hayo yamekufa, hayakuweza kuhimili na yameshindwa kujiendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya hata baadhi ya makampuni hayo mengine tumejaribu kuyabinafsisha lakini hatujapata wanunuzi. Lakini pengine ni vema tukakumbushana tu kwamba kuvunjwa kwa ile Mamlaka ya Mifugo *(LIDA)* ambayo ndiyo ilikuwa mhimili wa sekta hii ya mifugo na ndiyo iliyokuwa ikibeba dhamana ya Sheria yenyewe ya mifugo.

Mheshimiwa mwenyekiti, hiyo peke yake ilikuwa inachangia kuwafanya wawekezaji kusita kuwekeza katika viwanda vile vya nyama vilivyokuwa hapo awali tulivyokuwa tumekusudia kuvitaifisha. Kwa sababu sheria ilikuwa haipo na ile sheria ambayo zamani ilikuwepo mhimili wake *Livestock Development Authority* ilivunjika. Kila mwekezaji akitazama sheria yenyewe iko wapi inayomlinda yeye kuwekeza katika sekta hii ya nyama alikuwa haioni.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii ya kuwa na Muswada huu unaotuelekeza kutengeneza sheria hii ni hatua muhimu sana ambayo nina uhakika itatusaidia kuwezesha wawekezaji kukubali kuwekeza katika sekta hii ya mifugo hasa katika viwanda vya usindikaji hasa wa nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii ni muhimu sana na nimemsikia Mheshimiwa Waziri hapa anazungumzia uwezekano wa kutaka kufufua viwanda hivi, tuvikarabati, tuvitegeneze viweze kuwa katika hali ambayo itamvutia mwekezaji na vilevile mapendekezo au nia ya kujenga kiwanda kingine kule Dar es Salaam eneo lile la *KILTEX.* Lakini ni vizuri tukatazama sekta hii inakabiliwa na matatizo gani ili tuweze kuwa na kiwanda pale Dar es Salaam. Kwa mfano mifugo hii inatoka wapi, mifugo hii itatoka katika maeneo ya Shinyanga, mifugo hii itatoka katika maeneo ya Dodoma kuelekea Dar es Salaam kwa sababu eneo lenyewe la Dar es Salaam lina uhaba wa kuweza kupata mifugo ya kutosheleza kwa ajili ya kiwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini je, tunayatambua matatizo yanayoikabili sekta hii ili kuweza kufikisha ng'ombe Dar es Salaam kwa ajili ya kiwanda hicho, kunahitajika sana usafiri ulio rahisi na usafiri ambao ni wa gharama nafuu ni usafiri wa reli. Hebu

tuangalie reli yetu ya kati iko katika hali gani itaweza kuhimili kweli kazi hiyo ya kusafirisha ng'ombe kuwafikisha Dar es Salaam kwa ajili ya kiwanda tunachokusudia kujenga Dar es Salaam. Vinginevyo tutatumia malori makubwa na gharama kubwa, uharibifu kwenye barabara zetu na inawezekana tukafika mahali kiwanda kikashindwa kufanya kazi kwa saa 24 kama ambavyo wawekezaji wangekusudia kufanya.

Kwa hiyo, tutazame hilo kama moja ya tatizo kubwa katika sekta hii. Lakini yapo pia matatizo mengine je, tunayafanyia kazi. Ipo migogoro mikubwa sana kati ya wafugaji na wakulima je, tunachukua hatua gani ya kuhakikisha kwamba tunatatua migogoro hii ili kuhakikisha kwamba wafugaji wanapata hadhi na heshima na wanaendelea kufuga ili mifugo iendelee kupatikana kwa dhamira hiyo ya viwanda tunavyokusudia kuvijenga.

Mheshimiwa Spika, lakini tuangalie vilevile suala la muhimu sana. Unapotaka kujenga kiwanda na unadhamiria soko la nje, jambo kubwa la msingi ambalo lazima kulitazama je, tuna mikakati gani ya kuhakikisha ubora wa nyama? Kwanza, mifugo yenyewe iweze kutoa nyama yenye ubora unaotakiwa na kukubalika katika soko la nje. Viwanda vyetu hivi vingi tunavyotaka kuvijenga, tunavijenga kwa dhamira ya kusafirisha nje ya nchi nyama. Kwa hiyo, lazima tuangalie je, tumejiandaa vipi kwa ubora huo ili tukijenga viwanda basi tunayo nyama ambayo ubora wake unakubalika katika masoko ya nje. Haya ni mambo muhimu ambayo lazima tuyatazame hivi sasa, tuyafanyie maandalizi mazuri ili mafanikio yaweze kuwa mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika soko la hapa nchini, kwa Sheria hii ambayo tunakusudia bila shaka itapita na itakubaliwa, yapo mambo ambayo lazima tuyaangalie, tusitazame ubora wa kuuza nyama nchi za nje tu tukadhani soko la ndani siyo muhimu sana. Tumefanya mipango gani ya kuhakikisha kwamba ubora wa nyama inayouzwa katika mabucha ya hapa nchini unazingatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda katika bucha nyingi sana ukiwa muangalifu sana unaweza ukashindwa kula nyama. Nyama ambayo inawekwa juu ya gogo inakatwakatwa na shoka, vipande vya magogo vile vinachanganyika katika nyama unayonunua kuongeza hata uzito wa nyama hiyo, lakini umebeba vipande tu vya magogo. Lakini vilevile inachanwa chanwa na vipande vidogo vidogo vya magogo ambavyo vikiingia una hatari ya kula na kuhatarisha maisha yako.

Kwa hiyo, sheria yetu inasema nini kuhusu hilo. Tumejenga mkakati wa kuhakikisha kwamba sasa tunasimamia afya bora kwa walaji wa soko la hapa nchini kwanza kabla hatujafikiria kwenda nje ya nchi. Kwa hiyo, ni vizuri sheria hii ikatazama pia taratibu na kanuni za wauzaji wa nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Dodoma kuna bucha moja ya mfano imeanzishwa hivi karibuni kama miezi sita iliyopita. Ni bucha ambayo ukataji wa nyama siyo wa kutumia mapanga na mashoka, wanatumia mashine nzuri za kisasa huu ndiyo utaratibu ambao sheria yetu inapaswa kuelekeza wananchi wetu ili kulinda afya za wananchi.

Sasa ipo bucha moja hapa Dodoma ambayo nimeona na ni imani yangu kwamba sheria hii itatoa maelekezo na Wizara inayohusika itatoa mwongozo ili bucha za aina hiyo ziwe ndiyo bucha tunazotarajia zitawahudumia wananchi na si kwa Dodoma pekee yake bali kwa nchi nzima lazima tubadilike, lazima tuheshimu afya za Watanzania, lazima sheria zetu ziheshimu na kuthamini afya za Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina uhakika kabisa wafanyabiashara hao wakielekezwa watabadilika tu, lakini kama hakuna kitu cha kuwaelekeza, hakuna msisitizo, hakuna usimamizi, wataendelea kufanya kazi katika mazingira ya kizamani kwa miaka yote hata miaka 100 inayokuja, hawatabadilika. Kwa hiyo, tutunge sheria kwa dhamira ya kuwabadilisha na kubadilisha mifumo kwa lengo la kuwaboresha wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine ambalo sheria yetu hii lazima iliangalie, wote tunafahamu ukienda katika mabucha yetu haya nyama zimepigwa mhuri kwa maana ya kuthibitisha kwamba zimekaguliwa, lazima basi kama kweli nyama zinakaguliwa lazima tuwe na usimamizi wa kuthibitisha kweli hizo nyama zimekaguliwa na si kupiga mihuri tu.

Sisi tumeona katika maeneo mengi watu wanachinja wanasema mwite Bwana Afya aje huku, aende kufanya nini, haendi kupima ile nyama anakwenda kupima mhuri ile nyama. Sasa haya lazima tuhakikishe sheria inaweka mikakati ya kuhakikisha kwamba kweli nyama zinapimwa, zinathibitishwa na uthibitisho huo ndiyo baadaye kupigwa mhuri si kupiga mhuri tu kuwababaisha walaji kwamba nyama imepimwa lakini si kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka sheria zetu hizi ziweke maeneo ambayo yatasaidia kwamba haya tunayosema yafanywa kweli. Mabwana Afya kweli wapime nyama. Je, Mabwana Afya hao tunaodhani wanapima nyama hizi katika mabucha wana vifaa kweli vya kupimia nyama kuthibitisha ubora wa nyama hiyo kwamba haina matatizo kwa walaji, wanavyo vifaa, tuna uhakika. Kwa sababu wanapima nyama katika maeneo mengi na watu wa vijiji vilevile wanayo haki ya kula nyama iliyopimwa, je, vifaa hivyo vipo. Wizara inafahamu hilo na inawasaidiaje kuhakikisha kweli hao wanaopima nyama wana vifaa na wanapima nyama kwa uhalali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nisisitize hayo, niliona ni muhimu sana. Lakini naomba kusema kwamba katika Mikoa ambayo miaka kadhaa iliyopita haikuwa na mifugo mingi ilikuwa ni Mkoa wa Tanga. Sasa Mkoa wa Tanga umebadilika, tumebadilika, tuna wafugaji wazuri, tuna ng'ombe wazuri, tuna maziwa mengi, tuna Chama cha Ushirika cha Mkoa cha Wafugaji wa Mkoa wa Tanga kinafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Muheza tuna Chama cha Wafugaji Wilaya ya Muheza, tuna matawi ya wafugaji kule Amani, tuna matawi ya wafugaji Muheza Mjini, tuna matawi ya wafugaji Ngomeni na tunapata maziwa mengi, ninawapongeza sana na kuupongeza Mkoa wa Tanga kwa maziwa ambayo yanaitwa

*Tanga Fresh,* haya yanapatikana katika maeneo mengi kutoka katika Mkoa wa Tanga. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba kuwathibitishia ndugu zangu kwamba Mkoa wa Tanga sasa ni wafugaji wenzenu, tunawathamini na tunafurahia Sheria hii mpya. Tunategemea kwamba Sheria hii itaangalia pia mazao yanayotokana na mifugo yenyewe badala ya kudhani au tukafikishana mahali tukaanza kufikiria kuanzisha tena Sheria itakayoitwa *the Milk Act*, maana yake hii ni ya nyama, je, maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, naunga mkono Muswada huu ambao naamini kabisa utatusaidia wote. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii nami kuchangia Muswada huu ulio mbele yetu mchana huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kiasi kikubwa sana sehemu ya mambo niliyotaka kuyazungumzia yamekwishazungumzwa. Sasa na mimi labda nikanzie tu pale ambapo ninaona kuna umuhimu wa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu kwa wakati huu pamoja na kwamba umechelewa sana kwa sababu Sekta ya Mifugo ni sekta muhimu katika nchi. Lakini Waswahili wanasema bora kuchelewa kuliko kutokufanya kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianzie na suala zima la jinsi nilivyosoma *Act* hii na kuchanganyikia kidogo hasa inaposema: "*meat and meat products.*" Sasa hapa kwenye *meat and meat products* nimekuwa napata tatizo, je, maziwa ni *meat products?* Kama ni *meat product* sawa, lakini ufahamu wangu ni kwamba maziwa ni *livestock product*. Sasa kwa maana hiyo tungekuwa wazi basi ngozi ni *livestock product,* maziwa ni *livestock product.* Hivi haijitokezi waziwazi kwenye Muswada huu.

Kwa hiyo, ningeshauri tu ili tuondoe ule wasiwasi wa kutafsiri vinginevyo basi Muswada huu ujitokeze wazi unazungumzia nini kwenye *meat products.* Je, maziwa na ngozi vinahusika? Kwa sababu hivi vinakwenda pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia kuboresha maisha ya Watanzania hasa wakulima na ndani yake wamo wafugaji, katika wafugaji kuna eneo la nyama ambalo limetajwa vizuri sana, lakini vilevile kuna eneo la maziwa. Tukiwa na utaratibu mzuri wa kuwafuga ng'ombe wetu na kuboresha upatikanaji wa maziwa kwa wingi kutoka kwenye ng'ombe mmoja tutaongeza vipato vya wafugaji wetu kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo ningependa nilisisitize linatokana na jinsi ambavyo nilitaka nipendekeze *Section (1)* ukurasa wa 7 kwenda ukurasa wa 8 *functions of the Board shall,* eneo (l) linasema: *"To promote co-ordinate the*

*development of small, medium ana large scale livestock producers trader and meat processors*:" Kwa maana ile ambayo nimesema tukiwa tunataka kuwasaidia hawa basi tuwasaidie vilevile pamoja na uzalishaji wa maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *section* inayofuata nyingine ambayo ningependa kuzungumzia ni eneo la 4, *section 16 4(b)* inasema: "*liaise with other government institutions to obtain and keep a register of* – halafu inaonyeshwa hapo nataka niende mpaka mwisho romani (vii) *to keep register of abattoirs.* Sasa mimi nilitaka nishauri kwamba suala lisiwe ku- *keep register* tu za hizo *abattoirs* ila vilevile iwe ni ku-*set acceptable standards* za hizo *abattoirs* na kuzifanyia *periodic inspection* ku- *ensure* kwamba zina-*comply* na *the set* s*tandards*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu huko ndiko mambo yanakoanzia ng'ombe aliyechinjwa katika mazingira mazuri akawa *handled* vizuri nyama yake itakuwa nzuri na ya uhakika. Lakini tusiishie tu *keep registers* za *abattoirs.* Mfano, Tabora Mjini kuna *abattoir* unaweza ukawa unayo kwenye *register* yako lakini suala ni kwamba je, ile hali yake ilivyo vile ndiyo hali ambayo Wizara au Serikali ingependa kweli *abattoir* ya Tabora Mjini iwe vile? Hali hairidhishi. Kwa hiyo, tusiishie tu kwenye kuwa na *register* ya hizo *abattoirs*, tu *set standards* na tuhakikishe kwamba hizo *standards* zinakuwa *complied with.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Muswada huu, msisitizo umewekwa zaidi kwenye *meat.* Lakini tunapozungumzia wafugaji ni pamoja na ng'ombe mwenyewe kabla hajachinjwa kwa sababu ng'ombe akishachinjwa ndiyo unapata nyama. Lakini ng'ombe mwenyewe hatumfanyi biashara kama tuna mfanyiabiashara basi iko haja ya kujenga mazingira kwamba ng'ombe mwenyewe kama mfugo au mbuzi au kondoo waweze kutupatia fedha nyingi za kigeni katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi yetu ambao tumekwenda kwenye soko ambalo liko jirani sana, soko la *Middle East,* kuna kipindi katika soko la *Middle East,* Saudi Arabia pale katika kipindi cha mwezi mmoja mpaka miezi miwili walikuwa wanachinjwa mbuzi na kondoo takriban milioni tatu mpaka milioni tano. Soko hili liko jirani sana na Tanzania, lakini mbuzi na kondoo wanaochinjwa pale Saudi Arabia wengi wao wanatoka Argentina, Brazil na New Zealand. Swali la kujiuliza ni kwa nini sisi Watanzania hatuchukui faida ya kuwa karibu na soko hilo tena la uhakika? Mbuzi tunao na kondoo tunao , je, hatuzihitaji hizo fedha za kigeni kwa kupeleka mbuzi wetu na kondoo huko *Middle East?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunapozungumza kwamba Muswada unasema utafanya *market research,* sawa tunakubali. Lakini mimi nataka nianze kwa kuwashauri wale watakaofanya *market research,* soko liko kule *Middle East* wanatakiwa kondoo wengi sana na mbuzi wengi sana. Ni suala la kutengeneza mikakati ya kuuza kondoo hao na mbuzi hao tena kwa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia katika Muswada huu na mimi ninaunga mkono kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi ningependa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika Muswada huu. Vilevile naipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kuleta Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kupoteza muda ningekwenda moja kwa moja kwenye hoja zangu. La kwanza, ni ile kwamba Tanzania ni nchi ya tatu kuwa na ng'ombe wengi, lakini hatupati manufaa hayo. Botswana wana ng'ombe wasiozidi milioni tatu, lakini Botswana ndiyo inayoongoza katika Kanda hii kwa kuuza nyama katika nchi za nje. Vilevile nchi yenyewe sehemu kubwa ni jangwa, lakini wanafanya vizuri sana katika sekta hii ya nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nieleze ingawa mazungumzo na Muswada wenyewe unahusu nyama na bidhaa zake. Mimi ningependa niseme nyama bora itatokana na ng'ombe bora. Kwa sababu kama ng'ombe wetu ni hawa wanaoswagwa wanatembea kilometa kadhaa hawajapata maji, hawajala majani hawawezi kutoa nyama nzuri. Kwa hiyo, lazima turudi kwenye ng'ombe wenyewe kwamba ng'ombe wa Tanzania wawe bora tena hao hao mimi sizungumzii habari ya kuchinja ng'ombe wa Wakusuma au kuwapunguza hao ng'ombe wa Wamasai. Ng'ombe waliopo sasa hivi wanatosha kutupa fedha za kigeni. Kwa hali yetu wala hatuhitaji kupiga kelele ya kuanzisha mashamba mapya. Ng'ombe waliopo hawajashughulikiwa vizuri tena mambo ya msingi tu. Mara nyingine baadhi ya watu wakija wanadanganya na mimi siwezi kuelewa kwa nini wataalam siku hizi wanakubali. Ng'ombe aliyefugwa ili azae vizuri, chakula chake siyo mashuda. Chakula cha ng'ombe anayetakiwa azae vizuri ni majani bora. La pili, aogeshwe na apate madawa yote ya msingi ndiyo ng'ombe anakuwa mzuri.

Sasa sisi ng'ombe wetu majosho yaliyosemwa hebu wataalam, mimi namwomba Waziri na Waziri ni Msukuma anajua ng'ombe kwa hesabu ya majosho, leo wakati wa kujibu swali lile Wizara imesema hivi: "wana majosho 592." Sasa naomba atufanyie hesabu na atupe jibu leo, ng'ombe milioni 17 watawaogesha kwa majosho 592, ni kichekesho. Kwa asilimia kubwa ya ng'ombe wetu kwa jambo ndogo tu ambalo ndiyo baya sana kwa mfugaji ni kutokuogesha ng'ombe. Kwa hiyo, majosho haya hayatoshi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Serikali imefanya vizuri sana kuamua kutoa ruzuku kwa ajili ya dawa kwa wafugaji pamoja na dawa za kuogesha. Lakini mimi ninavyoona ni kana kwamba jambo hili linakuwa kama siri. Namna gani ruzuku hii itawafikia wafugaji, inakuwa kama siri. Kwa mfano, leo tunaambiwa itatolewa *tender,* sasa *obviously* watakaotangaziwa *tender* na watakaonunua *tender* hizo ni wafanyabiashara tu. Wafanyabiashara watanufaika kwa fedha ya Serikali na siyo wafugaji wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naomba Serikali itueleze wakati wa kujibu juu ya Muswada huu utaratibu gani umetengenezwa ambapo Serikali yenyewe ina hakika kwamba madawa hayo yatawafikia wafugaji. Mimi nashauri kwa sababu hatujui wangekuwa wametwambia utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua mimi nafuga lakini mpaka sasa mimi sijui ni utaratibu gani ambao utatumika sisi wafugaji kupata dawa. Nimekuwa nikienda mara kwa mara Wizarani kuuliza watueleze, wanasema msubiri tutakwambia . Sasa kwa nini iwe siri? *Tender* zinatangazwa kwenye magazeti ya Dar es Salaam, mtu wa Rukwa ana muda gani wa kusoma gazeti aone kuna *tender*. Maana miongozo hii ikipelekwa Mikoani kwa Wakuu wa Mikoa watachukua *incentive* ya kuwambia wafugaji wao utaratibu ambao unafaa kutumiwa na mimi nitashangaa kama Mkoa wa Rukwa atatafutwa mtu Dar es Salaam kutuletea madawa kule lazima atafutwe mtu wa kule kule Rukwa na kila Mkoa upate *supply* wake wenyewe, hapana kutuletea watu wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunazungumza habari ya ruzuku ya mbolea, matatizo ni kwamba mbolea yote wanapewa *tender* watu wa Dar es Salaam wala si wakulima wale hawajui matatizo ya wakulima lakini ndiyo wanaopewa *tender*. Sasa mimi naomba tusifanye makosa kwa madawa ya wafugaji. Ni kosa kubwa sana. Ubora wa ng'ombe wetu utatokana na matunzo. Hilo moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ningependa kuungana na Mheshimiwa Mbunge wa Tabora alivyosema ni sahihi labda mimi niseme kwa kuanzia pale alipofika. Mimi nadhani ni sahihi tukisema Tanzania *abattoirs* tukisema hivyo ndiyo itakuwa sawa, hakuna *abattoirs* hapa Tanzania, kuna machinjio ya kuangusha ng'ombe kwenye matope. Kama ukitaka kuwa *fair* maana yake tunapozungumza *abattoirs* tuzungumze *abattoirs* ya Dodoma kubwa, *abattoirs* ya Sumbawanga kubwa, *abattoirs* ya Arusha ni kubwa. Mimi nataka tuzungumze *abattoir* ya kawaida ya Mjini Dodoma na Mpwapwa. Kwa sababu *abattoir* zipo aina mbili, kuna zile za kawaida na yale makubwa *commercial* na zile ambazo ni *normal.*

Sasa kwa mfano, Mji wa Tabora mahitaji yao ya ng'ombe ni ng'ombe 50 au 40 kwa siku, ijengwe *abattoir* ya kisasa ya kiwango hicho hicho. Maana yake tukianza kuzungumza hapa tuzungumze *abattoirs* ya *export*. Mimi nataka tuanzie ile ya watu wa Tanzania wenyewe wapate nyama kutokana na *abattoirs* za kisasa nzuri *medium scale* na *small scale*. Sasa hizi nyingine kubwa kwa mfano, ile mimi ninayotengeneza Sumbawanga hiyo itakuwa kwa ajili ya *export.* Lakini tuzungumze na *abattoir* ndogo za kawaida. Kwa hiyo, mimi ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge alivyosema kwamba usajili kitu kimoja na *abattoirs* zenyewe na ubora ni kitu kingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, nyama inayotengenezwa na bidhaa zake kuna namna nyingi. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nataka kushauri Serikali kwa kuwa hizi *abattoirs* zitasajiliwa tuanze kuzikagua na kuona ubora wa nyama inayotoka katika hizo *abattoirs* na Serikali katika hili mimi *I declare my interest*. Mimi ningependa Serikali isimamie vizuri jambo hili idhibiti kabisa ili huko nje tunakopeleka nyama tusije

tukaharibu masoko. Lazima *quality* ifanane na *exports*. Kwa hiyo, mimi nataka Serikali isimamie *abattoir* hizi zifanane na dunia ya leo. Nyama itakayouzwa nje ya nchi iipe sifa Tanzania kwa sababu tuna nafasi kubwa sana ya kuleta fedha za kigeni kutokana na ng'ombe ambao wapo Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafanyaje ni kufanya ukaguzi kwa mfano, sisi tunajua kwamba kuna kampuni sitaki kuitaja. Kuna kampuni wanauza *sausages*, zile *sausages* ingawa zimeandikwa nyama, lakini hapana, *sausages* zinatengenezwa kutokana na soya. Mimi najua hiyo nimeona zinatokana na soya asilimia 5 au 10 tu ndiyo nyama. Lakini watu wanauziwa kama ni *sausage* za nyama. Sasa na mambo haya itabidi vilevile na Serikali nayo itembee kwenye *abattoirs* ione. *(Makofi)*

Lakini vilevile naomba Serikali ijenge mazungumzo na iwe karibu sana na wenzetu wenye viwanda vya nyama ili iweze kujua tangu mwanzo matatizo yao na namna inavyoweza kuwasaidia. Haitoshi kusema kwamba Serikali haifanyi biashara, hayo maneno Mheshimiwa Waziri naomba ayafute acheni kusema Serikali haifanyi biashara, hapana. Semeni Serikali haimiliki viwanda, lakini mfanyabiashara mkubwa lazima iwe Serikali yenyewe. Kwa vipi, Serikali ndiyo inatakiwa iunganishe wazalishaji na Balozi zake na nchi mbalimbali. Rais ameanza utaratibu mzuri sasa kila akisafiri anakwenda na wafanyabiashara wanapata nafasi ya kueleza watakayoyafanya. Kwa hiyo, nataka wasiwe wanasema Serikali haifanyi biashara, waseme hivi Serikali itasimamia biashara ifanikiwe.

Sasa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko maana yake nini? Maana kama Serikali haiwezi kusaidia wenye viwanda kuuza basi hakuna haja ya kuwa na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, sasa hili neno masoko limewekwaje. Neno masoko maana yake wenye viwanda wasaidiwe kuuza bidhaa kwa ufanisi kama hatufanyi hivyo hakuna maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, mimi sitaki kusema zaidi kwa sababu mimi ni *interested party* na mtu huwezi kujisifu mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ila mimi nataka kusema neno moja, sisi wanasiasa wa Tanzania tuwe mfano kwa vitendo na wale wanaojaribu wasipigwe vita na wenzao katika siasa. Jambo hili ni dhambi kubwa sana katika nchi, wewe huwezi kuanzisha kitu chochote, aliyeanzisha unampiga vita huoni kama unachuma dhambi. Maneno yetu ni tofauti na vitendo vyetu. Sasa viongozi wanapotokea kuwa ndiyo wa kwanza kupiga vita watu wanaohangaika wanajenga mfano mbaya kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili mimi nataka niliseme waziwazi tuhangaikie uchumi, tuache fitina za kisiasa katika uchumi. Ng'ombe ni ng'ombe, siyo mbuzi, mbuzi ni mbuzi siyo kondoo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, mimi naunga mkono Muswada huu. *(Makofi)*

**MHE. JOYCE N. MACHIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nitoe shukrani zangu za dhati kwa Serikali kuwasilisha Muswada huu ambao ni wa muhimu katika Sekta ya Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona nisimame niseme haya kwa sababu na mimi ni mmoja wa wale walengwa wa Muswada huu kama mwanashinyanga kwa mfano kwa upande wa wafugaji wa ng'ombe ili niweze kusema machache na kuwapa changamoto wafugaji waliopo Shinyanga, Mwanza, Kagera, Mara na Mikoa mingine ambayo inajishughulisha na ufugaji. Hasa nitajikita zaidi katika Mkoa wangu wa Shinyanga ambao umekuwa ni tatizo kubwa katika nchi nzima kwa vile wana mifugo mingi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, si tatizo kwa wanashinyanga kuwa na mifugo mingi lakini kupitia Muswada au Sheria hii naomba niwafariji wafugaji wa Shinyanga kupitia kauli ya Serikali ya kufufua kiwanda cha nyama cha Shinyanga basi wajiandae rasmi kwa biashara ili kuweza kutumia hiki kiwanda kupitia hiyo mifugo yao na wasihangaike kama wanavyohangaika sasa hivi kusafirisha mifugo kama Waheshimiwa wenzangu waliotangulia kuchangia wamekuwa wakifanya biashara kupitia kwa watu mbalimbali ambao wamekuwa hawakidhi matakwa ya biashara na hivyo kupelekea kuendelea maskini hawa wafugaji wa Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Muswada huu mimi niombe tu kitu kimoja kwamba niwashukuru Waheshimiwa Wabunge waliotangulia kuzungumza wamezungumza kwa upana sana suala hili la Sheria ya Nyama. Lakini cha msingi ni kwamba pamoja na kuwa tumefikia kujadili nyama, lakini pia tulitakiwa tuanzie kuzungumzia mifugo kwa maana ya kupata mifugo kama wenzangu walivyotangulia kusema.

Kwa hoja hiyo, mimi sina mazungumzo marefu bali ninamwomba Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii ya Maendeleo ya Mifugo apate nafasi ili kuwaunga mkono hawa wananchi waliopo Kanda ya Ziwa na hasa Mkoa wa Shinyanga ambao umekumbwa na ukame na kukosekana kwa maeneo ya malisho, awatembelee wafanyabishara wadogo wadogo waliopo barabara za Bukombe, Kahama, Shinyanga Mjini na Mwanza ili aone bidii wanazozifanya. Kupitia maandalizi ya kiwanda hiki cha nyama kitakapokuwa kimekamilika waweze kufaidika vipi kwa kwenda kutia changamoto aidha kufanya mkutano mkubwa sana ambao utawahusisha ili waweze kujiandaa na hii biashara ya kupitia hicho kiwanda kwa sababu sasa hivi wananenepesha ng'ombe kwa njia ambazo wanabuni wao wenyewe bila ushauri wa kitalaam lakini mpaka hapo wanakuwa na ng'ombe ambao wanaonekana ni bora.

Kwa hiyo, mimi namwomba kabisa Mheshimiwa Waziri aweze kuwatembelea ili akatie changamoto na atoe sera zilizo za ukweli na utaalam zaidi ili waweze kuungana na wafanya biashara wengine kama wenzangu walivyozungumza ng'ombe hawa wa

Shinyanga wanakwenda Comoro, Kenya lakini wanakwenda hivyohivyo kwa njia za panya. Sasa mimi namuomba kabisa Mheshimiwa Waziri aone umuhimu wa kuutembelea huu mkoa na kupunguza adha ambazo zinajitokeza katika mikoa mingine kupitia wafugaji hawa wa Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hoja hizo fupi naomba kuunga mkono hoja iliyopo mezani kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI - MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Joyce Nhamanilo Machimu, naona Shinyanga imecharuka na sasa anafuata Mheshimiwa Emmanuel Jumanne Luhahula, kutoka Bukombe, nadhani nitakuwa na dakika kumi hivi kama Mheshimiwa Zaynab Matitu Vulu, zitakutosha nitakuomba uzitumie. Mheshimiwa emmanuel Luhahula karibu.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Muswada huu.

Awali ya yote napenda pia kuipongeza Serikali kupitia Waziri mhusika wa Wizara ya Maendeleo ya Mifugo, Naibu Waziri, Makatibu na Watendaji wote kwa pamoja kwa kuandaa Muswada huu na Kamati ambazo zimepitia Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo ya Muswada huu kweli ni mazuri na ninaona yanafurahisha, lakini ninachotaka kusema katika Muswada huu tuna kila sababu ya kuwaelimisha wafugaji. Kama walivyoendelea kusema wenzangu ni kwamba ili tuweze kupata nyama ni lazima tuwe na mifugo wazuri. Lakini hawa mifugo wetu wamekuwa ni wa kutangatanga sana nafikiri kama walivyoendelea kusema wenzangu kumekuwa kama kuna vita kati ya wafugaji na Serikali, wafugaji wengine wanaendelea kuhama wanaendelea kusafiri na mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunapokwenda kupitisha Muswada huu kuwa Sheria ya Nyama tunaamini kwamba tunatakiwa kwanza mifugo tuliyonayo ndani ya nchi yetu tuiboreshe. Wamesema kwamba wanaweza wakaanzisha ranchi mbalimbali, kwa uelewa wangu nilikuwa nawaza je hizi ranchi zinazotaka kuanzishwa tutachukua baadhi ya wafugaji maarufu waweke mifugo yao pale ili iwe mfano na changamoto kwa wafugaji wengine? Kwa sababu, vinginevyo wapo wafugaji tuliowakuta sehemu kama za Ihefu na kadhalika wana mifugo kati ya 5000 na kadhalika, lakini hii mifugo wafugaji wanahangaika nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri ni muda mzuri wa kuiboresha mifugo yetu, Serikali imetamka kwamba watenge maeneo ya wafugaji kila sehemu ili kuweza kuboresha mifugo hii inaweza ikaondoa mgogoro uliopo kati ya Wafugaji na Wakulima. Ni kweli, kwa mfano katika Wilaya ya Bukombe tunayo Mifugo mingi sana lakini maeneo tunayokwenda kuyatenga ni ardhi za watu ambazo tayari walikuwa wanalima wananchi katika maeneo hayo, tunawaza tunapokwenda kutenga maeneo haya hao wenye maeneo wanakwenda kulima wapi? Au wenye maeneo wanapata fidia ipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nilikuwa na wazo au ushauri katika hili kwamba kama inawezekana kwa sababu maeneo mengine bado yapo na yana misitu mikubwa tunaweza tukachukua sehemu moja ya hifadhi tukatenga kwa ajili ya wafugaji ili tuweze kuangalia kama mifugo hawa ng'ombe, mbuzi na wanyama wengine tunawapa umuhimu katika Taifa letu, kwa nini tusiangalie maeneo ambayo yana hifadhi kubwa sehemu mojawapo tukatenga likawa eneo la wafugaji si tu kwa wananchi wa Wilaya hiyo bali hata wa maeneo mengine wakaweka mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia katika biashara hii kipengele cha 17 ambapo wenzangu walipazungumzia kwamba wanaotakiwa kufanya biashara hii ni lazima wapate *registration*. Lakini tunachofikiria ni kwamba tunataka kuboresha wafugaji wetu na wafugaji wetu ili waweze kuuza mifugo yao ili waweze kupata faida kutokana na mifugo yao ni lazima wauze, lakini kwa sababu wengi wetu hawaelewi utakuwa itakuwa ni tatizo sana la kuweza kuwanufaisha wafugaji hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kushauri Serikali kama inawezekana hata katika utoaji wa leseni hizi za kufanya biashara ya nyama ikiwezekana basi tupitie vyama vya ushirika vya wafugaji katika maeneo husika. Vinginevyo tutaachia wafanyabiashara wakubwa kutoka mjini ndiyo watakaokuja kuchukua leseni hizi na matokeo yake wataanza kunyanyaswa sana wafugaji wanaokaa na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafikiri tunahitaji sana tuboreshe mazingira haya kwa sababu tukishaboresha mazingira yao tukawaandalia vyama vyao vya wafugaji vikaweza kupata leseni mbalimbali za kufanyia biashara hii ninaamini viwanda vyetu hata vitakavyokwenda kufunguliwa tutanufaika kupitia mifugo yetu iliyopo ndani ya nchi yetu. Maeneo tunayoyatenga ya wafugaji ili mifugo yetu tuinenepeshe na kuiboresha ninaomba basi yazingatiwe kwa kuwekewa miundombinu. Kwa mfano katika Wilaya ya Bukombe tumeshaanza kutenga maeneo, wafugaji wanauliza tunapata wapi miundombinu katika maeneo hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kwa sababu nilihitaji kuchangia kidogo katika hayo naomba Serikali iweze kutuunga mkono hasa wafugaji kuwaboreshea mazingira yao, lingine la kuongezea ambalo alilisema Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya na lile la ruzuku inayotoka basi kila sehemu waweze kutoa mhusika wa kushughulikia uuzaji wa madawa hayo, vinginevyo madawa hayatafika kwa wafugaji wetu na mifugo yetu itaendelea kudhoofika na hata inapokwenda kwenye soko la nyama itaendelea kukataliwa/kupewa bei ndogo. Kwa hiyo, naomba sana Serikali itusaidie na iwasaidie wafugaji wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote napenda niwapongeze watoto wangu wawili Waziri na Naibu wake kwa kushika Wizara ya Mifugo. Nina uhakika hayo *mangombe* sasa yamepata wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ni ya wakulima, wafanyakazi na wafugaji na kila mtu ana haki lakini hofu ninayoiona hawa ng'ombe wanaovushwa hapo kuna mwanangu mwingine amesema labda warushwe kwa ndege au helikopta, lakini mimi wananipa mashaka. Mashaka wanayonipa ni kwamba tunazungumzia suala la kuwa na ng'ombe bora, wenye afya nzuri ili wauzwe kwa wananchi wa nchini Tanzania na hadi masoko ya nje. Lakini bado watu wana utamaduni ule wa enzi za zamani za *Old Stone Age,* ng'ombe anavushwa kutoka Mwanza anapelekwa Uzaramuni au Umakondeni kwa miguu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni alipokuwa anapita alikuwa anasema kwamba mchungaji kachoka, ng'ombe kachoka hii habari yake ni kubwa sana. Sasa mimi wasiwasi wangu ni kwamba tunataka tuwe na ng'ombe wazuri, tunataka tuwe na ng'ombe wazuri, tunataka tuwe na mifugo mizuri ni ninachoomba ni kwamba ni vema tuwe na uhakika kwamba ng'ombe hawa itolewe elimu ya malisho ya ufugaji kwa huko huko waliko ili waboreshe ng'ombe wao vinginevyo tutakuta Tanzania yote inakuwa ya wafugaji. Misitu itapotea, maji tutakuwa hatuna kwa sababu hawa ng'ombe watakwenda mwisho wake wataingia katika vyanzo vya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuchukulie mfano wa Mkoa ninaotoka mimi, mimi natoka Mkoa wa Pwani Wilaya ya Kisarawe kuna Wilaya ya Mafia, kuna Rufiji, Bagamoyo, Kibaha na Mkuranga ng'ombe wapo kiasi si wengi na waliokuwepo hao kiasi wanawatosha watu wa kule kwa ajili ya kupatia maziwa. Lakini sasa tatizo lililokuwepo katika Mkoa wa Pwani ni kwamba Mkoa wa Pwani kuna mambo mawili kuna mito ambayo Watanzania tunaitegemea kupata maji ng'ombe wakipelekwa kuna hatari hivyo vyanzo vya maji vitaharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna maeneo mpaka leo hii tunajiuliza, je, wananchi watapata lini maji safi na salama? Na bado tunachukua ng'ombe tunawapeleka huko na Serikali inasema iko tayari kwenda kuchimba malambo kwa ajili ng'ombe badala ya kufikiria wananchi walikuwa kule. Sasa hapa tunafanya nini? Tunataka kuwajenga wananchi au tunafikiria wale ng'ombe waliokuwa kule? Mimi naomba suala hili liangaliwe sana, ng'ombe watakapofika kwenye yale maeneo wanaweza wakaathiriwa na mbung'o wafugaji hawatakubali watakata miti tunakaribisha tatizo lingine la majangwa katika maeneo yetu, sasa tunakwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachoomba au ninachoomba mimi binafsi kwa niaba ya wenzangu wa Mkoa wa Pwani, wale ng'ombe wa hukohuko waliokuwepo wafundishwe kwa sababu ng'ombe mmoja wataalam wanasema anachukua hekta tano, sasa tuchukue mtu ana ng'ombe kama Wasukuma watoto wangu mmoja anakuwa na ng'ombe si chini ya 7000 wao wanachukulia sifa siyo kwamba wanataka wapate ng'ombe bora wao ilimradi ana ng'ombe wengi hajali. Wafundishwe njia bora za ufugaji yaani njia za kisasa za ufugaji ili tuweze kunusuru maeneo mengine yasiwe majangwa kusiwe na matatizo na kusiwe malumbano kati ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, nafikiri ujumbe umefika naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuleta Muswada huu Bungeni. Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa katika nchi yetu kuna mifugo mingi zaidi ya ng'ombe milioni kumi na nane na mifugo hii inachangia pato la Taifa kidogo sana, je, Serikali imeweka mikakati gani ya kuboresha hali ya ufugaji ili kupata mifugo bora itakayochangia pato la Taifa vizuri zaidi kuliko hali ilivyo sasa, kwa kuboresha huduma ya mifugo, maji madawa, tiba, kinga na malisho bora?

Kwa kuwa Mkoa wa Dodoma una ng'ombe zaidi ya 1,600,000 na mifugo hawa wanaweza kuwakomboa wananchi wa Mkoa wa Dodoma kuondokana na umaskini, je, Serikali ina mpango gani wa kujenga kiwanda cha kusindika nyama hapa Dodoma ili wafugaji wapate soko la kuuza mifugo yao na kuboresha maisha yao?

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga machinjio ya kisasa Wilayani Mpwapwa kwa kuwa kuna ng'ombe zaidi ya 400,000 na Mpwapwa ndipo kuna Taasisi ya kitaifa ya utafiti wa mifugo, Kituo cha Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo na Chuo cha Mifugo? Machinjio hiyo itasaidia sana wanachuo wa *LITI,* Mpwapwa kufanya *field practical* hasa kwa somo la *Meat Inspection* kivitendo. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachoomba au ninachoomba mimi binafsi kwa niaba ya wenzangu wa Mkoa wa Pwani, wale ng'ombe wa hukohuko waliokuwepo wafundishwe kwa sababu ng'ombe mmoja wataalam wanasema anachukua hekta tano, sasa tuchukue mtu ana ng'ombe kama Wasukuma watoto wangu mmoja anakuwa na ng'ombe si chini ya 7000 wao wanachukulia sifa siyo kwamba wanataka wapate ng'ombe bora wao ilimradi ana ng'ombe wengi hajali. Wafundishwe njia bora za ufugaji yaani njia za kisasa za ufugaji ili tuweze kunusuru maeneo mengine yasiwe majangwa kusiwe na matatizo na kusiwe malumbano kati ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, nafikiri ujumbe umefika naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuleta Muswada huu Bungeni. Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa katika nchi yetu kuna mifugo mingi zaidi ya ng'ombe milioni kumi na nane na mifugo hii inachangia pato la Taifa kidogo sana, je, Serikali imeweka mikakati gani ya kuboresha hali ya ufugaji ili kupata mifugo bora

itakayochangia pato la Taifa vizuri zaidi kuliko hali ilivyo sasa, kwa kuboresha huduma ya mifugo, maji madawa, tiba, kinga na malisho bora?

Kwa kuwa Mkoa wa Dodoma una ng'ombe zaidi ya 1,600,000 na mifugo hawa wanaweza kuwakomboa wananchi wa Mkoa wa Dodoma kuondokana na umaskini, je, Serikali ina mpango gani wa kujenga kiwanda cha kusindika nyama hapa Dodoma ili wafugaji wapate soko la kuuza mifugo yao na kuboresha maisha yao?

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga machinjio ya kisasa Wilayani Mpwapwa kwa kuwa kuna ng'ombe zaidi ya 400,000 na Mpwapwa ndipo kuna Taasisi ya kitaifa ya utafiti wa mifugo, Kituo cha Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo na Chuo cha Mifugo? Machinjio hiyo itasaidia sana wanachuo wa *LITI,* Mpwapwa kufanya *field practical* hasa kwa somo la *Meat Inspection* kivitendo. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachoomba au ninachoomba mimi binafsi kwa niaba ya wenzangu wa Mkoa wa Pwani, wale ng'ombe wa hukohuko waliokuwepo wafundishwe kwa sababu ng'ombe mmoja wataalam wanasema anachukua hekta tano, sasa tuchukue mtu ana ng'ombe kama Wasukuma watoto wangu mmoja anakuwa na ng'ombe si chini ya 7000 wao wanachukulia sifa siyo kwamba wanataka wapate ng'ombe bora wao ilimradi ana ng'ombe wengi hajali. Wafundishwe njia bora za ufugaji yaani njia za kisasa za ufugaji ili tuweze kunusuru maeneo mengine yasiwe majangwa kusiwe na matatizo na kusiwe malumbano kati ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, nafikiri ujumbe umefika naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara ya Mheshimiwa Waziri mwenyewe kwa kuleta Muswada huu ingawa umechelewa sana. Naunga mkono Muswada, hata hivyo nachangia kama ifuatavyo, suala la dawa za mifugo bado linawakatisha tamaa wafugaji, kwani ni ghali sana na inaathiri uwezo wao wa kufuga. Suala la ruzuku kwa madawa ya mifugo ni kitendawili, halieleweki na hivyo inatosha kusema wafugaji wanaona wakulima wamepewa ruzuku lakini wakulima hawafaidiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema Muswada huu unaitwa Muswada wa Nyama wa mwaka 2006, una maana pana na swali linakuja ni nyama ya nini? Serikali inasemaje kuhusu nyama ya kuku? Muswada huu unahusisha vipi nyama ya kuku? Wafugaji wengi wa ng'ombe wanafuga pia kuku. Maeneo mengi ya Mijini ambako kwa asili sio wafugaji kama Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Moshi na kadhalika, wanafuga sana kuku. Je, hawa wanasaidiwa vipi Muswada huu ukipitishwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Singida ni maarufu kwa ufugaji wa kuku, hivyo na sisi tunahitaji Serikali iweke utaratibu mzuri kuhusu soko la kuku au Serikali ilete Muswada wa nyama ya kuku. Katika kifungu Na. 9 na kifungu cha nne, *composition* ya *Council* na *Board* hawahusishi kabisa Wabunge ambao ndio wawakilishi wa wananchi. Wabunge

ni muhimu kuleta *check and balance* na usimamizi wa karibu kwa niaba ya wananchi. Naunga mkono Muswada huu.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika Muswada huu wa Sheria ya Nyama wa mwaka 2006. Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Anthony Diallo kuwa Waziri wa maendeleo ya Mifugo na Naibu wake pia, Bodi ya Wizara na watumishi wote wa Wizara, nawapongeza kwa kazi nzuri wanayoifanya katika maendeleo ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ni kuzuia kabisa uingizwaji wa nyama kutoka nje ya nchi ili tuweze kukuza masoko ya ndani ya nyama na kuongeza ajira kwa watu wetu. Bodi ya Nyama isimamie sana juu ya usafi wa nyama na ukaguzi wa mara kwa mara wa nyama. Pia, kwenye Jimbo langu la Njombe Magharibi kuna mifugo mingi na kuna minada ya Wanging'ombe na Saja, naomba iimarishwe kwa kutengewa fedha za kutosha kwa ujenzi wa Minada hiyo ya kisasa ya Saja na Wanging'ombe. Mwisho, nawatakia kazi njema.

**MHE. VUAI ABDALLA KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali ya Awamu ya Nne chini ya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete. Pia naipongeza Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Waziri na Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni wakati mzuri na muafaka kwa marekebisho ya Sheria ya Nyama. Basi katika kifungu cha 13 Bodi ndio yenye uwezo. Kwa hiyo, naiomba Serikali kutoa uwezo kwa Bodi na Bodi iweze kutekeleza na kusimamia vyema. Baraza la mwaka, hatua ziwe za uhakika wa vikao na mazungumzo kwa ajili ya Serikali ya Tanzania. Maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji wa mifugo kwa ajili ya nyama, naomba Serikali iwape uwezo wa hali zote ili tupate nyama bora kwa mahitaji ya Watanzania wenyewe kwa afya zao na hata kupata fedha za ndani na za kigeni. Naomba Serikali ipate masoko bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Magogoni, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. JOB Y. NDUGAI - MWENYEKITI:** Ahsante tunakushukuru sana Mheshimiwa Zaynab Vulu, msemaji wetu wa mwisho mchana wa leo, ujumbe umewafikia Wasukuma.

Napenda kukumbusha tu zile Kamati ambazo zilikuwa zikutane saa 7.00 mchana Miundombinu, Maliasili na nyingine waendelee na ratiba hiyo. Pia napenda kuwakumbusha Wenyeviti wa Kamati mbalimbali za Bunge kwamba wanatakiwa wafike kwa kikao kifupi pale kwenye ukumbi wa Mheshimiwa Spika.

Kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge wote walioomba kusema wamepata fursa hiyo na wamekwisha hatuna ombi hata moja kwa hiyo maana yake ni kwamba jioni tutatoa fursa moja kwa moja kwa Mheshimiwa Naibu Waziri na Waziri mwenyewe waanze kupitia hoja hizi na tutaendelea na utaratibu kama utavyotakiwa kwa jioni ya leo.

Baada ya kusema hayo, naomba kusema kwamba sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni ya leo.

*(Saa 6.45 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii iliyo mbele yetu ambapo nitazungumzia hoja za Waheshimiwa Wabunge. Nianze mchango wangu kwa kutamka kwamba naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaingia kwenye maelezo ya hoja, kwanza naomba nitoe pongezi zangu nyingi kwa Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri walioteuliwa na Mheshimiwa Rais katika nafasi mbalimbali kwenye mabadiliko ya Baraza la Mawaziri yaliyofanyika mwezi Oktoba, 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nitoe maelezo ya hoja za baadhi ya Waheshimiwa Wabunge zilizojitokeza katika kujadili Muswada wa Sheria ya Wanyama wa Mwaka 2006 uliowasilishwa leo asubuhi. Mpangilio wa maelezo wa hoja za Wabunge ni kwamba, kutakuwa na hoja na Waheshimiwa Wabunge waliochangia na maelezo ya hoja yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja ya kifungu cha tisa cha Muswada inayopendekezwa kwamba Chama cha Wataalamu wa Mifugo waongezwe *(TVA),* yaani *Tanzania Veterinary Association*. Pia kifungu cha 13 cha Muswada kinaipa Bodi kazi za kiutendaji na kwamba inashauri kijiandae kwenye utendaji. Pia kifungu cha 4 cha Muswada hoja ilikuwa ni kuhusu uanzishwaji wa Baraza Kuu la Wadau katika sekta ndogo ya nyama. Neno "*Annual Stakeholders Meat Council"* liongezwe.

Pia, kulikuwa na hoja ya kifungu cha 30 cha Muswada. Inashauriwa taarifa ya Mkaguzi wa Mahesabu isipelekwe kwenye Baraza, bali ijitosheleze kama ilivyo. Pia, uandikishwaji *Registration* kwenye kifungu cha 20 isiwe ya mwaka mmoja, bali iwe ni ya kudumu, *Permanent Registration*. Pia, kulikuwa na hoja ya kifungu cha 25 za kazi za mfuko *(Functions of the Fund)* zijumuishe uendelezaji wa huduma za ugani na uendelezaji nyanja za malisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hizi zilichangiwa na Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli. Maelezo ni kwamba *Tanzania Petroleum Association* ni Taasisi isiyo ya Kiserikali, hivyo kifungu cha 5(i) ya kifungu cha Muswada kinachotamka *Two Members from Non- Governmental Organizations active in the meat*

*industry development* kinajibu hoja hiyo. Pia, watumishi wanaozungumzwa ni wale wa *Staff of Board.* Hivyo ni busara wakaajiriwa na Bodi yenyewe baada ya kuidhinishwa na Baraza. Ushauri kuhusu kifungu cha nne umezingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hoja katika kifungu cha 30 ni kwamba, kifungu hiki kinatamka taarifa pamoja na maoni ya Mkaguzi wa Mahesabu yapelekwe kwenye Baraza ndani ya miezi mitatu na Mwenyekiti baada ya kupokea. Hii ni kwa ajili ya Baraza kutoa uamuzi juu ya taarifa na maoni yaliyotolewa na Mkaguzi wa Mahesabu na sio vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *Permanent Registration,* ushauri umezingatiwa. Kuhusu kifungu cha 25 kama walivyoshauri Mheshimiwa Shellukindo pia ushauri huu umezingatiwa. Kulikuwa na hoja ya je maziwa na ngozi zinatambuliwa na Sheria ya Nyama? Hoja hii ilitoka kwa Mheshimiwa Kaboyonga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ndogo ya Maziwa inasimamiwa na Sheria ya Maziwa, *The Dairy Industry Act* ya Mwaka 2004. Pia, Sekta ndogo ya Ngozi inasimamiwa na Sheria ya *Hides and Skins Trade Act*. Hivyo, Sheria za Nyama kwa sheria hizi za Maziwa na Ngozi haihusiki hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha Mheshimiwa Kaboyonga alizungumzia suala la Machinjio ya Tabora kuwa hayaridhishi. Maelezo ni kuwa, Wizara itashauriana na Halmashauri ya Tabora ili kushughulikia suala hili. Ni azma ya Serikali kuwa na machinjio ndogo ndogo za Mikoani lakini ziwe za kisasa ili nyama inayotoka pale iwe inayokubalika kwa mujibu wa sheria ambayo Muswada wake ndio tunao mbele yetu hapa.

Pia, Mheshimiwa Kaboyonga alikuwa na hoja ya biashara ya wanyama hai haizingatiwi hasa kwa mbuzi, kondoo hasa kwa soko la Uarabuni ambalo mahitaji yake ni mbuzi, kondoo takribani milioni tatu mpaka tano kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa biashara ya kuuza mbuzi na kondoo imeanza na kiasi cha mbuzi au kondoo takribani 350 huchinjwa hapa nchini na kuuzwa Uarabuni kila wiki na nyama hii hupelekwa nchi za Kuwait, Oman na *United Arab Emirates*. Kwa sasa hivi hatujaanza kuuza wanyama hai kwenye nchi hizo. Juhudi za kuanzisha masoko ya wanyama hai zinaendelea. Mbuzi na kondoo wanaotakiwa lazima wawe chini ya miaka miwili na wawe na uzito wa nyama wa kilo takribani nane mpaka 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Kaboyonga nyingine ilikuwa, ni kwa nini maziwa hayakuzungumzwa katika Sheria ya Nyama? Maelezo ni kuwa, Sheria ya Nyama haikuingizwa katika Sheria ya Maziwa kwa sababu tayari kuna sheria inayosimamia zao hili la mifugo ambalo nilitaja, ni Sheria ya *Diary Industry* ya Mwaka 2004.

Kulikuwa na hoja kutoka kwa Mheshimiwa Kaboyonga kwamba kwa nini Bodi inashughulikia *Registratio*n za Machinjio peke yake? Maelezo ni kuwa, mbali ya

kuweka *register* kubwa ya machinjio, pia viwango *standards* zitawekwa na ukaguzi utafanyika pia. Usajili utafanyika kwanza na baadaye kufuatiwa na huduma nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja kutoka kwa Mheshimiwa Mntangi ambaye ilikuwa ni kuhusu suala la migogoro ya ufugaji na wakulima na watumiaji wengine wa ardhi kwamba itatatuliwaje migogoro hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999 inasimamia utengaji wa maeneo katika ardhi za Vijiji. Wizara ya Maendeleo ya Mifugo inatoa ushauri wa kitaalamu kwenye Halmashauri za Wilaya na Vijiji kuhusu maeneo yanayofaa kwa ufugaji.

Mheshimiwa John Cheyo, Mbunge wa Bariadi Mkoani Shinyanga alikuwa na hoja kwenye kifungu cha 17 cha Muswada kwamba kinamkataza kila mfugaji asiye na hati ya kuandikishwa kufanya biashara yoyote ya mifugo. Maelezo ni kuwa, hoja hii inajibiwa na kifungu kidogo cha pili kinachosema kuwa sheria hii haitawahusu wale wasiojihusisha na biashara ya nyama au walaji wa kawaida ambao hapa ninanukuu kwa Kiingereza lakini, *"Without prejudice to sub section one of this Act, shall not apply to meat and meat products not intended for sale and those produced consumption of the producer, members of the family or his employees."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa pia na hoja ya Mheshimiwa Mzindakaya ambaye kwanza nimpongeze sana kwa kupigania sana suala hili la sekta la wanyama. Hoja ilikuwa ni kuwepo kwa machinjio bora kwa ajili ya soko la ndani na nje na kwamba Serikali idhibiti ubora wa machinjio katika soko la ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inatoa miongozo ya kanuni juu ya ujenzi na uendeshaji wa machinjio chini ya kifungu cha 53 cha Sheria Na. 17 ya Magonjwa ya Wanyama ya Mwaka 2003 (*The Veterinary Act of 2003)*. Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri na *Tanzania Food and Drugs Authority,* zina jukumu la kusimamia utekelezaji wa kanuni hizi ili kuhakikisha ubora wa machinjio unazingatiwa. Aidha, awamu ya kwanza Mikoa 11 itahusika ambayo ni Arusha, Kilimanjaro, nadhani hili nimechanganya na kitu kingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kulikuwa na hoja kutoka kwa Mheshimiwa Mzindakaya kuwa hivi ni kweli majosho 592 yataogesha ng'ombe takriban milioni 17?

Mheshimiwa Mwenyekiti, majosho yanayohitajika kwa ng'ombe milioni 18 na nusu, tuliyonayo ni majosho 3,700 na majosho yaliyopo kwa sasa ni 2,141. Kwa hiyo, kuna upungufu wa majosho 1,559. Kati ya majosho 2,141 yaliyopo, majosho 1,148 yanaweza kufanya kazi kwa sehemu kubwa. Tatizo linaweza likawa hakuna maji au madawa. Majosho 592 niliyoongelea asubuhi yalikarabatiwa kwa kipindi nilichokitaja asubuhi cha 2003/2004, 2005/2006 na hivyo yako ndani ya majosho yaliyoko 2,141 hapa nchini.

Pia kulikuwa na hoja ya Mheshimiwa Mzindakaya kuwepo na *link* kati ya mfugaji, mnenepeshaji wa viwanda vya nyama. Mfugaji anapaswa kuwa na mifugo iliyo bora kwa ajili ya kumwuzia mfanyabiashara aliyenenepesha mifugo ili auze kwenye Kiwanda cha Kusindika nyama. Mfugaji anatakiwa kuwa na makubaliano na mnenepeshaji katika shughuli hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa na hoja ya Mheshimiwa Yono Kevela kwamba kuzuia kabisa uingizwaji wa nyama kutoka nje ya nchi ili tuweze kukuza masoko ya ndani ya nyama na kuongeza ajira kwa vijana wetu kwamba tuzuie kabisa uingizaji wa nyama kutoka nchi za nje. Pamoja na nia njema ya kukuza soko la ndani na kuongeza ajira, Serikali inazingatia mahitaji halisi ya nyama na uwezo wa viwanda tulivyonavyo kabla ya kuzuia uingizwaji wa nyama. Lengo la Serikali ni kuimarisha viwanda vya nyama ili viweze kuzalisha nyama itakayoweza kuhimili ushindani kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwe Mwenyekiti, aidha, Mheshimiwa Kevela alizungumzia kwamba Serikali itenge fedha za kutosha kwa ujenzi wa Minada ya Wanging'ombe na Saja. Kwa sasa Serikali ipo kwenye programu ya kuimarisha Minada ya Mifugo katika maeneo ya Kusini mwa Reli ya Kati zikiwemo Minada ya Saja na Wanging'ombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Luhaula, Mbunge wa Bukombe Mkoa wa Shinyanga pia alichangia kwa kuomba maeneo kutengwa ya wafugaji na kwamba alipendekeza pia sehemu za hifadhi zimegwe kwa ajili ya ufugaji. Kwamba maeneo ya ufugaji nadhani linaendelea lakini sinalo tena hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ni kuwa, kazi za kutenga maeneo ni ya Halmashauri kama nilivyosema. Kwamba Wizara ya Maendeleo ya Mifugo inatoa ushauri wa kitaalamu kuhusu kufaa kwa maeneo yanayopendekezwa kwa ajili ya malisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia inatoa mwongozo wa kuhamasisha Halmashauri kuibua miradi inayohusisha miundombinu ya ufugaji bora na majosho, malambo na vituo vya huduma. Nilisema awali kuwa nitachangia maelezo ya baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge na hivyo baada ya kusema hayo, kwa mara nyingine tena naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikushukuru tena kwa kunipa fursa hii ili niweze kujibu hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa kuchangia hoja ya Muswada Ulio mbele yetu leo asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijafanya hivyo, napenda kuwatambua wafuatao ambao walitoa michango yao kwa kuzungumza hapa kwenye Ukumbi, nikianzia na Mheshimiwa Maida Hamid Abdallah kwa niaba ya Kamati, Mheshimiwa Mwadini Jecha kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa John Cheyo,

Mheshimiwa James Mntangi, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Joyce Machimu, Mheshimiwa Emmanuel Luhaula na Mheshimiwa Zainab Vulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafuatao walitoa mchango wao kwa maandishi. Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mheshimiwa Joyce Machimu pia alichangia kwa maandishi, Mheshimiwa Vuai Abdallah na Mheshimiwa Yono Kevela. Napenda niwashukuru sana kwa michango yao ambayo imetuwezesha kwanza kupitia kwao, wananchi kusikia hoja iliyo mbele yao ambayo inawahusu moja kwa moja. Lakini pia imetusaidia sana na itatusaidia sana sisi wakati wa kutengeneza kanuni za utekelezaji wa sheria hii tuweze kuzingatia kama Mheshimiwa Naibu Waziri alivyokuwa anasema kwamba maelezo na maoni ambayo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wameyatoa tutayazingatia wakati wa kutengeneza kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza michango mingi iliyotolewa asubuhi majibu yake yameshatolewa, lakini nitapenda nipitie machache, baadhi na mengine kwa udhibitisho tutawaletea Waheshimiwa Wabunge kwa maandishi licha ya kutoa maelezo ya michango yao hapa.

Kwanza napenda kuishukuru sana Kamati ya Kilimo na Ardhi kwa kuliona kwanza, kwamba Serikali za Mitaa zinahusika moja kwa moja katika usimamizi wa sekta hii ndogo ya nyama na kwamba kuna umuhimu wa Serikali za Mitaa kupitia Mabaraza ya Halmashauri kuona kwamba miradi ambayo inahusu mifugo na sekta ndogo ya nyama inazingatiwa katika mipango yao ya kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kupitia Bunge lako Tukufu napenda kusisitiza kwamba kama Kamati ilivyozungumza, kuna umuhimu wa pekee kwa Halmashauri zetu zikishirikiana na Wilaya kutenga maeneo ambayo yameainishwa katika Sheria ya Ardhi ili kupunguza migogoro ya wafugaji na wakulima. Napenda pia kumshukuru Msemaji wa Upande wa Upinzani kwanza kwa kuunga mkono hoja ya Muswada ulio mbele yetu na pili kwa kusisitiza kwamba huu Muswada utahalalisha ile dhana nzima ya *Private Sector* kuhusika katika biashara ya nyama na pia katika kuchangia kwenye pato letu la Taifa.

Mheshimiwa Shellukindo amezungumzia vifungu kwa sababu alijikita zaidi kwenye vifungu vya sheria na ufafanuzi umetolewa ambao unazingatia maeneo karibu yote aliyoyasema. Ila moja ambalo ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Shellukindo ni kwamba Muswada ulio mbele yetu ni Muswada wa Nyama. Kwa hiyo, tafsiri yote iliyotolewa pale itahusu huu Muswada ambao uko mbele yetu. Kwa hiyo, hatukuona tena umuhimu wa kila sehemu tusisitize kwamba hii itahusu nyama kwa sababu Muswada wenyewe na kulingana na ushauri tuliopewa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu inatosha kukidhi umuhimu wa kuona kwamba *document* hiyo au sheria nzima na tafsiri zake kama zilizotolewa nchini ya tafsiri inakidhi Muswada na utekelezwaji wa Muswada huo. Lakini napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Shellukindo kwa kuonyesha *concern* kwenye maeneo ambayo nadhani ilikuwa sio peke yake inawezekana kulikuwa na

Waheshimiwa Wabunge wengine hawakupata ufafanuzi wakati nikiwasilisha Muswada huo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir nadhani amezungumzia sana umuhimu wa kujali baadhi ya kanuni zetu za dini katika shughuli nzima ya kuchinja mifugo.

Lakini napenda nimhakikishie Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir kwamba suala la namna gani ng'ombe au mbuzi atachinjwa, ukiacha tu kwamba mila na desturi zetu, baadhi yetu kidini inataka aina fulani ya utaratibu kufuatwa lakini pia ni lazima ieleweke pia kwamba hao wanaohusika kwenye ununuzi wa nyama moja kwa moja wanatengeneza kundi la watu wengi ambao wanahitaji kununua hiyo nyama.

Kwa hiyo, muuzaji nyama yeyote ni lazima atazingatia kitu ambacho ni desturi na mila na matakwa ya wanunuzi wa nyama hiyo. Kwa hiyo, hatuhitaji kuweka kwenye sheria kwa sababu tunafahamu Serikali yetu haina dini na hatuwezi kuanza kuingiza vifungu vya kutamka mahitajio ya dini moja au dhehebu moja ndani ya sheria tunakiuka Katiba ambayo inatukataza Serikali isijihusishe na uhuru wa dini ni wa kila mtu sio wa Serikali.

Mheshimiwa Lekule Laizer, nampongeza sana kwa kutoa mfano kwamba Longido wamefikisha mifugo yao kwenye kiwango ambacho kinahitajika kwenye soko la Kimataifa. Lakini pia katika kutatua tatizo ambalo analizungumza nimelisikia hili tatizo mara nyingi kwenye Mikutano yetu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwamba wafugaji wetu au wafanyabiashara wa mifugo wanahangaishwa sana wanapokuwa upande wa Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kupitia Mheshimiwa Mbunge, ningewashauri kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Longido ambayo sasa hivi ni Wilaya mngeweza kutenga eneo karibu na mpaka ukawa na Mnada ambao mtawahitaji wale wanaotafuta nyama upande wa Kenya wakaja kununua kwenye huo Mnada ambao ni wa Halmashauri au unaosimamiwa na Halmashauri. Itapunguza sana kwa sababu tunapojipeleka sisi wenyewe kupeleka mifugo upande wa pili kwa kweli inabidi kwanza tufuate sheria za kule. Lakini pia kuna uwezekano wa wao kutunga masharti au zile Halmashauri au Serikali za Wilaya upande wa pili kutunga masharti ambayo kwa kweli kwa kiwango fulani yanaweza kuwa yanatudhalilisha.

Kwa hiyo, dawa yake kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, sisi ndio tulio na mifugo mingi, sisi ndio tunaouza hii mifugo, sioni kwa nini Halmashauri ya Wilaya ya Longido msitenge eneo karibu na mpaka likawa soko la mifugo na mnaruhusu watu waje kutoka upande wa pili. Ninavyofahamu, eneo lipo lakini huo Mnada hauko kama ilivyotarajiwa.

Kwa hiyo, ni kiasi cha Wilaya kusisitiza kwamba eneo hilo kwa kutumia sheria ndogo ndogo linaweza kutumika vizuri zaidi na watu wakawa wanakuja hata kama mkiwaambia wewe ukija huku tunataka utulipe kwa dola, watalipa kwa dola. Tunataka

uje ulipe kwa fedha za Kitanzania watalipa kwa fedha za Kitanzania. Au ukiwaambia walipe kwa fedha za Kenya wanaweza kulipa fedha za Kenya kuliko ilivyo hivi sasa tunajipeleka wenyewe kwenye mdomo wa simba halafu inakuwa matatizo.

Pia, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, suala aliloliuliza la baadhi ya ranchi zetu tutahakikisha kwamba watakaopewa maeneo hayo ni wale tu ambao wataendeleza sekta hiyo ya ufugaji, kwa vile hatujatamka kwamba ni lazima tutawapa wageni, kwa hiyo tunakaribisha watakapokuwa wanatangaza maeneo hayo, wananchi nao wahusike na hilo tumeliona.

Mfano mzuri ni kwa Mheshimiwa Shellukindo, walipotangaza kuuza Kiwanda cha Chai, wakajitokeza wananchi wa Jimbo lake la Bumbuli wengi wao wakanunua Kiwanda cha Chai na Serikali ilikubali na ikawauzia. Kwa hiyo, tusije katika kuamini kwamba Serikali muda wote inauza maeneo au ranchi zake kwa wawekezaji wa nje.

Lakini mfano mzuri pia ni maeneo ambayo yalitengwa kando kando ya ranchi, baada ya kutenga maeneo kwa ajili ya watu wa kunenepesha wenye ranchi wa kuweka ranchi ndogo. Nayo maeneo karibu yote tuliyagawia kwa Watanzania ambao ni hao hao Mheshimiwa Lekule Laizer anawazungumzia.

Mheshimiwa Cheyo amezungumzia mambo muhimu manne. Moja, ni ile kuonyesha wasiwasi wake kwamba Serikali inakuwa kama iko kwenye matatizo na wafugaji. Lakini hili nataka nimhakikishie Mheshimiwa Cheyo kwamba Serikali haiko kwenye ugomvi wowote na wafugaji.

La pili, Muswada huu unalenga pia kuonyesha kwamba Serikali inajali mazao na bidhaa zote ambazo wafugaji wanahusika moja kwa moja katika uzalishwaji wake na hilo linaelekezwa vizuri hata kwenye Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi kwamba Serikali inatambua umuhimu wa wafugaji na umuhimu huo nadhani mnafahamu kwamba wafugaji ni kati ya wananchi ambao katika nchi hii wanajihusisha kwenye shughuli za uchumi.

Mheshmiwa Mwenyekiti, tukifikiria kwamba nyama ambayo tunaila sisi kila siku, majumbani kwetu, leo tusingekuwa na mifugo na kutokuwatambua wafugaji, nyama hiyo ingekuwa inaagizwa kutoka nje kama wanavyofanya Kongo. Mamilioni mangapi ya Dola leo yangetumika? Utaona kabisa kwamba mazao ya mifugo, ukweli ni kwamba kwa kiwango kikubwa, yanaokoa fedha nyingi sana za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya, baada ya *LIDA* kuvunjwa, umuhimu wa kusukuma kwa nguvu zaidi mazao yatokanayo na mifugo ulipungua kidogo. Lakini, sasa nataka kumhakikishia Mheshimiwa John M. Cheyo, kuwepo mimi kwenye hiyo Wizara, maana yake ni kusisitiza hilo kwamba Serikali inaona umuhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nimhakikishie pia kwamba Kiwanda cha Shinyanga kitakapoanza uzalishaji, nina hakika kinaanza uzalishaji katika kipindi kifupi kijacho. Sasa wale watu ambao Mheshimiwa Emmanuel J. Luhahula amewazungumza,

wanaonenepesha mifugo. Kwa bahati nzuri Watanzania wako *pro-active*, yaani wanaanza kitu na kukielewa haraka haraka.

Mwanza, eneo la Igoma amelitamka, wameishaanza unenepeshaji. Ng'ombe wote wanaopita hapa nawaona kwenye magari sasa hivi baada ya kuteremshwa kwenye treni hapa, wengi wametoka sehemu ya Kahama na wengi wametoka maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja. Sasa, eneo hilo, *catchment area* ya Kiwanda cha Shinyanga ambacho kinatarajiwa kuanza kwa kuchinja ng'ombe 180,000, mwaka wa kwanza na wataongeza idadi hadi kufikia karibu nusu milioni kwa mwaka. Itakuwa na eneo kubwa sana la *catchment* ikiwemo Bariadi na sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vyema kama tulivyowaomba wawekezaji wote ambao wameonyesha nia ya kukinunua hicho Kiwanda, *extension service* au Ugani, itawabidi kuanzisha maeneo pamoja na eneo ulilolisema la Mwabuki, litakuwa ni eneo la kufundishia wafugaji jinsi ya kulisha mifugo ili wafikie uzito na hali bora ambayo inatakiwa na hivi viwanda. Kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Mbunge akirudi kwenye eneo lake ahamasishe na ninajua eneo lake na maeneo mengine ya sehemu hizo za Shinyanga na Mwanza ni ya watu wachapakazi ambao wanaweza kufanya hiyo kazi kwa mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kama alivyosema Mheshimiwa John M. Cheyo na Kamati ilivyotushauri, kazi ya Malambo tulianza kwenye Bajeti ya 2004/2005. Kuna fedha nyingi sana zilitolewa kuchimba malambo, mengi yamechimbwa. Lakini, tatizo linalotusumbua sana, usimamizi kwenye Halmashauri zetu. Unakuta *standard* ya malambo yanatofautiana Wilaya hadi Wilaya. Lakini Wilaya ambazo zimefanya kazi vizuri, malambo ni mazuri na yanakidhi. Kwa kuzingatia hilo, napenda pia kugusia suala ambalo Mheshimiwa Zaynab M. Vulu alilizungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malambo ya maji ya ng'ombe au ya wafugaji yanayochimbwa, yanakidhi matumizi aina mbili:- Moja, wanatengeneza *trough* kwa ajili ya mifugo, kunyweshea ng'ombe upande mmoja. Lakini pia wanatengeneza *oftake* ya bomba kwa ajili ya maji ya kunywa. Kwa hiyo, kwa kuzingatia hilo, nawahakikishieni wenzangu, watani zangu wa Mkoa wa Pwani, wasiwe na wasiwasi wowote. Ng'ombe wakiingia Pwani, wakiingia na hivi vitu ambavyo tunavizungumza hapa yaani kama malambo, majosho na kadhalika, moja kwa moja itafaidisha Wilaya zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani matatizo ambayo alikuwa nayo Mheshimiwa Herbert J. Mntangi kwenye Muswada, yamejibiwa vizuri ikiwemo hilo la kutambua kwamba kuna Sheria ya Maziwa ambayo tuliitunga hapa Dodoma kwenye Bunge letu Tukufu ya mwaka 2004 na Sheria ya Ngozi imekuwepo kwa kipindi kirefu kilichopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya wafugaji, nakubaliana na Mheshimiwa Herbert J. Mntangi kwamba kwa kiwango kikubwa, migogoro inakuwepo wakati mfugaji asipomjali mkulima na mkulima asipomjali mfugaji. Kwa hiyo, kutakuwa na mgogoro tu. Lakini kwa bahati nzuri baadhi ya wafugaji wanafanya vyote viwili; wanafuga na wakati huo huo wanalima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara ya kwanza mimi nilipokwenda Mkoa wa Rukwa, nilikwenda eneo fulani wanaita Chipeta. Chipeta kule, kuna wafugaji ambao wamebadilika kweli. Ni sehemu ambayo iko porini, lakini wafugaji wamepunguza mifugo yao au wamevuna mifugo yao na kuuza na kuanzisha biashara nyingine kama *Guest House* na sehemu nyingine wamenunua hata hisa kwenye Benki zetu kama *CRDB*. Kwa hiyo, mfugaji tusimwone kama adui. Mfugaji ni kama mfanyabiashara yeyote yule, ni kama mkulima. Tunapofikia mahali tunaanza kudharau wafugaji, pale ndipo tunakuta kwamba tunashindwa kuelewana na baadhi yao. Ni vizuri kuheshimiana, mfugaji atamheshimu mkulima, mkulima atamheshimu mfugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kuna wakati mwingine inatokea ng'ombe wanaingia kwenye shamba la mkulima, lakini hizo ni *incidences* za mara moja moja. Sasa huwezi uka-*generalise* ukaona kwamba ndio makosa ya wafugaji wote. Inatokea tu kwamba tatizo kama hilo linajitokeza na mara kwa mara sheria zipo za Halmashauri zetu. Sheria ndogo ndogo zimewekwa kwa ajili ya kulinda wakulima na wakati huo kuhakikisha kwamba kati ya wakulima na wafugaji wote wanafuata sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, soko la *Middle East* ni kubwa sana. Sasa hivi kuna mtu ambaye anaomba tani 150 kwa wiki. Kuna mtu ambaye anaomba mbuzi 700 kwa wiki. Lakini, matatizo siyo ya upatikanaji wa mbuzi au nyama, matatizo pia tunayo upande wa usafirishaji. Kupata ndege ya kupakia tani 150 kwa wiki kutoka Dar es Salaam au kutoka *KIA* kwenda Dubai, siyo rahisi.

Nafasi hiyo inagombewa na watu wenye maua, inagombewa na wenye matunda na kadhalika. Lakini nina hakika kwamba baada ya baadhi ya Viwanja vyetu vya ndege kupanuliwa, mfano kiwanja cha Mwanza kikiwekwa kwenye hali ambayo ndege kubwa zitakuwa zinatua, usafirishaji wa nyama utakuwa rahisi zaidi na wa mazao mengine kama samaki na kadhalika.

Tumemwelewa Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya na napenda nichukue fursa hii kumpongeza sana. Ni katika wawekezaji wazalendo ambao wameamua kujiingiza moja kwa moja kwenye biashara hii ya nyama na kiwanda cha Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya nadhani baada ya muda mfupi kitaanza kazi na kina eneo kubwa sana ambalo watapata mifugo na itapunguza matatizo mengi sana. Lakini uzuri wake ni kwamba yeye yuko karibu na Zambia. Sasa tusipokimaliza kiwanja cha ndege cha Mbeya mapema iwezekanavyo, ina maana atakuja kupata matatizo tu ya usafirishaji kama wanavyopata matatizo hawa wenzetu wengine walioko maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nampongeza Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya na kama nilivyosema leo asubuhi, ninyi Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Viongozi wa Serikali wa ngazi mbalimbali, ndio wa kuonyesha mfano. Huo wivu aliokuwa anausema, mimi nina hakika ni mambo ya kizamani. Sasa hivi hakuna anayemwonea wivu mtu na hata akikuonea wivu, wewe *proceed*, *life goes on*.

Sidhani kwamba ndio binadamu anakufanya uishi. Maneno ya watu nadhani yasitukwaze sana. Yatakuwepo tu na yamekuwepo kabla hata ya Yesu Kristo kuzaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Joyce N. Machimu, ameniomba tutembelee maeneo hayo. Kwa bahati nzuri Mheshimiwa Joyce N. Machimu, maeneo hayo nayafahamu vizuri sana na ninawafahamu hata wanaohusika na biashara hiyo. Lakini, nikipata nafasi katika *position* hii niliyonayo, mimi au mwenzangu ambaye yuko karibu pia na maeneo hayo, tutatembelea ili kuona ni matatizo yapi ambayo yanawakwaza wenzetu wafugaji au wafanyabishara wanaojishughulisha na unenepeshaji wa mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Emmanuel J. Luhahula, amezungumza juu ya fidia ya ardhi sehemu ambazo watakwenda. Napenda kwa kweli kwa kiwango fulani nikubaliane naye. Suala la mifugo nchi hii siyo tatizo la nafasi. Wengi sana tunasikiliza maneno watu wanazungumza kwamba wafugaji wanahitaji maeneo. Lakini, sidhani kama ni maeneo kwa sababu hata tukiwapatia maeneo leo, tusipofanya utaratibu ambao ameuelezea Mheshimiwa mmoja hapa asubuhi wa *range management*, kwamba tukawa na maeneo na uwezekano wa kuvuna nyasi ili zitumike wakati wa kiangazi, hata ukipewa eneo kubwa nmna gani leo, hata tukikupa eneo la pori la akiba, nyasi zile utazimaliza na utarudi pale pale penye matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala siyo maeneo, suala ni kuwafundisha wafugaji wetu ufugaji bora ambao unahusisha uvunaji wa nyasi ili zitumike wakati ule wa kiangazi na pia kuwapatia huduma nyingine za ugani kama majosho na kadhalika. Kwa hiyo, sioni tatizo kwa sababu kimila hata kwetu kule watu wamekuwa na ngitili. Lakini, walikuwa wanafanya hiyo *rotation* kwamba kati ya mwezi wa tatu labda na wa sita, anakuwa eneo moja, mwezi huu anakuwa eneo lingine. Lakini hilo katika miaka ya karibuni tulilipuuza, nadhani ndio maana tumefika hapa tulipo na nina hakika sasa hivi kila mmoja wetu hapa nchini ameelewa umuhimu wa matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ruzuku ya dawa, nadhani hapa lilizungumzwa na Waheshimiwa Wabunge kwa sababu tuna uzoefu. Mwaka 2004 kulikuwa na fedha zilizotolewa kwa ajili ya ruzuku ya dawa. Lakini hatukuona matunda yake kwa mfugaji.

Sasa nakubaliana nanyi kwamba tutaangalia utaratibu bora ambao tutawatambua ni akina nani wanaoifanya hii shughuli kule kwenye Mikoa yetu na Wilaya zetu badala ya kumpa mtu mmoja Dar es salaam anachukua hiyo tenda halafu anaamua kufanya biashara kama kawaida na hachukulii maanani ni kwa sababu gani ruzuku hii imetolewa. Kwa hiyo, hilo napenda niwahakikishie kwamba tutajaribu kusimamia vyema safari hii ili tuone kwamba wafugaji na wale walengwa wamefaidika na ruzuku ambayo imetolewa na fedha za walipa kodi wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Zaynab M. Vulu nadhani ningeomba nirudie kumshauri kwamba waruhusu kiwango ambacho wamepangiwa kuchukua ng'ombe Mkoa wa Pwani na Wilaya ya Kisarawe.

Ninapozungumza hivi, kuna ng'ombe tayari, asije akasema kwamba hakuna ng'ombe, mimi nafahamu nimeshakwenda Kisarawe hivi karibuni. Kuna ng'ombe wako maeneo hayo tayari. Lakini ng'ombe ni uchumi, hili jambo tunajaribu kulisahau. Mheshimiwa mmoja hapa amezungumza, Shule za Msingi zimejengwa kwa mchango mkubwa sana wa wafugaji, Zahanati zinajengwa kwa mchango mkubwa sana wa wafugaji. Sasa, kwa wewe kama mwananchi wa kawaida unachojali ni nini? Ni huduma tu za jamii. Baada ya hapo, mambo mengine ni juu yako mwenyewe. Sasa, tunapowakataa wafugaji, ina maana unakataa uchumi. Serikali sidhani kwamba ina uwezo wa kumwezesha kila mmoja apate fedha kwa ajili ya ujenzi wa Zahanati, ujenzi wa shule na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningewaomba sana, bahati nzuri Waziri Mkuu aliteua Kamati hapa ambayo imepita imetoa mapendekezo yake karibu kila Wilaya wamepangiwa ili wapange sehemu za wafugaji na idadi ya mifugo wanayopangiwa kwenda kule. Sasa tusifike mahali tukakataa kwamba sisi hatutaki, hatutaki wenye mifugo! Ni kama hujui unachozungumza kwa sababu mifugo ni uchumi. Ila, nakubaliana na wale wanaosema kwamba tutachukua idadi ambayo ardhi iliyopo inatosha. Hapo inakubalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani mengi ya yaliyozungumzwa nimeyafafanua. Ila kuna kifungu kimoja ambacho Mheshimiwa John M. Cheyo alikizungumza; tafsiri hasa ya ni wakati gani ufugaji unakuwa wa kibiashara na wakati gani ufugaji wa kawaida, nadhani unakuwa wa kibiashara unapoamua *exchange,* yaani fedha na mifugo, yaani inakuwa biashara yako ni kununua na kuuza.

Tafsiri hiyo ndiyo ambayo tunaikubali kwenye sheria ya biashara na inakubalika kwenye sheria nyingine zozote hizo kwenye sekta nyingine kwamba unapoanza biashara ya kununua na kuuza, wewe ni mfanyabiashara. Lakini hii ya kutoa unaamua kuvuna mifugo yako, una ng'ombe 500, unaamua kuvuna ng'ombe 100 kwa kuwapeleka kwenye Mnada, sasa hiyo sheria au utaratibu huo umeelekezwa na Halmashauri husika, wana sheria zao ndogo ndogo. Kama ni maeneo wanatoza chochote, ni maamuzi ya Halmashauri ambazo ndio wanaosimamia biashara hizi ndogo ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini humo kwenye sheria, tumezungumza ufugaji ambao ni *Commercial*, ina maana ni wale ambao wanakata leseni, kwanza inabidi akate leseni ya kufanya biashara. Kwa hiyo, anakata leseni ya kutoka kwenye Halmashauri kule kama ni mfanyabiashara wa mifugo. Sasa wale itabidi sasa ndio waingie kwenye hii sheria kama wamesajiliwa kwenye shughuli hiyo. Hatuzungumzii hawa wadogo wadogo; hawa wadogo wadogo nadhani mtu ameamua kuvuna mifugo yake, nina hakika kwamba sheria kulingana na Halmashauri walivyojipangia na walivyoelekeza, zina-*take care of*, siyo sheria hii ambayo ni ya sekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa mchango wao mzuri. Nina hakika utatusaidia sana kwenye kutunga kanuni za utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki!

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa kwa Mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Nyama wa Mwaka 2006**
***(The Meat Industry Bill, 2006)***

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 3

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakupongeza kwa kukalia kiti na nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kutaka kupata maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi ambao nilimpelekea Mheshimiwa Waziri, nilieleza pamoja na mambo mengine, mambo mawili: Moja, suala la nyama ya kuku. Katika Kifungu Na. 3 ukisoma tafsiri ya *Livestock*, anasema: *"Livestock means*, *cattle*, *sheep*, *goat*, *poultry*, *rabbit or pig.*" Nadhani hapa *Poultry* na kuku anaingia hapa! Lakini hata ukija kwenye tafsiri ya *meat*, inasema: "Means *the whole or part of the dressed carcass of any slaughtered livestock*." Kwa hiyo, kwa maana ya tafsiri ya awali, basi na kuku anaingia kama nyama ya *livestock*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini, sioni kwingine kokote huku ambako suala la nyama ya kuku, suala la wafugaji wa kuku ambao kwa kweli nchini hapa limetapakaa sana. Tunafahamu katika Miji yetu mikubwa hii, Dar es salaama, Arusha, Moshi, Kilimanjaro wapi huko, wamejaa wafugaji wa kuku. Hawa nao wanatoa nyama na nyama yenyewe unajua ni adimu, nyama nzuri. Wataalam wanasema nyama ya kuku, nyama ya bata ni nyama tamu kuliko nyama nyingine zote. Lakini hawazungumzi popote hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile mimi kama Mbunge wa Singida, unafahamu wewe ni jirani yangu, kwamba Singida tunazalisha sana kuku na soko letu kubwa liko Dar es Salaam. Wewe mwenyewe na Waheshimiwa Wabunge hapa kila siku

mnasema mnataka nyama ya kuku wa asili na hao wanatoka Singida. Sasa katika Muswada huu ukiacha hii tafasiri hapa ambayo inamhusisha kuku, sioni mahali pengine ambapo suala la kuku linazungumzwa, soko lake, mfugaji wa kuku atahudumiwa namna gani kama ambavyo ilivyoelezwa katika baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningependa Mheshimiwa Waziri anifahamishe: Je, Muswada huu unamhusu vipi kuku na mfugaji mwenyewe wa kuku katika masoko na kadhalika. Kwa sababu kama tukitengeneza kuku vizuri sasa hivi, tungeweza hata kupata mwekezaji akawekeza kiwanda cha kuku kule Singida, tukawa tunapata nyama nzuri ya kuku kulikoni kuhangaika. Sasa hivi ukifika kwenye *bar* na hoteli, soko kubwa sasa hivi ni kuku wa asili kutoka Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningependa kupata maelezo. La kwanza, hapa ukiangalia kwenye ukurasa wa tano kwenye *composition* ya *Annual Council*, hakuna mahali popote pale ambapo panaonyeshwa suala la kuku au wafugaji wa kuku wanahusishwa. Ukiangalia ukurasa wa saba kwenye Bodi pale, hakuna mahali popote pale ambapo unaona mfugaji wa kuku au watu wanaohusika na biashara ya kuku wanahusishwa. Sasa, Je, kuku siyo nyama wakati tunajua nyama tamu ni kuku na bata? Hilo la kwanza. Lakini la pili…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed Missanga, tuelewane kuhusiana na hilo la kwanza. Fungu la tatu tulipo ni suala la *interpretation* kuhusiana na maneno ambayo yameorodheshwa pale. Sasa, *unless* ungekuwa na swali kuhusu *definition* fulani kwamba ina tatizo au nini, ndio tungeweza kulichukua. Halafu hizi kurasa unazokwenda, unakwenda mbele ya Kamati. Kamati haijafika huko.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa labda niseme kwamba hii *definition* iliyoko hapa niliyoeleza kwenye *livestock* na *meat*, huku mbele siioni. Mheshimiwa Waziri anieleze, kwa sababu unapoweka *definition* maana yake huku mbele ya Muswada lazima kuna mahali inatajwa, inaelezwa na kadhalika. Mheshimiwa Waziri anieleze sasa, Je, ukiacha *definition* hii hapa ambayo imeelezwa, huku mbele wapi kuku wanatajwa?

**MWENYEKITI:** Kabla sijamruhusu Mheshimiwa Waziri kujibu, nikumbushe tu kwamba kuna *schedule of amendment* ambayo neno *livestock* limeondolewa kutumika kwa sehemu kubwa. Lakini, nimruhusu mwenyewe Mheshimiwa Waziri, inawezekana amemwelewa zaidi Mheshimiwa Mohamed Missanga.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mohamed Missanga nadhani nimemuelewa. Huu Muswada ni wa nyama na nyama kwenye hicho kifungu anachokizungumza ina-*include poultry*. Sasa, ukishamaliza *poultry* hata kwenye vifungu anavyovieleza ambavyo bado hatujafikia, kuna kifungu ambacho tunazungumzia juu ya walaji wa nyama. Sasa walaji wa nyama kwa *definition* kama tumekubali kwamba nyama ya kuku imo, itakuwa ni moja kwa moja wanahusika.

Lakini, la pili, lazima tuelewe kwamba kuna sheria ya *Verternary Services* ambayo inazungumzia juu ya kuku kabla hujamchinja au ng'ombe akiwa bado hai. Sasa hiyo sheria ukitaka kuipata tafsiri vizuri zaidi, kuku anatunzwaje au anashughulikiwaje, ni kuangalia hiyo Sheria ya *Verternary Services Act* ambayo inahusu kuku na mifugo wakiwa bado wazima. Lakini naelewa sana *concern* ya Mheshimiwa Mbunge na niwapongeze sana, ni watoaji wa kuku wakubwa sana nadhani wanaotumia treni nchi nzima, wanawafahamu kuku wa Singida.

**MWENYEKITI:** Namwona Mheshimiwa Hafidh Ali, lakini hukusimama mwanzo. Nakupa *favour* ya Mwenyekiti.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee?

**MWENYEKITI:** Unaweza kuendelea!

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipendelea!

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nachangia Muswada huu, kwanza nilikuwa nachangia kwa hadhari sana kama Mheshimiwa Waziri sijui alinifahamu. Nilikuwa nachangia kwa hadhari kwa sababu maalum. Lakini pia nilikuwa nategemea, kwa hiyo, hadhari niliyokuwa naitoa katika mchango wangu na Mheshimiwa Waziri angekuja kunijibu kwa hadhari vile vile na katika mtiririko mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri alipokuwa akijibu, naona kanijibu kwa mkato, kitu ambacho bado kinanitia wasiwasi na naendelea kutoa mawazo yangu kwa hadhari tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingekuwa suala hili ni la mtu binafsi, hiyo nisingechangia. Lakini suala hili ni la Kitaifa, halafu utaifa zaidi uliopo hapa ni wa biashara ya Kitaifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hafidh Ali, tuko kwenye *interpretation* ukurasa wa nne pale. Ni orodha ya maneno na jinsi yalivyotafsiriwa kisheria. Kwa hiyo, kwa hatua hii ni kwa mtu ambaye anakwazwa na tafsiri fulani, ndiye anaweza kuchangia. Kwa hiyo, kama unataka kuendelea, basi utupeleke moja kwa moja ni tafsiri ya neno gani ambayo inakupa tatizo. Unaweza kuendelea!

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata wasiwasi kwa sababu huko mbele kila nikiangalia vifungu, hili ninalotaka kulizungumza silioni. Lakini kwenye kifungu hiki 3(e)(4), kinazungumzia suala la uchinjaji na ndio maana nikaona, basi nilizungumze hapa kwa sababu hapa ndio kwenye tafsiri ya uchinjaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama nimekosea, basi baadaye uje kunipa nafasi katika kifungu chochote pale nipate kuzungumza, vinginevyo unipe ruhusa niendelee hapa.

**MWENYEKITI:** Nakuruhusu uendelee hapa!

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya mchango wangu huo, Mheshimiwa Waziri nilikuwa nategemea ataelekeza zaidi katika suala zima la Kitaifa na hasa biashara ya Kitaifa. Lakini pia nilikuwa namtegemea vile vile angekuja hapa nyumbani kwa hao wawekezaji ambao tunataka tuwape nafasi ya kutuchinjia hao wanyama wetu ili sote tupate kuwatumia, tuwatumie nyumbani na vile vile tuwauze nje. Pia nikatoa mfano mie, wenzetu wengine huko nje wana namna kadhaa ya kuchinja wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mie vile vile nilisema hapa kwamba Tanzania haina dini, lakini Watanzania wana dini. Sasa hawa wawekezaji tunataka kuwapa nafasi hii ya kutuchinjia wanyama, basi angalau wangekuwa ama na kanuni au kungewekwa utaratibu mwingine kwa sababu kasema sasa hivi hakuna sheria na kweli nakubali, lakini nchi jirani zina sheria. Kwa mfano Uganda lazima uchinje kwa namna fulani. Lakini hata hapa Tanzania bado kuna watu hawapo katika hiyo, ambayo nimekwenda mie kwa maana ya Waislam wanawachinjia kwa maana ya kupata kitu halali. Au vinginevyo Mheshimiwa Waziri angetuambia, mtaona nyama imetundikwa katika mabucha haikuandikwa nyama halali msinunue. Sasa kidogo angenisaidia maelezo ambayo yangesaidia sana. Naomba nipate maelezo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nadhani ni jambo la kanuni zitakazotengezwa baadaye.

**WAZIRI WA MAENDELEO MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimwelewa Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir. Nimeeleza vizuri sana kwamba kuna baadhi ya vitu ambavyo tunavifanya kama mila/desturi. Mila zinaweza kuwa na misingi ya kidini, inaweza kuwa na misingi ya utamaduni ambao ni kawaida *(common practice).* Sasa nimemhakikishia na ninamhakikishia Mheshimiwa Hafidhi Ali Tahir, *butcher* zote na machinjio yote wanafuata taratibu ninazozieleza. Lakini hatuwezi kuziweka kwenye sheria kwa sababu Serikali haina dini ndiyo nilichoeleza. *(Makofi)*

Lakini *is a common practice* kwamba ng'ombe au mbuzi machinjio wanafuata mila ya watu ambao ni kati ya jamii ya Watanzania. Yote uliyoyaeleza yanafahamika na ndiyo maana hatuhitaji kuweka *label* ya huyu ng'ombe ni halali au ni vipi kwa sababu ni mila na tumezingatia hiyo kama utamaduni wetu. Kama watachinja mnyama mwingine ambaye ni tofauti kuna taratibu. Karibu kila Halmashauri wameweka utaratibu kwenye sheria zao ndogo ndogo, itabidi uonyeshe kama huyu atakuwa ni kitimoto ama huyu atakuwa ni nani.

Kwa hiyo, wanaeleza. Hutakiwi kuficha. Kwa hiyo, kwa upande wetu nina hakika kwamba nimekidhi kinachohitajika kwenye Muswada wenyewe. Lakini mambo mengine ya kidini hatuwezi kuyazingatia moja kwa moja kwenye Miswada kwa sababu Serikali haina dini na ndiyo nilivyoeleza na nimeeleza kwa lugha ambayo ningeweza kukueleza ukaelewa sehemu yoyote.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri naona ananizonga tena na sasa hivi kanizonga zaidi. Kanizonga zaidi kwa sababu kaling'ang'ania neno mila na nilikuwa nimeliacha pale mwanzo, lakini Mheshimiwa Waziri alisahau kwamba katika suala hili la kidini sio mila. *Quran* ndiyo ilivyosema. Sasa *Quran* ikisema sio mila. Mila ni kitu ambacho kimezoeleka kufanyika na wazee wa zamani ndio mila. *Quran* imesema mnapotaka kuchinja mchinje mwelekee Kibla na achinjwe katika desturi, imesema *Quran* sio mila.

Sasa ananipeleka kwenye mila wakati *Quran* ilishaandika ananihangaisha zaidi na aliposema kwamba Tanzania haina dini, mimi nakubali. Lakini Watanzania tuna dini. Sasa basi hajalifikiria hili akaona kwamba hapa hapana kitu ambacho kinaweza kutokea? Nilipokuwa nachangia asubuhi nimesema hivi kwa sababu tunataka kufanya biashara, basi tufanye jambo ambalo tutawakinga maadui wa Tanzania, ndio nilivyosema hivyo. Tufanye jambo ambalo linaweza kutusaidia kuwakinga maadui wa Tanzania ili biashara ya nyama isiharibike nje, kwa sababu asitoke mtu akasema kwamba nyama ya Tanzania kwa mfano nchi za Kiarabu tunataka kupeleka biashara na biashara tunafanya sana na akasema kwamba nyama ya Tanzania haichinjwi kihalali. Kwa hiyo, huko isije. Hatuoni kama tunapoteza biashara yetu? Ndio nilikokuwa nimeelekea mimi Mheshimiwa.

**MWENYEKITI:** Kwa maneno mafupi ili sote tukuelewe Mheshimiwa Hafidh nia yako ni kusema kwamba itungwe sheria kwamba mnyama yeyote atakayechinjwa Tanzania achinjwe kwa utaratibu wa Kiislam au unasemaje? Ili iwe rahisi Mheshimiwa Waziri, aweze kujibu kitu ambacho kinaeleweka moja kwa moja. Badala ya kuzunguka, jaribu kwenda moja kwa moja.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijasema hivyo, ukitaka kunipeleka huko ndiyo unataka kunifanya sasa Tanzania ina dini. Tanzania haina dini. Nilichotaka kusema, kuwekwe kanuni inayozungumzia masuala haya mawili, hiyo itatusaidia kwani ina ugumu gani? Kwa sababu kuna Watanzania wana dini! Tunachotaka kufanya hapa ni biashara ndani na nje ya Tanzania. Ninachoomba mimi, itungwe kanuni tu.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge ameeleweka, tunamshukuru. Tutakapofika kwenye kutunga kanuni, tutajaribu kuona kama inawezekana, kama tutakuwa hatuvunji masharti. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 4

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nimwelewe Naibu Waziri kwa sababu wakati Naibu Waziri alitoa maelezo kuhusu mchango wangu nilimwelewa na Waziri alipoamka alizungumza vinginevyo. Nilichosema mimi ni kwamba, ile *part two,* ile *caption* yake, *establishment of the Annual Council* nikasema ni vizuri angetumia maneno yaliyoko katika madhumuni ya Muswada

na sababu katika sehemu ya pili ambayo inasema kuanzishwa kwa Baraza la Mwaka la Wadau wa Sekta Ndogo ya Nyama ndiyo niliomba. Ingetokea hapa, basi itasaidia huko kwingine hata ukiandika *Annual Council* inajulikana, ni hii ambayo umeiweka hapa ambayo imetokana na madhumuni ya Muswada. Sasa ukisema hakuna marekebisho ni kwamba yanabaki jinsi yalivyokuwa na ule mchango hauna maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kusema kitu kimoja hapa, *bill* hii ni ya Serikali, ikishakuwa sheria ni Sheria ya Bunge. Kwa hiyo, ni vizuri tukaelewa wote ni kitu gani, maana tunakwenda kuitumia ikiwa Sheria ya Bunge, hatutasema ni Sheria ya Serikali wala Sheria ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninajaribu kumwelewa Mheshimiwa Mbunge. Muswada kama nilivyoeleza ni, *The Meat Industry Act.* Upande wa tafsiri ambacho ni kifungu cha tatu tumezungumza juu ya *Annual Council* inayomaanisha hapa. Inasema: *"Annual Council means a Council established under section four of this Act*." Sasa *of this Act; Act* gani? Ni ya nyama?

Hata hiyo *page* ya *part two section four* juu imeandikwa: *"Meat Industry*." Sasa mimi nadhani kuongeza maneno ni kwa sababu *Annual Council for Meat Industry* inakuwa ni *superfluous,* tunakuwa tunaongeza kitu ambacho tayari kimekuwa *taken care off*. Ni kwa sababu ni Muswada wa nyama na *Annual Councils* zinaweza kuwepo kama alivyoeleza vizuri sana Mheshimiwa Mbunge asubuhi, kwa ajili ya madhumuni mengine lakini kwa madhumuni ya Muswada huu, unaporuhusu Muswada huu *Annual Council* hii itahusika na *Meat Industry* siyo kitu kingine chochote. Sasa kwa kweli nashindwa kuelewa kwa nini tuongeze maneno mahali ambapo tunaweza tuka-*serve* kwa kusoma dhana yenyewe nzima na Muswada wenyewe. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri. Mimi nilikuwa nataka *clarity* ya kitu ambacho tunafanya ndiyo hiyo tu. Nilikwenda kwenye madhumuni, umeandika Baraza la Mwaka la Wadau wa Sekta Ndogo. Mbona hukuandika Baraza la mwaka tu halafu ukaacha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shellukindo umesikika.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 5

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jedwali la marekebisho kifungu B Mheshimiwa Waziri amefanya marekebisho ya *Clause* 9 (1) *paragraph* (i) kwa kuondoa neno *public* kwenye *Public University*. Sasa nilitaka nimwelewe kwamba alitaka kubadilisha hiyo tu au alitaka vile vile katika *Clause* 5 (1) (j) ambayo vile vile ina *Public University of Agriculture?*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani inawezekana wamesahau kutoa. *Public* tulitoa kwenye sehemu zote mbili.

**MWENYEKITI:** Tunaomba *clarification* ndogo tu kwa Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba una-*move* kwamba *amendment* kwamba neno *public* liondoke hapo ndicho unachotuambia?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Ndiyo kwenye (j).

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Mabadiliko yake)*

Kifungu cha 6
Kifungu cha 7
Kifungu cha 8

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 9

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi. Lakini pili, nikiri kwamba mimi sijapokea *schedule of amendments.* Kwa hiyo, nasema limeshughulikiwa? Utaniwia radhi na utaniongoza. Langu ni dogo tu kwenye kifungu Na. 9.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, kwa taarifa tu ni kwamba iligawiwa asubuhi pamoja na *Order Paper.* Lakini endelea.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Katika ukurasa wa saba pale Na. 9 nimeangalia *composition* ya Bodi, uko mlolongo wa wale watu ambao wanatakiwa kuwa kwenye Bodi inayohusika.

*Concern* yangu kama nilivyoandika kwenye mchango kwa maandishi ukiangalia pale, maana yake ni kwamba, hakuna nafasi ya Mbunge au mwanasiasa yeyote kuwa kwenye *composition* ya ile Bodi. Sasa mimi najiuliza, hiki ni chombo cha umma, sisi ni Wabunge tuko hapa tumechaguliwa na wananchi tusimamie Serikali kwa karibu zaidi.

Njia mojawapo ambayo imekuwa ikitumika hadi sasa inatumika ni kwamba Wabunge wanakuwepo katika Bodi mbalimbali hasa zile taasisi zinakuwa *owned* na Serikali kama hii itakavyokuwa. Sasa nashangaa pale hata lugha tu ya kubabaisha ya kumwachia liwe Waziri anayehusika angalau akaangalia uwezekano wa kumteua Mbunge yeyote ama wa kutoka Shinyanga, Mwanza na kadhalika, wale wafugaji wakubwa hakuna. Yaani imefungwa kabisa hakuna nafasi yeyote ya Waziri?

Hii sasa unisamehe imekuwa *trend* ya Miswada mingi inayokuja hapa ya mambo kama haya kwamba nafasi ya Mbunge kwenda kusimamia kwa karibu imekuwa ikiondolewa. Imeonekana kuna jitihada za makusudi za wenzetu hawa Serikali kufifisha uwakilishi na jitihada za Wabunge kusimamia mambo kama haya. Mimi ningependa kupata maelezo, ni sababu zipi za msingi ambazo Muswada huu kwenye *composition* hii hapa haina *provision* hata ya kuruhusu Waziri kuwa akiona kwamba anafaa Mbunge yeyote aweze kumweka? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemwelewa Mheshimiwa Missanga, lakini napenda nitofautiane naye kidogo kwa sababu, mfano tumesema hapa *a member represent meat processors* na tukatoa mfano. Mfano Mheshimiwa Mzindakaya ana-*process* nyama, pili upande wa (f*) one member representing meat consumer,* Mheshimiwa Missanga ni *meat consumer* wa nyama. Sasa *unless* aniambie kwamba asingependa yeye kuwa *considered* kama *meat consumer*.

Kwa hiyo, Waziri hakufungwa na mara kwa mara kumetumika busara. Waheshimiwa Wabunge wengi tu wako hapa ambao wanaingizwa kwenye Bodi licha ya kwamba wakati mwingi unakuta kwamba sheria inatungwa haiku-*specify specifically* kwamba ni mjumbe kutoka kwenye Bunge hili Tukufu. Mara kwa mara busara inatumika kwa sababu tunapenda mchango wa Waheshimiwa Wabunge ndani ya Bodi na maeneo mengi Wabunge wametumika.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na pia nashukuru maelezo ya Mheshimiwa Waziri. Kwanza, kimsingi anakubali kwamba upo umuhimu wa Waheshimiwa Wabunge kushiriki katika vyombo kama hivi, ndivyo nilivyomwelewa. Kwa busara yake ndiyo amenionyesha vile vifungu ambavyo kwa kweli inategemeana na busara ya Mheshimiwa Waziri mwenyewe. Kama Diallo busara zake zinamtuma kutumia vifungu hivi viwili kama *consumer* wa nyama, sasa ime-*happen* kama Mheshimiwa Mzindakaya anashiriki. Lakini inaweza ikafika Bunge ambalo hamna hata mtu mmoja ambaye ana kiwanda cha nyama hapa, hiyo itamnyima Waziri anayehusika kuangalia uwezekano.

Sasa kuna ubaya gani kuonyesha bayana hapa kuweka kifungu ambacho angalau kiko bayana cha kuonyesha hiyo? Kuna tatizo gani? Hivi kuna uwoga gani wa kuwahusisha Wabunge katika vyombo kama hivi ili waweze kutekeleza majukumu yao waliyopewa kwa mujibu wa Katiba ya kuisimamia Serikali kwa karibu? Kuna tatizo? Kuna ubaya gani wa kuonyesha bayana hapa mpaka ikae kwenye kificho kificho hapa kwamba anaweza akatumia? Tukimpata Waziri ambaye hana busara kama alivyo Mheshimiwa Diallo itakuwaje? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Missanga na Waheshimiwa Wabunge, mimi nadhani suala hapa ni *concern* ya Wabunge kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na natumaini imeshafika kwamba sheria nyingi zinazotungwa hapa hazitoi nafasi kwa Wabunge kuteuliwa kuwa wajumbe wa Bodi mbalimbali. Ni *trend* ambayo imeonekana, ni tabia ya kawaida. Kwa hiyo, ni *concern* ambayo imeshafika, naamini kabisa imesikika.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 10

**MHE. WILLAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *clause* ya 10 (h) ukurasa wa nane nilitaka Waziri apatazame kwamba hii sheria ilivyo pale (h) panaposema: *"To develop implementation and monitor strategies."* Nadhani hapa lugha kwa kweli haikukaa sawasawa. Ingekuwa: *"To develop implement and monitor strategies*." Halafu kwenye *clause* 10 (l) hapo ukisoma hiyo sentensi kuna maneno hapa yamekaa bila kukosekana koma na mimi ninawaheshimu sana Mheshimiwa *Attorney General,* anatuambia *comma matters a lot,* sasa pale kuna *comma* inakosekana, *second sentence, and large scale livestock producers traders* kuna *comma* hapo. *Livestock producers, trade and meat processors,* kama anakubaliana nayo ni hiyo tu kwamba usije ukatoka Muswada huu na haya makosa na mimi nitahusika kwenye hayo.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Sawa, Mheshimiwa Shellukindo, amenitumia busara zake na elimu yake ya juu ya masuala haya. Ni kweli ni: *"To develop implement and monitor."* Ni sahihi kabisa alivyosema na pale kuna *comma* tena hata mimi hapa kwenye *copy* yangu nimeiweka mwenyewe. Nakubali, lakini hata hivyo masahihisho madogo kama haya nadhani kuna sheria inamruhusu Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakati anatengeneza Muswada kurekebisha *typographic errors.*

*(Kifungu kilichotajwa hapo kilipitishwa na Kamati ya Bunge zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 11
Kifungu cha 12
Kifungu cha 13
Kifungu cha 14
Kifungu cha 15
Kifungu cha 16

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 17

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kifungu namba 17 (1) kwanza nataka kukiri maelezo ya kina yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri, ameniridhisha sana. Natumaini pia wafugaji waliomsikia wameridhika. Zaidi inapokuja kwa watu ambao wanapeleka ng'ombe zao kwenye Minada kwamba hawatasumbuliwa kwamba hawana kibali, hawana leseni kutoka kwa Bodi ambayo wameitaja. Lakini ukiisoma hiyo *section* unaona kwamba *no person shall carry on the business of a livestock producer.* Hapo mimi ndiyo kidogo napata matatizo. Unasema ni wakati gani ni

*business* ya kuzalisha ng'ombe, maana akisema *livestock keeper* labda ningeelewa vizuri. Lakini inapokuwa *business of livestock producer* ni wakati gani ni *business?* Hapa ndiyo inanipa shida kwamba huenda hii haitatekelezeka au ikitekelezeka wafugaji wengi sana wanaweza wakawa ni lazima akiwa na ng'ombe 500 hata kama anaziweka tu na baadaye aziuze itabidi lazima wajiandikishe au waandikishwe na Bodi. Sasa hii inanipa taabu.

Ningependa kama yeye angeniambia kwamba ataweka kwenye *regulation* kutoa *limitation,* yaani kiasi fulani ndiyo anakuwa anaangaliwa kama ni mtu wa biashara au kiasi fulani siyo cha biashara, hapo ningeona kwamba labda inasaidia wafugaji. Hii nazungumzia kwa sababu leo yeye ni Waziri, kesho siyo Waziri wa sehemu hii, mtu mwingine atakuja kusoma hii halafu watu wetu watapata matatizo sana. Unajua watu wanavyopenda kukamata wengine hii inaweza kukawa chanzo cha kamata kamata kwa kila mmoja aliye na ng'ombe. Naomba maelezo ya kina zaidi.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona *concern* ya Mheshimiwa Mbunge, lakini kama nilivyoeleza *the business of livestock producer,* tunaposema *business automatically* tunamu-*exclude* huyu ambaye ni mfugaji wa kawaida wa kienyeji. Huyu *business producer* au *livestock producer* Mheshimiwa Cheyo atakuja huyu atakayenunua mifugo anenepeshe auze. Yule anaingia moja kwa moja kwa sababu dhamira yake ni kwa ajili ya kuzalisha kwa ajili ya biashara. Sasa mwenyeji na kama unavyoshauri tutaangalia kwenye kanuni tuhakikishe kwamba amekuwa *excluded* huyu mwenyeji. Ahsante. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge zima bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Malima hukusimama mwanzo na kama ulisimama sikukuona. Kwa hiyo, kwa utaratibu ule ule wa ruhusa ya Mwenyekiti, endelea Mheshimiwa Malima.

**MHE. ADAM K. A. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. *Concern* yangu ni kwamba ,jana wakati wa semina tuliambiwa kwamba ni vizuri sheria hizi zikawa zinaangalia pia utekelezaji wake kama sheria. Sasa tafsiri ya *livestock producer* hapa ipo na ukitaka kupata *register* ya *livestock producer* bila kuwa na *quantification* ya namna yoyote, hii sheria itakuwa inakuwa na ugumu kidogo katika utekelezaji wake ndiyo maana nilikuwa nataka kumwuliza Waziri, isingekuwa vizuri zaidi kwamba hii *registration* ikawa imefunga kwenye *no person shall carry on the business of a livestock trader or livestock market operator,* hii *producer* ikawa imekaa kwenye hatua ambayo hata mtu kama ana ng'ombe wawili/watatu, basi haihitaji kuwa na *registration,* maana anaweza kuwa ana ng'ombe wake watatu halafu hajafanya bado maamuzi ya kuwauza, lakini akafika hatua siku moja hali ikikamata akaamua kuwauza.

Sasa *at what stage does he become a livestock producer intending to produce for business?* Sana sana ili sheria yenyewe iwe ni *workable,* kwa nini Waziri asikubali kwamba ikawa tu *on the business of a livestock trader or livestock market operator,*

ikawa kwamba *registration* ianze pale mtu anapokusudia kumuuza ng'ombe wake au anapozalisha kwa makusudio ya kupeleka sokoni *or something*. Nilikuwa nauliza tu utendaji wa kipengele hiki utekelezaji wake unakuaje? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nikumbushe taratibu na kanuni zetu kwamba katika hatua hii hairuhusiwi ku-*move amendment.* Ni vizuri tukaelewana. Ukitaka ku-*move amendment* kuna utaratibu wake ambao inatakiwa uwe umeshauchukua kabla ya hatua hii. Lakini kwa vile tunakwenda kwa kujifunza. Mheshimiwa Waziri kama una cha kusema.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza, Mheshimiwa Malima anajaribu kuleta dhana ambayo sijui mimi nimekaa *trade*, *trade* inaanza pale *production* inapoishia. Sasa huyu *producer normally* anakuwa na *intention*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukishaanza kusema ni *business producer* au ni *commercial producer definitely* anakwenda mwisho ku-*trade*. Ile *transaction* atakayoifanya ya *exchange of goods* ni *trade*.

Kwa hiyo, kama nilivyoeleza wakati nampa maelezo ya ziada Mheshimiwa Cheyo kwenye kanuni, tutajitahidi ku-*exclude definition* zaidi, tutajaribu kui-*exclude* wale ambao hawahusika kabisa kama hawa wafugaji wa kienyeji ili tuweze kukidhi kwa sababu tukiweka unavyo-*suggest* Mheshimiwa Malima, ina maana tutakapofikia lengo ambayo *vision* yetu ni kuona kwamba wafugaji wote *eventually* watafuga kibiashara na ndiyo nchi za wenzetu walivyo, kama ni biashara itakuwa unafuga kwa ajili ya ku-*produce* maziwa ya kuuza, utakuwa unafuga kama ni kondoo kwa ajili ya kuuza manyoya, kama ni ng'ombe wa nyama ni kwa ajili ya kuuza nyama. Sasa ina maana itabidi urudi Bungeni.

Sasa kama nilivyoomba, tuachie tutaangalia kwenye kanuni ku-*exclude* kwa sababu naelewa wanaozungumzwa na *quantification* ambayo anahitaji Mheshimiwa Malima. Ni kweli tusipoiweka vizuri kwenye kanuni inaweza kuleta *confusion* kidogo. Lakini kama tutakubali hilo litokee kwa sababu kanuni tutazipitia vizuri zaidi, *eventually* kanuni Wabunge pia wanakuja kuziona mwisho wa safari, Kamati ya Sheria na Katiba.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 18
Kifungu cha 19
Kifungu cha 20
Kifungu cha 21
Kifungu cha 22
Kifungu cha 23
Kifungu cha 24
Kifungu cha 25

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 26

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni suala la ufafanuzi tu ili niwe na uhakika kwamba tuko pamoja 26 (d) *income derived from investments,* kwa maana ya Muswada huu ni *investments* zipi?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ku-*create fund* Mfuko wowote ule, kawaida ya anayetengeneza mfuko anauacha wazi ili yeyote anayeweza kutupia ndani ya mfuko atupie. Sasa tunazungumza, kuna maeneo mengine *investors* wanaweza ku-*shy away* kutokuingia kwenye shughuli fulani ambao wanaona ina hasara. Sasa *temporarily* mfuko huu ukatumika ku-*hague,* baada ya muda zile pesa ambazo zitarudishwa *definately* lazima ziwe *accepted* kama zimetoka kwenye *investment.* Lakini ni kitu ambacho kinawekwa tu kama kupanua wigo wa *income* ya mfuko. Kwa hiyo, kwa maelezo hayo ya hii (d) ni *income* yoyote ambayo inaweza kuwa *derived from investment.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kaboyonga ameridhika.

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na Mabadiliko yake)*

Kifungu cha 27
Kifungu cha 28
Kifungu cha 29

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 30

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 30 na kifungu kidogo cha (5) wakati ambapo mimi nachangia pamoja na Mheshimiwa Shellukindo, tuliweka tahadhari kwamba hizi hesabu lazima ziletwe Bungeni kwa sababu tunatoa fedha kwa hii Bodi.

Hakuna mahali hapa ambapo inamtaka Waziri kuweka haya mahesabu kwenye Meza ya Mheshimiwa Spika, mpaka Waziri kuweka haya mahesabu kwenye Meza ya Mheshimiwa Spika. Nataka maelezo.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kifungu hiki kinajaribu kuweka utaratibu wa Bodi itakavyotoa taarifa zake. Lakini bado Waziri chini ya Sheria nyingine ya mashirika inamtaka taarifa ya Bodi

kuileta, kui-*table* kwenye Bunge kama tunavyofanya kila siku, mashirika ambayo yako kwenye Mashirika ya Umma, kwenye Sheria ya Mashirika ya Umma. Kwa hiyo, sioni tatizo lolote. Nadhani hii ni Bodi, jinsi inavyoripoti taarifa zake za mahesabu kwenye ile *Council* ambayo ndiyo *source* ya kile chanzo ya ile *formation* ya ile Bodi, ni kwa ajili ya taarifa tu. Lakini bado haimkatazi hapa Waziri kuleta taarifa hiyo, kui-*lay* kwenye *table* kama ilivyo kwa sheria ya mashirika ya umma.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Waziri akisema atarekebisha hiyo kwenye *regulation* sina matatizo. Lakini kuachia tu kwamba ni *description* au ni uamuzi wa Waziri *whether* ataleta asilete, mimi naona Sheria haitoshelezi kuhakikisha kwamba tunafanya kazi yetu kama Bunge la kudhibiti matumizi ya Serikali.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna *description* hapo. *Copy* inapoletwa kwa Waziri maana yake inaletwa taarifa hiyo kuwa *tabled* Bungeni na ndiyo utaratibu Mheshimiwa Cheyo. Nalifahamu hili kwa sababu Sheria nyingi zina utaratibu huu huu kwamba *copy of audited report* inapelekwa kwa Waziri halafu taarifa ile *inventually* inakuwa *tabled* kwenye *House.* Ni utaratibu. Sio *description,* ni lazima.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamatiya Bunge zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 31
Kifungu cha 32

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 33

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 34

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo ya Waziri, wakati nikitoa maeneo ambayo niliona kwamba yanahitaji kuangaliwa katika *clause 34,* ile sentensi ya kwanza nilitaka tu kutahadharisha kwamba neno *advise and advice* mara nyingi yanachanganya watu sana. Sasa hapa nadhani inatakiwa ni *advice.*

**MWENYEKITI:** Unachosema ni ‘c’ badala ya ‘s’ kwenye neno *‘advice’.*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Sawa! Ni Kiingereza tu. Ni ‘c’.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge zima bila ya marekebisho yoyote)*

Kifungu cha 35
Kifungu cha 36

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge zima pamoja na marekebisho yake)*

Jedwali la 1

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge zima bila marekebisho yoyote)*

Jedwali la 2

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge zima bila marekebisho yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Nyama wa Mwaka 2006**
***(The Meat Industry Bill, 2006)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kuwa, baada ya Kamati ya Bunge Zima kuupitia Muswada wa Sheria iitwayo *The Meat Industry Act, 2006* kifungu kwa kifungu pamoja na mabadiliko yake na kuupitisha kama ulivyo, hivyo basi, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa *The Meat Industry Act, 2006* sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja ilitolewa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, katika utaratibu wetu wa kutunga Sheria, Muswada huu wa Sheria ya Nyama wa mwaka 2006 umepita hatua zote za Bunge na umeafikiwa katika hatua zake zote.

Kwa hiyo, kinachofuata ni hatua za kwenda katika kumpelekea Mheshimiwa Rais ambapo utaratibu wake utatolewa taarifa baadaye katika kikao kijacho na Mheshimiwa Spika.

Kwa kuwa hatuna matangazo yoyote mengine na shughuli zilizopangwa katika *Order Paper* ya leo zote zimekamilika. Basi nachukua nafasi hii kuahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.39 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne, Tarehe 7 Novemba, 2006 Saa Tatu Asubuhi)*